**Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA MBILI

**Kikao cha Thelathini na Nne - Tarehe 29 Julai, 2003**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaanza kuna masahihisho ya *Order Paper* ile *agenda* namba tatu inayoonyesha Kauli za Mawaziri. Mheshimiwa Waziri mhusika ameomba kauli hiyo aitoe kesho badala ya leo. Kwa maana hiyo, *Order Paper* ya leo *agenda* hiyo haipo itaonekana kwenye *Order Paper* ya kesho.

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:**

Taarifa ya Mwaka ya Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha kwa mwaka 2001/2002 *(The Annual Report of the Arusha International Conference Centre (A.I.C.C.) for the year 2001/2002).*

Hotuba ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa mwaka 2003/2004.

**MHE. DR. WILLIAM F. SHIJA - MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NCHI ZA NJE:**

Taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje, kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, katika mwaka uliopita, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2003/2004.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 329

### Matatizo Yaliyopo katika Kituo cha Afya cha Nanyumbu

**MHE. ARIDI M. ULEDI** aliuliza:-

Kwa kuwa Kituo cha Afya cha Nanyumbu kinakabiliwa na matatizo kadhaa yakiwemo ya upungufu wa wafanyakazi na ukosefu wa umeme wa aina yoyote; na kwa kuwa matatizo hayo yamekuwepo kwa muda mrefu sasa:-

(a) Je, ni lini Kituo hicho kitapatiwa wafanyakazi wa kutosha ili kuboresha huduma zake kwa wananchi?

(b) Je, ni lini Serikali itakipatia Kituo hicho umeme?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aridi Uledi, Mbunge wa Nanyumbu, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiw Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Masasi ina Hospitali ya Wilaya moja, Vituo vya Afya vinne na Zahanati 39. Upungufu wa Watumishi katika Wilaya hiyo ni 261, upungufu huo kwa upande wa Wilaya ni wanane, kwa upande wa Vituo vya Afya ni 21 na Zanahati ni watumishi 25. Kwa mujibu wa takwimu zilizopo Kituo cha Afya cha Nanyumbu kwa sasa kina jumla ya watumishi wa Afya nane na kwamba kina upungufu wa watumishi watano kama ifuatavyo:- Afisa Afya Msaidizi mmoja, Muuguzi mmoja, Muuguzi Msaidizi mmoja, Mchanganya dawa mmoja na Msaidizi wa Maabara mmoja.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Masasi ilikwishaomba kibali cha kuajiri watumishi wapya kwa barua namba *MDC/S/20/1/vol.300/21* ya tarehe 22 Mei, 2002 ili iweze kuajiri watumishi wapya kukabiliana na tatizo la upungufu wa watumishi hao. Kibali hicho bado hakijapatikana na Halmashauri inaendelea kufuatilia.

(b) Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Masasi kwa sasa haina mpango wa kupeleka umeme katika Kituo cha Nanyumbu. Juhudi za Halmashauri ya Wilaya hiyo kwa kiasi kikubwa zinategemea sana mpango wa Shirika la Taifa la Umeme *(TANESCO)* wa kusambaza umeme katika Wilaya hiyo ya Masasi. Hata hivyo, Kituo cha Afya cha Nanyumbu na vinginevyo, kila mwezi hupata mgao wa mafuta ya taa kwa ajili ya kuchemsha vifaa mbalimbali na pia kutolea huduma nyingine wakati wa usiku kwa kutumia taa za kandili. Aidha, kituo hicho kina jokofu linalotumia gesi kwa ajili ya kuhifadhia dawa mbalimbali katika Kituo.

**MHE. ARIDI M. ULEDI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa Kituo cha Afya cha Nanyumbu kinahudumia wagonjwa mbalimbali wakiwemo wale ambao wamejeruhiwa na wanyama wakali kama Simba, Chui, Tembo na Mamba kutoka Hifadhi ya Lukwika Lumesule; na kwa kuwa Kituo hicho hivi sasa hakina gari la wagonjwa. Je, Serikali itakipatia lini Kituo hicho gari la wagonjwa?

(b) Kwa kuwa matatizo ya Kituo cha Afya cha Nanyumbu yanafanana sana na yale ya Kituo cha Afya cha Michiga. Je, ni lini Serikali basi itahakikisha matatizo haya katika Kituo cha Afya cha Michinga nayo yanapatiwa ufumbuzi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la tatizo la gari katika Kituo cha Afya cha Nanyumbu, Serikali kwa ujumla bado inafanya juhudi kubwa kutafuta usafiri wa magari si kwa ajili ya Kituo hicho cha Afya peke yake, lakini kujaribu kukidhi haja ya tatizo hili kwa Kitaifa kwa ujumla. Tunaamini mafanikio yatapatikana kwa kuwa tunaendeleza juhudi hizo kwa nguvu sana. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira kidogo tuone namna gani tatizo hilo litaweza kumalizika.

Lakini kuhusu swali lake la pili, labda niseme tu kwamba tatizo la watumishi kama ambavyo tumekuwa tunasema muda wote katika Sekta ya Afya ni kubwa na kwa taarifa ya Mheshimiwa Mbunge kwa Wilaya ya Masasi nzima tuna upungufu wa watumishi karibu 54 bado hatujaweza kufikia haja inayohitajika. Kwa hiyo, tunaendelea na juhudi na tuna hakika vile vile tutafanikisha.

**SPIKA:** Swali la msingi linahusu Kituo cha Afya cha Nanyumbu. Sasa Vituo vya Afya vingine yatakuwa ni maswali mapya.

**MHE. PAUL E. NTWINA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Kituo cha Afya cha Nanyumbu hakina *Solar Power* ambayo haifanani na kununua mafuta kila siku ya taa za kandili na mishumaa. Je, kwa Vituo vyote vinginevyo Serikali itaweza kuvipatia Vituo hivyo *Solar Power* hasa Kituo cha Afya cha Nanyumbu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ni wajanja sana! *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ushauri wa Mheshimiwa Mbunge ni mzuri na napenda kumjulisha tu kwamba baadhi ya Halmashauri zimefanya juhudi hizo na zikaweza kuweka *Solar Power* katika Vituo vyao vya Afya na hata kwenye Zahanati. Kwa hiyo, tutakachofanya tutamwomba Mheshimiwa Aridi Uledi, ashauriane na Halmashauri yake kuona kama uwezekano huo upo. *(Kicheko)*

Na. 330

**Ujenzi wa Nyumba kwenye Fukwe za Bahari ya Hindi**

**MHE. PETER KABISA** aliuliza:-

(a) Je, ni sheria zipi kwa sasa zinafuatwa kuhusiana na umbali unaotakiwa kuzingatiwa na mipango Miji, kuhusu ujenzi wa nyumba za watu binafsi na ni nyumba za ghorofa binafsi ngapi zinaruhusiwa kujengwa karibu na fukwe za Bahari ya Hindi?

(b) Je, viwanja 117 hadi 120 na viwanja 126, 127 vilivyoko *Jangwani Beach* vinakidhi vipi sheria hizo, kama vinaruhusiwa kujengwa nyumba kwa mujibu wa umbali toka kwenye fukwe za Bahari?

(c) Je, Serikali inatamka nini juu ya viwanja hivyo na je, kwa kuzingatia sheria za mipango Miji na *Safer Cites,* Serikali itakubali kuvifanya viwanja hivyo viwe vya burudani?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Peter Kabisa, Mbunge wa Kinondoni, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, sheria zinazosimamia ujenzi wa umbali kutoka kwenye fukwe za Bahari na maziwa unaotakiwa kufuatwa ni sheria ya mipango Miji sura ya 378 ya mwaka 1960 na sheria ya Ujenzi Mijini sura ya 101 ya mwaka 1920. Lakini vile vile ipo sheria ndogo ambayo imetangazwa katika Tangazo la Serikali namba 76 la mwaka 1992 *(Public Beaches Planning Area, Order of the Year 1992),* chini ya kifungu cha 6 cha *order* hiyo umbali unaotakiwa kuachwa wazi wakati wa kufanya ujenzi kwenye fukwe za bahari ni mita zisizopungua 60 kutoka kwenye alama ya mwisho ya maji ya kujaa *high water mark.*

Eneo hili linatakiwa litumike kwa hifadhi ya mazingira na shughuli za ufukweni ambazo ni pamoja na uvuvi, kuogelea, na shughuli nyinginezo kama hizo. Aidha, sheria nilizokwisha kuzitaja, zinaelekeza kuwa nyumba binafsi zinazoruhusiwa kujengwa kwenye maeneo ya fukwe za Bahari ya Hindi hazipashwi kuzidi ghorofa tatu na kwamba hatimiliki ya viwanja katika maeneo hayo hutoa barua ambayo vilevile inaelekeza matumizi mengine au masharti mengine

(b) Mheshimiwa Spika, viwanja 117 hadi 120, na viwanja 126, 127 ambavyo vipo kwenye ufukwe wa Bahari ya Hindi, ni nyumba za makazi ya watu zenye ghorofa moja moja. Wakati wa upimaji wa viwanja namba 117 hadi 120 umbali wa mita 60 ulizingatiwa kama Sheria inavyoelekeza. Lakini

kutokana na mabadiliko mbalimbali katika hali ya hewa kumekuwepo na mmomonyoko wa ufukwe na hivyo kufanya baadhi ya maeneo kuonekana kwamba haviko ndani ya umbali wa mita 60.

Viwanja namba 126 na 127 viko umbali wa mita 110 kutoka ufukwe wa bahari na kwa hiyo viko ndani ya alama zilizowekwa. Viwanja hivyo vilipimwa na kugawiwa na kuendelezwa kabla ya sheria ndogo 1992 haijaanza kutumika. Lakini kifungu cha 8 cha sheria hiyo hiyo ndogo kinaelekeza kwamba nyumba zote zilizojengwa wakati huo zitaendelea kuheshimika hadi hapo itakapoelekezwa vinginevyo.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kwamba viwanja hivyo vilitengwa kwa matumizi ya makazi. Napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa maeneo ya burudani hutengwa kwa mujibu wa mipango iliyobuniwa na kuidhinishwa na Halmashauri husika chini ya sheria ya mipango Miji, sura ya 378 ya mwaka 1960 na sheria ndogo iliyomo katika Tangazo la Serikali Namba 167 ya mwaka 1994 iliyotungwa chini ya sheria ya Viwanja vya Umma vya Burudani Sura ya 320. *(The Public Recreation Grounds Ordinance - Cap. 320).*

Hivyo,endapo Serikali itapokea maombi ya kubadilisha matumizi ya ardhi kwa ajili ya viwanja hivyo basi taratibu za kubadilisha matumizi haya zitazingatiwa.

Na. 331

**Miradi ya *HIPC***

**MHE. HERBERT J. MNTANGI** aliuliza:-

Kwa kuwa Mkoa wa Tanga ni miongoni mwa Mikoa 12 iliyoingizwa katika mpango wa kukarabati barabara zake chini ya Miradi ya *HIPC:-*

(a) Je, ni barabara zipi na madaraja yapi yameingizwa katika mradi huo kwa Wilaya ya Muheza?

(b) Kwa kuwa daraja katika barabara ya Kicheba hadi Kwalubuye iliharibiwa kabisa na mvua za *El-Nino* na Halmashauri ya Wilaya ya Muheza imekosa uwezo wa kulijenga upya na kufanya sehemu ya barabara hiyo kufungika kwa miaka mingi; je, Serikali haioni haja ya kusaidia ujenzi wa daraja hilo kwa Mpango huo wa *HIPC?*

(c) Iwapo barabara ya Mashewa-Kimbo-Potwe hadi Maguzoni haipo katika mradi wa *HIPC;* na kwa kuwa barabara hiyo ni muhimu sana kiuchumi na katika kuunganisha Wilaya ya Muheza na Wilaya ya Korogwe; je, Serikali itakuwa tayari kuongeza barabara hiyo katika mradi huo kwa Wilaya ya Muheza?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mbunge wa Muheza, naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, chini ya mpango wa msamaha wa madeni kwa nchi maskini *(HIPC),* sekta ya barabara chini iliteua Mikoa kumi na mbili ambayo ilionekana ni maskini zaidi Kitaifa ili baadhi ya barabara zake za Mkoa na za Wilaya ziweze kufanyiwa matengenezo makubwa. Lengo la kufanya matengenezo hayo lilikuwa ni kufufua mawasiliano katika maeneo muhimu ya uzalishaji ili hatimaye uchumi wa maeneo husika uwezi kuboreshwa na hivyo kutimiza lengo la kupiga vita umaskini.

Kwa kuwa Serikali imepatiwa msamaha wa madeni yake mengi chini ya Mpango wa *HIPC,* hii inaiwezesha sasa kuboresha zaidi Bajeti yake kwa sekta ya barabara ili kutimiza malengo ya mradi wa *HIPC.* Kwa hiyo basi, kuanzia mwaka wa fedha 2002/2003 suala hilo limezingatiwa kwenye Bajeti ya Serikali, hivyo ni jukumu la watendaji wote sasa kuendelea na utekelezaji wa barabara zilizopendekezwa chini ya mradi wa *HIPC* kulingana na Bajeti inayotengwa mwaka hadi mwaka. Ni dhahiri kutakuwa na tofauti kati ya malengo ya awali na utekelezaji halisi kulingana na mwenendo wa bajeti, hivyo kulazimu kazi kufanyika kwa vipaumbele.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo ya utangulizi, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mbunge wa Muheza, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, barabara zilizoingizwa katika mradi wa *HIPC* kwa Wilaya ya Muheza ni pamoja na barabara ya Muheza- Amani ambayo ni ya Mkoa itakayojengwa kwa kiwango cha lami kilometa 22.4. Barabara hii imekadiriwa kugharimu shilingi bilioni 2, ambazo Wizara yangu inaendelea kuzitafuta. Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Muheza iliingiza barabara zenye jumla ya urefu wa kilometa 132.3. ambazo ni Mtindiro-Kwabota-Bagamoyo (kilometa10), Mtindiro - Kwale-Monga (kilometa 6), Mamboleo - Bwembwera - Nkumba (kilometa 9.05), Darajani - Kambai - Mhinduro (kilometa 16.3), Stakishari - Mkinga - Magodi (kilometa 15.5), Zigi - Kwendumi (kilometa 9), Kicheba - Paramba - Mlingano (kilometa 12), Doda - Pamba (kilometa 4.8), Mwakijembe - Daluni (kilometa 33), Gezani - Tawalani (kilometa 4) na barabara Kuu hadi Kwakifua (kilometa 10). Barabara zote hizi zinakadiriwa kugharimu shilingi milioni 925.470

(b) Serikali inauona umuhimu wa kujenga daraja katika barabara ya Kicheba hadi Kwalubuye kupitia mpango wa *HIPC,* lakini kama nilivyoeleza awali, mpango huu ulizihusisha Halmashauri za Wilaya katika kuandaa na kupendekeza barabara ambazo zingejengwa au kutengenezwa.

Aidha, Mheshimiwa Mbunge atakubaliana nami kwamba suala hili ni vyema akalipeleka mbele ya Halmashauri ya Wilaya ya Muheza ili lishughulikiwe katika taratibu za mradi wa *HIPC* au litafutiwe ufumbuzi kwa kutumia vyanzo vingine vya mapato ikiwa ni pamoja na *Road Fund* ili liweze kutekelezwa.

(c) Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwishaeleza katika sehemu (b) ya jibu langu kuwa lilikuwa ni jukumu la Halmashauri ya Wilaya ya Muheza kuamua ni barabara zipi zipendekezwe katika mradi wa *HIPC,* hivyo kwa kutumia utaratibu huu barabara ya Mashewa -Kiuta - Poture hadi Maguzoni ingeweza ikapendekezwa humo. Hata hivyo, barabara hii inaweza ikafanyiwa matengenezo kwa kutumia vyanzo vingine vya mapato kulingana na umuhimu wake kwa Wilaya.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu mazuri aliyoyatoa katika swali hili. Hata hivyo, ningeomba kuuliza swali dogo tu moja la nyongeza.

Kwa kuwa ilitokea bahati mbaya kwamba barabara hii ya Mashewa- Kibo- Poture ambayo pia inaunganisha barabara ya Mkoa inayotoka Korogwe Miyuzi hadi Maguzoni haikuingizwa katika mpango huu. Je, bado Wilaya ya Muheza inayo nafasi ya kuweza kufanya marekebisho ili kuiingiza barabara hii muhimu sasa?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa barabara hii hakuingizwa kwenye mpango huu na Wilaya sasa kama inaona ni muhimu kabisa barabara hii sasa iwekwe kwenye mpango huu na kwa sababu mpango ukwishapangwa itabidi watoe barabara nyingine ili kusudi waweke barabara hiyo.

Na. 332

**Barabara ya Kolandoto - Bariadi**

**MHE. PAUL N. MAKOLO** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara ya kutoka Kolandoto- Mhunze- Lalago -Maswa-Bariadi, ni muhimu sana katika kusafirisha mazao ya biashara na usafiri kwa wakazi wa maeneo hayo; na kwa kuwa kipindi kirefu sasa barabara hiyo haijafanyiwa matengenezo ya kuimarisha; je, Serikali ina mpango gani wa kuitengeneza barabara hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Paul Makolo, Mbunge wa Kishapu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kolandoto-Lalago-Maswa-Bariadi ni barabara ya Mkoa inayohudumiwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara *(TANROADS)* Mkoa wa Shinyanga na ni kiungo muhimu katika kusafirisha mazao ya biashara na usafiri kwa wakazi wa maeneo yanayotumia barabara hii. Barabara hii ilijengwa kwa kiwango cha barabara kuu na kwa muda mrefu sasa haijapata matengenezo maalum *(Periodic Maintenance)* kutokana na ufinyu wa Bajeti ya Serikali.

Hata hivyo, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara wa Mkoa wa Shinyanga, imekuwa ikiifanyia matengenezo ya kawaida na matengenezo ya maeneo korofi kwa lengo la kuifanya ipitike wakati wote.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2002/2003, Wizara yangu kupitia Ofisi ya Meneja wa Mkoa Wakala wa Barabara *(TANROADS)* iliendelea kuifanyia barabara hiyo matengenezo ya kawaida ambayo yalihusisha kufukua mifereji, kuchonga na kuweka changarawe kwenye maeneo korofi kwa gharama ya shilingi milioni 161.5. Matengenezo haya yalifanyika katika maeneo yafuatayo:-

Katika barabara ya Kolandoto hadi njia panda ya Ukenyenge yenye urefu wa kilometa 15, matengenezo yamekamilika na kugharimu shilingi milioni 30, Lalago-Maswa yenye urefu wa kilometa 35, matengenezo yamekamilika na kugharimu shilingi milioni 32, Bariadi-Sapiwi yenye urefu wa kilometa 54.5, matengenezo yamekamilika kwa kugharimu shilingi milioni 36.5.

Aidha, barabara ya njia panda ya Ukenyenge -Lalago, matengenezo yanaendelea kwa gharama ya shilingi milioni 45 na barabara ya Maswa - Bariadi, yenye urefu wa kilometa 5, matengenezo pia yanaendelea kwa gharama ya shilingi milioni 18.

Mheshimiwa Spika, kwa matengenezo hayo, Wizara yangu inaamini kuwa barabara hii inapewa uzito unaostahili ili kukidhi mahitaji ya usafiri na usafirishaji kwenye maeneo husika ingawaje fedha hazitoshelezi sasa.

**MHE. PAUL N. MAKOLO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kuuliza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa sehemu zinazolima kahawa na kadhalika barabara zake zinahudumiwa na *STABEX.* Je, ni kwa nini maeneo yanayolima pamba yasishughulikiwe kama maeneo mengine yanayolima kahawa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, sehemu ambazo wanalima kahawa kuna utaratibu wa kutengeneza barabara kwa utaratibu wa *STABEX.* Lakini utaratibu huo haupo kwenye mazao kama Pamba, Ufuta, Mapunga na Mahindi.

Mheshimiwa Spika, huo ni utaratibu uliopangwa rasmi kwa mazao maalum. Kwa hiyo, hapo itakapotokea tukawa na uwezo wa kupata fedha hizo tutazitengeneza barabara zinazokwenda kwenye sehemu ambazo zinalima pamba pamoja na Morogoro Kusini.

Na. 333

**Hali ya Usalama Wilayani Geita**

**MHE. ERNEST G. MABINA (k.n.y. MHE. FAUSTINE K. RWILOMBA)** aliuliza:-

Kwa kuwa hali ya usalama Wilayani Geita inazidi kuwa mbaya kutokana na mwingiliano wa watu wengi na ujambazi uliokithiri; na kwa kuwa katika Bajeti ya mwaka 2002/2003 Serikali ilikiri

kwamba Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ni miongoni mwa Wizara zilizopewa kiasi cha fedha za kuridhisha:-

(a) Je, Wilaya ya Geita imepewa kiasi gani ili kukabiliana na hali hiyo, na ni magari mangapi mapya yanatarajiwa kununuliwa kwa ajili ya Polisi Geita?

(b) Je, ni Polisi wangapi walioongezwa ili kuimarisha usalama wa wananchi hususan katika maeneo ya Bukoli, Rwangasa, Katoro, Nyarugusu na Butundwe?

(c) Je, kwa nini Serikali isiweke sheria ya kuwashirikisha sungusungu na Polisi ili kukabiliana na hali ya ujambazi inayoelekea kuwashinda Polisi peke yao?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba, Mbunge wa Busanda, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2002/2003 Wizara yetu haikuwa imepata fedha kwa ajili ya kununulia magari. Kilichofanyika ni kulipia deni la magari yaliyonunuliwa kwa mkopo kwa mwaka 2001/2002 baada ya kuona kwamba ujambazi ulikuwa unaongezeka sana nchini na Polisi hawakuwa na magari. Jumla ya magari 165 ya aina ya *Landrover 110 pick up* yalihusika. Magari haya yaligawanywa katika Wilaya mbalimbali nchini na Wilaya ya Geita ilipata mgao wa gari moja, lenye namba za usajili *STJ 3728* na kufanya Wilaya hiyo kuwa na jumla ya magari mawili.

Hata hivyo, kulingana na ukubwa wa Wilaya ya Geita ni nia ya Serikali kuongeza gari lingine hapo uwezo wa fedha utakaporuhusu.

(b) Mheshimiwa Spika, katika kupambana na uhalifu, Serikali imeweza kueneza Askari Polisi kwa ajili ya kushirikiana na wanamgambo na sungusungu katika sehemu alizozitaja Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Kituo cha Polisi Bukoli wamepelekwa Askari watano, Kituo cha Polisi Rwamgasa Askari wanne, Kituo cha Polisi Katoro Askari sita, Kituo cha Polisi Nyarugusu Askari wanne na Kituo cha Polisi Butundwe Askari wanne.

Mheshimiwa Spika, ni wazi kuwa idadi hii ni ndogo lakini wanafanyakazi nzuri kwa kushirikiana na walinzi wa sungusungu katika maeneo hayo. Ni mpango wa Jeshi la Polisi kuongeza idadi hiyo mara tu Askari waliopo sasa mafunzoni katika Chuo cha Polisi Moshi watakapohitimu na kupangiwa vituo vya kazi.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali ilikwisha kutunga sheria ya Magambo na Sungusungu Na. 25 ya mwaka 1975 na kama ilivyorekebishwa na Sheria Na. 9/1989. Sheria hiyo imeweka bayana uwezo na jukumu la wanamgambo na sungusungu katika kupambana na uhalifu kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi. Kwa sasa sheria hii inakidhi mahitaji hayo, hivyo Serikali haina mpango wa kutunga sheria nyingine.

Aidha, kwa kutumia sheria hiyo, walinzi wa sungusungu katika maeneo mbalimbali Wilayani Geita wanafanyakazi nzuri na napenda kuchukua nafasi hii, kupitia Bunge hili Tukufu kuwashukuru na kuwapongeza wanamgambo na sungusungu hao kwani bila wao, taathira ya ujambazi katika Wilaya ya Geita ingekuwa kubwa zaidi.

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba Wilaya ya Geita ni kubwa na ameipa magari mawili tu. Je, Serikali inaweza ikaisaidia Wilaya ya Geita kuongeza kasma yake katika Fungu la mafuta na matengenezo ya magari ili angalau yasaidie katika mizunguko katika Wilaya ile?

(b) Kwa kuwa Vituo alivyovisema Mheshimiwa Waziri vya Butundwe, Rwamgasa na Katoro amepeleka Askari na hakupeleka silaha. Je, Wizara ina utaratibu gani wa kupelaka silaha katika maeneo yale ambayo yana ujambazi kubwa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu kuongezwa kasma ya mafuta na matengenezo ya magari kama ambavyo mlivyopitisha Bajeti yetu ya mwaka huu. Nashukuru mmetuongezea Bajeti ya Jeshi la Polisi kutoka shilingi 55,000,000,000/= za mwaka 2002/2003 mpaka shilingi 70,000,000,000/= kwa Bajeti ya mwaka huu.

Ongezeko hilo ambalo mmetupatia litaendana na vile vile kuongeza uwezo sasa wa Polisi kuongeza fedha za ununuzi wa mafuta na matengenezo ya magari. Halitakuwa kubwa sana, lakini tutegemee kwamba sasa Polisi watakuwa na mafuta zaidi ya mwaka huu kuliko ya mwaka 2002 na vile vile fedha za kutengeneza magari zitakuwa nyingi zaidi mwaka huu kuliko za mwaka jana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu silaha nia yetu kusema kweli kila mahali ambapo kuna Kituo cha Polisi tunapeleka Polisi pamoja na silaha. Sasa kama kuna vituo katika Wilaya ya Geita ambapo tumepeleka askari lakini silaha hazijapelekwa hiyo ni dosari ambayo tutairekebisha mara moja.

Na. 334

**Ujenzi wa Maghala Vijijini**

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali katika kipindi cha mwaka 1985-1990 iliwahamasisha wananchi kujenga maghala ya kuhifadhia mazao vijijini na wito huo ulipokelewa na wananchi:-

(a) Je, ni maghala mangapi yalijengwa na kati ya hayo ni mangapi yanayotumika?

(b) Kwa yale maghala ambayo hayatumiki, je, Serikali imeyawekea mikakati gani?

(c) Je, Serikali haioni kwamba mipango ambayo sio endelevu inawakatisha wananchi tamaa na ari ya kujitolea?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo na Chakula, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Kati ya mwaka wa 1985 na 1994 Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Kilimo na Chakula *(FAO),* Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Canada *(CIDA)* na Tume ya Uchumi ya Nchi za Ulaya *(European Economic Commission - EEC)* ilijenga maghala 382 katika Mikoa 18 ya Tanzania Bara. Maghala 30 yanamilikiwa na Vyama vya Ushirika na 352 yanamilikiwa na vijiji.

Aidha, katika kipindi hicho maghala madogo 1,474, yenye uwezo wa kuhifadhi tani moja hadi moja na nusu kila moja, yalijengwa kwa msaada wa *FAO* na *Sasakawa Global 2000* katika ngazi ya kaya kwenye mikoa 11 ya Tanzania Bara.

Lengo la kujenga maghala hayo lilikuwa ni kuongeza uwezo wa kuhifadhi mazao ya chakula na kuboresha maghala ya asili ya wakulima ili kupunguza upotevu wa mazao wakati wa hifadhi. Ujenzi wa maghala ulilenga zaidi mikoa inayozalisha mazao ya nafaka kwa wingi, hasa mahindi.

(b) Kwa kuwa maghala hayo yanamilikiwa na wakulima, vijiji vya Vyama vya Ushirika, wamiliki hao ndio wenye jukumu la kupanga matumizi ya maghala hayo. Jukumu la Serikali ni kuhimiza wananchi kujenga maghala zaidi na kutoa utaalamu kuhusu ujenzi wa maghala na mbinu bora za kuhifadhi mazao.

(c) Ujenzi wa maghala niliyoyataja ni endelevu kwa kuwa mpaka sasa yanatumika kuhifadhi mazao na pembejeo. Maghala hayo yalijengwa chini ya miradi maalum na kwa hiyo fedha zilizotumika zilikuwa ni kwa kipindi cha miradi hiyo.

Hata hivyo, baada ya miradi hiyo kuisha, Serikali imeendelea kuhamasisha wananchi kujenga maghala bora ili wahifadhi chakula cha kutosha kwa ajili ya matumizi ya familia zao na kwa ajili ya kutunza ziada au mazao ya biashara hadi bei itakapokuwa nzuri kwenye masoko.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Kwa kuwa Waziri amekiri kuna maghala yasiyotumika na naamini Wabunge wenzangu watakubaliana nayo anathibitisha kwamba huu mradi si endelevu. Je, Waziri sasa atasimamiaje kidete kuhakikisha haya maghala pia yanatumika? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, kwa taarifa tulizonazo Kiwizara, maghala yasiyotumika kabisa ni machache sana kama yapo. Kwa sababu Vyama vya Ushirika maeneo mengi sana yanatumia maghala hayo vijijini kwa kutunza mazao kabla hayajapelekwa kwenye soko kuu, mara nyingi sehemu za nje.

Aidha, kuanzia mwaka huu tutakuwa na mpango katika maeneo mengi tu kupeleka dhana mbalimbali hasa pembejeo. Maghala haya yatatumika vilivyo na ninaamini tatizo la kutokutumika sio kubwa kiasi hicho na kama lipo naomba tuonane tulijadili kwa undani zaidi.

**MHE. WILLIAM J. KUSILA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa ni dhahiri kabisa kwamba mpango wa ujenzi wa maghala haya haukutokana na mahitaji halisi ya uzalishaji, kwa sababu baadhi yake yaligeuzwa *immediately* kuwa Mahabusu na mengine yakawa vilabu vya pombe na bado yanatumika hivyo mpaka leo.

Je, Serikali itakubali kwamba mpango huu ni mfano mbaya wa mipango ambayo imeanzishwa bila utafiti wa kutosha na kwa hiyo kuelekeza raslimali mahali ambapo pengine hapatufaidishi zaidi kuliko tungelielekeza mahali pengine? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, mpango huu ulipoanza katika hiyo miaka niliyoitaja ilikuwa ndiyo tumeingiliwa na yule mdudu dumuzi. Kwa hiyo, ulijengwa mahsusi kutoa nafasi mazao yote yawekwe mahali pamoja iwe rahisi kumdhibiti huyu mdudu dumuzi. Utafiti ulifanyika na ilieleweka maeneo yale yanahitaji kutunza nafaka ya ziada kwa ajili ya kazi hiyo. Papo hapo tusisahau kuwa sasa hivi kuna wafanyabiashara wengi sana wanaotumia maghala haya kukusanya kidogo kidogo mazao na kuyatunza mahali kabla hawajatoa. Bado umuhimu wa maghala haya upo na tunaomba tushirikiane na wanavijiji kuwahimiza wayatumie vilivyo. *(Makofi)*

**MHE. BENITO W. MALANGALILA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa katika majibu ya Serikali yaliyotolewa hapa imeonekana kwamba Serikali haina maghala huko vijijini; na kwa kuwa katika Kijiji cha Ifwagi na Kilolo kule Iringa yako maghala hayo, je, Serikali inakubali kwamba kuanzia sasa maghala hayo ni mali ya wanavijiji?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, maghala yaliyopo Ifwagi na Kilolo bado yana kazi ya kufanya. Narudia tena kuwa mwaka huu huko Nyanda za Kusini, tutahitaji kupeleka pembejeo zitunzwe karibu kabla ya msimu wa ukulima. Kwa hiyo, naomba sana

Waheshimiwa Wabunge na kutoa wito kuwa tuyatumie maghala haya kusogeza pembejeo karibu kusudi kilimo kikishaanza tusihangaike. *(Makofi)*

Na. 335

**Migogoro ya Wachimbaji wa Kampuni ya Kigeni *Tanzanite* - Mererani**

**MHE. TALALA B. MBISE** aliuliza:-

Kwa kuwa kwa muda mrefu sasa kumekuwa na migogoro kati ya wachimbaji wadogo wadogo na Kampuni ya Kigeni kwenye machimbo ya *Tanzanite,* Mererani, Mkoani Manyara:-

(a) Je, ni nini sababu za migogoro hiyo na Serikali imechukua hatua gani dhidi ya tatizo hilo?

(b) Je, Serikali imeamua nini juu ya Nembo inayotumika na Kampuni ya Kigeni katika kutambua na kuuza madini ya *Tanzanite* nje ya nchi kana kwamba ndiye muuzaji pekee wa madini hayo?

(c) Kwa kuzingatia kasi ya uchimbaji wa sasa wa madini hayo; je, madini hayo yanaweza kudumu kwa muda wa miaka mingapi kuanzia sasa, na Tanzania itakuwa imefaidika kwa kiasi gani na kupata hasira/madhara gani?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Talala Mbise, Mbunge wa Arumeru Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)(i) Sababu za migogoro kati ya wachimbaji wadogo na Kampuni ya Kigeni kwenye machimbo ya *Tanzanite,* Mererani ni pamoja na zifuatazo:-

Baadhi ya wachimbaji wadogo huchimba chini kwa chini ardhini kuingia eneo la leseni la Kampuni ya Kigeni ambapo ni kinyume cha sheria ya madini, fujo zinazofanywa na vijana wazururaji, malalamiko dhidi ya *AFGEM* kuwa matumizi yake ya nembo yanaathiri biashara ya wachimbaji wadogo na malalamiko ya wachimbaji wadogo kuwa Kampuni ya *AFGEM* imemega kipande cha eneo la Kitalu (B).

(ii) Kufuatia ushauri wa Tume tatu zilizoundwa na Serikali kati ya 2000 na 2003 yaani ya *Major General* Mstaafu Mang'enya, *General* Mstaafu Mboma na Profesa Muhongo, Serikali imechukua hatua zifuatazo:-

Mererani imeshatangazwa kuwa *Controlled Area* kwa mujibu wa kifungu Na. 94 cha Sheria ya Madini ya 1998 na kanuni maalum zimeundwa na kutangazwa kwenye gazeti la Serikali kwa mujibu kwa kifungu Na. 110 cha Sheria ya Madini ya mwaka 1998. Hivi sasa Serikali ilikwishatoa fedha na zoezi la kuwaondoa watu wasio na kazi maalum linaendelea, wachimbaji na wafanyakazi wa Mererani sasa wana vitambulisho, kituo cha Polisi kimejengwa katika eneo la Machimbo kwa kuwashirikisha wadau yaani kwa kuwachangia fedha na vifaa na Ofisi ya madini imefunguliwa Mererani na *Tanzanite* inayosafirishwa nje sasa lazima ipate *Tanzanite Warranty* inayoambatana na *Export permits* yaani ruhusa maalum ya kusafirisha bidhaa nje katika kutekeleza makubaliano ya Kimataifa ya *TUSCON.*

Mheshimiwa Spika, utata wa mpaka kati ya kitalu B na C utashughulikiwa na upimaji utafanyika mara baada ya zoezi linaloendelea la kuwaondoa wazururaji kukamilika mwezi Septemba, 2003, Serikali imefikishwa umeme katika maeneo ya wachimbaji wadogo wa Kitalu B na D ili kuboresha miundombinu na Kamati ya Usuluhishi, kitalu B na D zimeimarishwa kwa kupewa Mhandisi mmoja mmoja kwa ajili ya kutoa ushauri wa kitaalamu.

(b) Mheshimiwa Spika, kuhusu Nembo ya *Tanzanite.* Serikali inalifahamu suala la Nembo ya *AFGEM* kama moja ya mambo yanayochochea migogoro kati ya *AFGEM* na wachimbaji wadogo. Kati ya

Tume tatu zilizoundwa na Serikali, kati ya mwaka 2000 na 2003, mbili zilishughulikia suala la Nembo ya *Tanzanite.* Tume ya kwanza ni Kamati ya Ushauri ya Madini inayoongozwa na *Major General* Mstaafu Mang'enya na ya pili ya *General* Mstaafu Robert Mboma.

Kamati ya ushauri ya madini ilishauri pawe na muafaka kati ya wachimbaji wadogo na *AFGEM* kuhusu matumizi ya Nembo. Ili kufikia muafaka huo, Kamati ilipendekeza kusitisha matumizi ya Nembo ya *AFGEM* na halafu uitishwe mkutano wa wadau wote kutafuta ufumbuzi wa suala hili.

Tume ya *General Mstaafu* Robert Mbona, ilisema kuwa *AFGEM* kutumia Nembo katika *Tanzanite* italeta ukiritimba katika biashara ya *Tanzanite* ambao utawafanya *AFGEM* kuhodhi soko na kudhibiti bei za *Tanzanite* na hivyo ilipendekeza pawepo na Nembo moja tu ya Kitaifa. Vinginevyo kusiwepo na nembo kabisa kwani *Tanzanite* ni ya kipekee *(Unique). (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa suala hili ni la Kibiashara na Bunge hili limetunga sheria ya ushindani halali wa Kibiashara *(Fair Competition Act. No. 8)* ya 2003, Serikali inafanya mashauriano kwa madhumuni ya kupata ufumbuzi wa suala hili kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizopo.

(c) Kwa kuzingatia kasi ya uchimbaji wa sasa, madini ya *Tanzanite* yatadumu muda wa miaka mingi ijayo, zaidi ya miaka 20. Mbali ya vitalu vinavyochimbwa sasa, Kitalu A ndio kwanza kinaanza kuchimbwa na kuna maeneo mengine nje ya Vitalu A na D ambayo hayajaanzwa kuchimbwa kabisa. Aidha, katika vitalu B na D uchimbaji unaofanyika hivi sasa, kwa wastani, unaenda hadi kina cha mita 100 tu chini ya ardhi wakati miamba yenye Tanzanite inaendelea chini zaidi ya kina cha mita 300 chini ya ardhi.

**MHE. TALALA B. MBISE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Namshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana. Pamoja na kumwomba pia atupatie Ripoti ya Tume naomba kuuliza swali moja dogo la nyongeza kwamba kwenye hiyo migogoro kuna wananchi ambao ni wachimbaji wadogo wadogo waliopoteza maisha yao. Aidha, kwa kufukuziwa mbwa au kupigwa risasi moja kwa moja na Kampuni husika au watu walioajiriwa naye je, ni wangapi hao waliopoteza maisha yao na Serikali ilichukua au inachukua hatua gani kuhakikisha kwamba wanafidiwa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Kwanza, napenda niseme kwamba katika Tume zilizoundwa na Serikali malalamiko ya unyanyasaji wa wananchi yalitolewa na Serikali ilichukua hatua ya kuionya Kampuni husika kwamba wasichukue hatua mikononi mwao.

Kuhusu wananchi ambao wameathirika katika njia moja au nyingine. Haya yamekuwa ni masuala ambayo Jeshi la Polisi limekuwa likiyashughulikia kikamilifu na kuwapeleka Mahakamani watu ambao wamekuwa wamehusika pale ambapo imebidi kuwapeleka Mahakamani.

**MHE. PARSEKO V. KONE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza suala la nyongeza.

Kwa kuwa Waziri amekiri kwamba kati ya mambo yanayosababisha mgogoro kati ya *AFGEM* na wachimbaji wadogo wadogo ni kumegwa eneo la Kitalu B la wachimbaji wadogo wadogo kuwekwa Kitalu C na kwa kuwa sikubaliani naye kwamba wachimbaji wadogo wadogo wanachimba chini kwa chini mpaka Kitalu C ila ni kwa sababu imemegwa eneo la Kitalu B. Je, Waziri anaweza kunipa tarehe ya kwenda kuamua mgogoro huo wa Kitalu na C na B. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa ushahidi wa kwamba pamekuwa na uchimbaji wa chini kwa chini si wetu sisi.Tunaona unatokana na Tume tatu zote zilizoundwa.

Pili, nimesema kwamba ni malalamiko ya wachimbaji dhidi ya *AFGEM* kama ambavyo *AFGEM* wana malalamiko yao dhidi ya wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la migogoro wa mpaka napenda niseme yafuatayo:-

Kwanza kabisa kama tunavyofahamu kila mgogoro una pande zinazohusika. Katika mgogoro huu wa mpaka kwa upande mmoja kuna wachimbaji wadogo na upande mwingine kuna Kampuni. Lakini kuhusu suala la *Tanzanite* pale Mererani na kama ilivyo katika migogoro mingi kuna wahusika wa mgogoro ambao wanaonekana na wengine ambao hawaonekani dhahiri.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa maana nyingine kuna wahusika wengi wa mgogoro huu na mgogoro wa mpaka wa Mererani kuhusu vitalu.

Kwa kweli ulichipukia kuanzia 1992 na wakati huo palikuwa na Kampuni mbili ya *GRAPHTAN* na *Building Utilities.* Moja hii ya *GRAPHTAN* ikiwa katika *area C* na *Building Utilities* ikiwa katika Kitalu B. Hawa wakati ule wa *GRAPHTAN* wenyewe pia walikuwa na mgogoro wa mpaka na *Building Utilities* ambao ndio walikuwa katika kitalu B wakisema kwamba wao *GRAPHTAN* ndio wamemegewa eneo lao.

Mheshimiwa Spika, ilipofika wakati huo wachimbaji wadogo walikuwa bado hawajapewa eneo hili la *Block B* na baadaye *Mererani Mining Company* yaani hawa *AFGEM* wa sasa ndio wakaja kuchukua eneo la *GRAPHTAN* yaani eneo la C wakalichukua na wakapewa leseni halali kulingana na *coordinates* zilizokuwepo.

Mheshimiwa Spika, sasa ninachotaka kusema ni kwamba *AFGEM* wamerithi lile eneo la *GRAPHTAN* na wakati huo na hawa *Building Utilities* walikuwa na mgogoro wao wa ardhi kwa maana ya eneo lakini ilipofika mwaka 1996 wachimbaji wadogo wakapewa eneo hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu tarehe wakati najibu swali la msingi nilisema kwamba mgogoro huu utatatuliwa kwa maana ya eneo kupimwa upya baada ya Septemba kwa sababu lazima wale wazururaji waondolewe katika operesheni maalum inayofanyika hivi sasa, operesheni ambayo muda wake ni miezi mitatu na ambayo iko chini ya uenyekiti wa Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro. *(Makofi)*

Na. 336

**Mradi wa Maji *Manolo Group***

**MHE. CHARLES H. KAGONJI** aliuliza:-

Kwa kuwa tatizo la maji safi na salama leo ni tatizo la nchi nzima na hata yale maeneo ambayo zamani yalikuwa yanaonekana kutokuwa na matatizo hayo siku hizi nayo yana matatizo ya maji:-

(a) Je, Serikali inalishughulikia vipi tatizo la Mradi wa Maji wa *Manolo Group* katika Jimbo la Mlalo?

(b) Je, kwa jinsi ambavyo matatizo ya maji katika vijiji vya Manolo, Madala, Mkunki, Nywelo na vinginevyo yalivyo makubwa, Serikali haiwezi kuwapatia wananchi wa maeneo hayo visima vifupi wakati jitihada za kutafuta ufumbuzi wa mradi wa *Manolo Group* zikiendelea?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Charles Kagonji, Mbunge wa Mlalo, kama ifuatavyo:-

(a) Serikali ilijenga mradi wa maji wa bomba wa Shume kutoka kijito cha Gologolo kuhudumia Vijiji vya Gologolo, Nywelo, Nkuki, Gemai na sehemu ya Kijiji cha Manolo mwaka wa 1968. Kutokana na uvunaji mkubwa wa misitu, chanzo hiki cha maji kimeathirika kwa ukame, hivyo kusababisha upungufu mkubwa wa maji kutoka chanzo hicho. Mradi pia umechakaa na kuharibika kutokana na kukosa matunzo na matengenezo.

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha huduma ya maji katika vijiji hivi, Serikali imebuni mradi wa *Manolo Group* ili kuongeza upatikanaji wa huduma ya maji katika Vijiji vya Gologolo, Nywelo, Gemai,

Manolo na Madala. Mradi huu tayari umefanyiwa upimaji na usanifu. Gharama ya mradi inakisiwa kuwa shilingi 767,400,000/= kwa gharama za mwaka 1999. Serikali inaendelea kutafuta fedha hizo kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo.

(b) Nakubaliana na ushauri wa Mheshimiwa Mbunge wa kuwachimbia visima wananchi wa maeneo hayo wakati juhudi zikiendelea za kutafuta fedha za ujenzi wa mradi wa *Manolo Group*.

Katika kipindi cha mwaka 2003/2004 Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto imetenga kiasi cha shilingi 3,000,000/= kwa ajili ya uchimbaji wa visima vifupi na uvunaji wa maji ya mvua katika vijiji hivyo. Serikali itaendelea na uchimbaji wa visima katika miaka inayofuata katika kipindi cha mwaka 2003/2004 Wizara itafanya utafiti wa maji chini ya ardhi katika maeneo hayo ili uchimbaji wa visima uwekwe kwenye Bajeti ya mwaka 2004/2005.

**MHE. CHARLES H. KAGONJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu yenye matumaini ya Naibu Waziri, ningependa kufahamu kwamba kwa sababu tatizo la maji katika Kata ile ya Shuma ni kubwa sana na kama alivyokiri mwenyewe kwamba mradi huo mdogo wa zamani umeharibika sana haufai hivi sasa.

Je, hizi shilingi 3,000,000/= zitatosha visima vingapi na pengine jitihada hizo zitaanza lini na kama Halmashauri yetu haiwezi kuikamilisha hiyo kazi, Wizara itakubali kusaidia kuchangia angalau kwa kipindi hiki ili wananchi wale wanaoteseka hasa akinamama waweze kupata maji kwa muda huu wakati tukitafuta fedha za mradi wa *Manolo Group?*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, fedha zilizotengwa shilingi 3,000,000/= nina hakika Mheshimiwa Mbunge na uongozi wa maeneo husika wakishirikiana na Halmashauri yao wanaweza kupata visima visivyopungua vitano vifupi. Kwa hiyo, jukumu ninaloomba Mheshimiwa Mbunge alifanye ni kuhamasisha wanakijiji ili mfano wa uchimbaji wa kisima unaweza ukifanywa na wana Kijiji ili fedha zilizotolewa na Halmashauri ziweze kutumika mahali ambapo wananchi hawawezi kuwa na uwezo navyo kama kununua ring au kununua lambo.

Kuhusu ni lini Serikali Kuu au Wizara yetu itasaidia kama nilivyosema mwaka huu wa fedha tutakwenda kufanya uchunguzi ili kuona upatikanaji wa maji uko katika kiwango kipi, maji ya kutoka ardhini. Hii ikiwa ni pamoja na kuthibitisha kwamba maeneo yatakayochimbwa yatakuwa na maji badala ya kwenda tunabuni tu.

Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mbunge tuvumiliane ili tuweze kufanya hiyo kazi kama nilivyosema kwenye jibu la msingi mwaka kesho tutaona kiasi gani Wizara iweze kusaidia.

Na. 337

**Maji Mjini Sumbawanga**

**MHE. PAUL P. KIMITI** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali iliahidi kumpata mhisani wa kushughulikia tatizo la maji kwa Mji wa Sumbawanga; na kwa kuwa tatizo la mhisani huyo ni kuwa hajaanza kazi:-

(a) Je, kwa nini Serikali isingeanza kusaidia jitihada za Mamlaka ya maji safi na maji taka katika uchimbaji wa visima virefu katika eneo la mji ili kupunguza upungufu huo wa maji mjini?

(b) Kwa kuwa Mji wa Sumbawanga una vijiji vipatavyo 28 ambavyo viko nje ya mji, vingine vikiwa na umbali wa zaidi ya kilometa 20 kutoka mjini; je, isingekuwa vizuri vikaendelea kuhudumiwa na Serikali Kuu chini ya Mhandisi wa Maji Mkoa na vitengewe Bajeti yake pekee?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Paul Kimiti, Mbunge wa Sumbawanga Mjini, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Mji wa Sumbawanga unakisiwa kuwa na wakazi wapatao 80,000 na unapata maji ya bomba kwa njia ya kutega kutoka katika mito midogo iliyopo katika msitu wa Mbizi, Mashariki ya mji. Pia mji huu unapata maji kutoka katika visima 18 vyenye kina cha kati ambavyo vinatumia pampu za mkono.

(b) Mheshimiwa Spika, ili kupunguza tatizo la maji Serikali Kuu ikishirikiana na Mamlaka ya Maji safi na maji taka Sumbawanga Mjini inaimarisha vyanzo vipya vya maji. Hii ikiwa ni pamoja na kutumia maji ya Mto Mwambazi. Jitihada hizo zitaongeza wingi wa maji Mjini Sumbawanga, kwa wastani wa mita za ujazo 1,4000 kwa siku wakati wa masika, na mita za ujazo 500 wakati wa kiangazi.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuisaidia Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Sumbawanga Mjini katika kuboresha huduma ya maji wakati tunasubiri Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB)* ambayo walikubali kufadhili utayarishaji wa mpango mpya wa Majisafi na Majitaka Sumbawanga mjini.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2001/2002, Serikali ilitoa shilingi 30,000,000/= na kipindi cha 2002/2003 shilingi milioni 40,600,000/= ili kusaidia jitihada za Mamlaka za kuikamilisha ujenzi wa mtambo wa kutibu maji, ujenzi wa chanzo kipya cha Mto Duwa, kukarabati mfumo wa maji uliopo, kupanua huduma ya usambazaji maji kwa maeneo mapya ya kununua dira za maji ili kudhibiti matumizi ya maji na kuboresha mapato.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuisaidia Mamlaka kuboresha upatikanaji wa maji Mjini Sumbawanga, ikiwemo kuchimba visima virefu.

(b) Kabla ya kuundwa kwa Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Sumbwanga Mjini mwaka 1998, miradi ya maji katika vijiji 28 vya Halmashauri ya Mji wa Sumbawanga, ilikuwa ikisimamiwa na Mhandisi wa Maji wa Mkoa.

Baada ya kuundwa kwa Mamlaka hiyo miradi ya maji katika vijiji hivyo inasimamiwa na Halmashauri ya Mji wa Sumbawanga kulingana na Sera ya Taifa ya Maji.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri hiyo imeunda Idara yake ya Maji baada ya kuwatakia kufanya hivyo wakati wa ziara yangu mwaka 2002 na imetenga shilingi 2,000,000/= kwa ajili ya kutoa huduma ya maji katika vijiji vya Halmashauri. Halmashauri hiyo itaendelea kuimarisha huduma hiyo kwa vijiji vyake.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia maelezo hayo na mfumo uliopo kwa sasa wa ushirikishwaji haitakuwa busara kwa vijiji hivyo kuhudumiwa na Serikali Kuu chini ya Mhandisi wa Mkoa.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza namwomba Mheshimiwa Waziri asiwe anakisia idadi ya watu wakati Sensa ya mwaka 2002 ilitwambia kwamba Mji wa Sumbawanga una zaidi ya watu 80,000. *(Makofi/Kicheko)*

(i) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Kata za Vijiji ambavyo amevitaja Mheshimiwa Naibu Waziri ambayo ni pamoja na Ntendo, Matanga, Fito, Milanzi, Senga, Molo pamoja na Kasense vina zaidi ya wakazi kuliko wale wanaoishi Mji wa Sumbawanga na kwa sababu uzito wa suala la maji ni muhimu katika Vijiji vinavyozunguka, je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kwamba ni vizuri sasa tukawa angalau tuna Mamlaka ndogo ambazo zinahusiana na Vijiji peke yake ambavyo vinazunguka Halmashauri ya Mji?

(ii) Kwa kuwa tatizo hili la Vijiji vinavyozunguka Halmashauri nyingi sana hasa Miji ya Mikoa havina msaada wowote, je, ni kwa nini utaratibu usiandaliwe ili angalau Vijiji hivyo vikawa na utaratibu

wa kuwa na ikama yake peke yake na ikiwezekana viwe na Wahandisi ambao ni wa kujitegemea wao wenyewe? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, Mji wa Sumbawanga ni mojawapo ya miji ambayo imeanzishwa siyo kipindi kirefu. Ili ku-*qualify* kuwa miji, miji hiyo ikiwemo Dodoma imechukua maeneo makubwa sana ya Vijiji kuwa katika eneo moja la Utawala wa Halmashauri ya mji au Manispaa.

Kwa hiyo, inawezekana kabisa idadi ya watu walio katikati ya mji wakawa katika kiwango ambacho siyo sahihi utakapoangalia takwimu za Sensa. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Paul Kimiti, labda tuzungumze kuhusiana na hili kwa sababu takwimu hizo na sisi tunazo.

Mheshimiwa Spika, lakini kama nilivyoeleza, maeneo ya Vijiji vinavyozunguka Mji wa Sumbawanga vilikuwa havina huduma hapo awali kwa sababu tulipoanzisha mamlaka maeneo hayo ambayo ni *peril-urban* yaliachwa na Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga ilikuwa haina Idara ya Maji ambayo sasa hivi wameiunda. *Focus* yetu kama Wizara itakuwa kuangalia na kusaidia Halmashauri ya Mji wa Sumbawanga ili ivihudumie Vijiji pamoja na Kata zote ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitaja.

Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira, hilo tumeliona na masahihisho yanaendelea ili tuweze kuwasaidia wanakijiji ambao wanazunguka Mji wa Sumbawanga.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha na Mheshimiwa Margareth Bwana hayupo, kwa hiyo, swali lake halitajibiwa. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, vikao vya leo ni kama ifauatavyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje, Mheshimiwa Dr. William Shija, anaomba Wajumbe wake wakutane saa 8.30 mchana chumba namba 56.

Tangazo la pili, *Chief Whip* wa Upinzani, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote wa Upinzani wakutane leo saa 7.00 baada ya kuahirisha Bunge. Hiyo inahusu vikao.

Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo moja la ziada. Mwanzoni mwa mkutano huu tulipata taarifa kwamba baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliibiwa fedha zao huko *VETA*.

Tulimwita *Managing Director* wa *CRDB* kumuuliza kama anaweza kutuwekea huduma za kibenki katika majengo yetu hapa ili kuondokana na hiyo adha ya Waheshimiwa Wabunge kubeba pesa mfukoni na alikubali. Jana alikuja na yale mambo yanayohitajika ya kuanzisha huduma za kibenki kwenye majengo yetu hapa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, mnaarifiwa kwamba *CRDB* sasa iko hapa kwa ajili ya huduma za kawaida za kibenki za kuweka na kuchukua pesa katika saa za kawaida.

Lakini zaidi ya hapo wamekuja na zile mashine za *Tembo Card* ambapo unaweza ukachukua pesa wakati wowote, siku yoyote, saa 24. Wataalam wako kwenye eneo letu wanaweza kuwapa maelezo zaidi, lakini taarifa ni kwamba huduma hizo zimeanza sasa rasmi katika majengo yetu ya Bunge maalum kwa ajili ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mwisho wa matangazo, tuendelee na *Order Paper* kama ilivyorekebishwa, Katibu.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2003/2004
### Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likae kama Kamati ya Matumizi ili liweze kupokea na kujadili shabaha na malengo ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na hatimaye kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze hotuba yangu kwa kutoa pongezi za dhati kabisa kwa Wabunge wenzetu wapya waliochaguliwa katika uchaguzi mdogo wa Bunge la Jmahuri ya Muungano uliofanyika mwezi Mei, 2003. Nawapongeza na kujumuika nao katika kusherehekea ushindi wao. Nawapa pole kwa majukumu waliyokumbana nayo katika harakati za uchaguzi. Kuchaguliwa kwao kumetusaidia kuzima midomo ya malipyoto wa ndani na wa Kimataifa ambao wanaishi kwa kueneza umbea dhidi ya nchi yetu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naomba kwa namna ya pekee nimshukuru Waziri Mkuu, Mheshimiwa Frederick Sumaye, kwa kutaja bayana katika hotuba yake maeneo muhimu ya Ushirikiano wa Kimataifa ambayo Serikali itayapa umuhimu wa juu. Nawashukuru pia Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil Mramba na Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, kwa hotuba zao nzuri zilizoainisha maeneo mbalimbali ya Uhusiano na Ushirikiano wa Kimataifa ambayo Serikali yetu inayapa umuhimu wa juu.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii pia kuwashukuru Wabunge wenzangu ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Dr. William Shija, ambao walijadili Makadirio ya Wizara yangu kabla ya kuyafikisha hapa leo. Kamati hiyo ilifanya uchambuzi mzuri, tena wa kina na kutoa ushauri ambao utaisaidia Wizara yangu katika kuboresha utekelezaji wa malengo ya Bajeti hii. Mimi na wenzangu Wizarani tumefaidika sana na michango yao na ushauri wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niruhusu pia niwashukuru Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Abdulkader Shareef, Katibu Mkuu Ndugu Philemon Luhanjo, Wakurugenzi, Mabalozi wetu walioko nchi za nje pamoja na wafanyakazi wenzangu wote Wizarani na katika Balozi zetu kwa juhudi wanazozifanya kutetea na kuendeleza maslahi ya Taifa letu nje. Nawapongeza kwa moyo wao wa uzalendo na uchapakazi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka wa fedha wa 2002/2003 ulikuwa mzuri kwa upande wa upatikanaji wa fedha. Ukusanyaji wa maduhuli katika Balozi zetu ulivuka lengo lililokadiriwa kwa 150%. Makadirio ya Bajeti yalikuwa kiasi cha shilingi 3,573,112,600/= na makusanyo halisi hadi tarehe 30 Juni, 2003 yalikuwa shilingi 5,373,607,401/=. Mafanikio haya yametokana na juhudi za Balozi zetu katika kuitangaza nchi yetu kiuchumi, kibiashara na hasa katika nyanja za utalii. *(Makofi)*

Sisi tunaamini kuwa kama pasingekuwepo ushauri wa Serikali za Marekani, Uingereza, Italia, Hispania na Australia kwa raia wa nchi za nje dhidi ya kutembelea Afrika Mashariki hususan Zanzibar na Kenya mambo yangekuwa mazuri zaidi. Ushauri huo uliotolewa kwa madai ya kuwepo kwa tishio la ugaidi katika nchi zetu, ulipunguza watalii na wageni waliopanga kuja kutembelea nchi yetu. Balozi zetu zinastahili pongezi maalum kwa kazi kubwa waliyoifanya kuelezea Jumuiya ya Kimataifa kuwa Tanzania ni nchi salama. Tutaendelea kufanya hivyo kwa nguvu zaidi mwaka huu wa miaka ijayo. Kadhalika tutaendelea kuchukua hatua za kuwahakikishia raia wa nchi yetu na wageni wetu usalama wao.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mapato kutoka Hazina, Wizara yangu imepokea kiasi cha shilingi 30,074,654,462/=. Ukijumlisha na shilingi 5,373,607,401/= zinazotokana na maduhuli Balozini, Wizara yangu ilikuwa imepata jumla ya shilingi 35,448,261.263/=. Kiasi hiki kinajumuisha shilingi 28,266,845,500/= zilizoidhinishwa wakati wa kikao cha kawaida cha Bajeti cha mwaka 2002/2003 na shilingi 7,181,416,636/= zilizotolewa kama Bajeti ya nyongeza. Aidha, Wizara ilikuwa imetumia kiasi cha shilingi 34,862,942,462/= hadi tarehe 30 Juni, 2003.

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa mafanikio makubwa ya Wizara yangu katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2002/2003 ni pamoja na kufungua tena Ubalozi wetu Bujumbura na kuhamisha Ubalozi wa Lagos kwenda Abuja na wa Bonn kwenda Berlin.

Aidha, tumeweza kumalizia ujenzi wa jengo la ofisi ya Ubalozi wetu Addis Ababa na kununua jengo la ofisi huko Roma, Italia. Kadhalika tumenunua nyumba moja ya kuishi huko Pretoria, Afrika Kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeweza pia kuendeleza ujenzi wa Chuo cha Diplomasia na hivi sasa kazi hiyo inaelekea kukamilika. Kwa kukubaliana na Hazina tuliahirisha kufungua Ubalozi Uholanzi na kuzitumia fedha zilizotengwa kwa ajili hiyo kuendeleza ujenzi hapo chuoni. Tulilazimika kufanya hivyo kwa sababu ujenzi ulikuwa unaendelea na bahati mbaya Hazina hawakuweza kututengea fedha kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Spika, tumenunua magari ya Balozi zetu za Lusaka, Kigali, Abu Dhabi, Bonn, New Delhi, Bujumbura na Washington. Mwaka huu tunatarajia kuendelea kununua magari kwa ajili ya Balozi zetu nyingine kulingana na Bajeti na upatikanaji wa fedha. Aidha, tulinunua magari saba kwa ajili ya Idara za Makao Makuu na kusaidia sana kuboresha huduma ya usafiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa jumla hali ya dunia ilivyo sasa kwa upande wa usalama na maendeleo ya kiuchumi na kijamii haina mabadiliko makubwa na ilivyokuwa mwaka jana nilipokuwa natoa taarifa kama hii Bungeni. Amani na utulivu vimeendelea kuwa bidhaa adimu duniani. Taarifa za vita, mapigano na migogoro ya kisiasa na kijamii zimeendelea kusikika duniani kote, lakini nyingi zaidi zikiwa zinatokea Afrika na Mashariki ya Kati. Magonjwa ya Ukimwi, Malaria na Kifua Kikuu yameendelea kuta tishio. Yamekuwa yanatesa na kuua mamilioni ya watu hasa katika nchi zinazoendelea.

Mheshimiwa Spika, katika Bara la Afrika kumekuwepo na migogoro katika nchi za Liberia, Sierra Leone, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Angola, Burundi, Sudan, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Comoro, Eritrea, Ethiopia, Somalia, Madagascar, Algeria, Mauritania na hivi karibuni Sao Tome na Principe. Bahati nzuri kwa migogoro yote hiyo, Waafrika wenyewe kupitia Umoja wa Afrika, Umoja wa Kiuchumi wa Kanda na ushirikiano wa nchi jirani na marafiki wamekuwa wanajihusisha kwa ukamilifu katika jitihada za kutafuta ufumbuzi. Mafanikio ya kutia moyo yamekuwa yanapatikana pamoja na ugumu uliokuwepo wa kupata suluhisho endelevu. Tunafurahi pia kwamba Umoja wa Mataifa, kupitia kwa Katibu Mkuu, Kofi Annan na Baraza la Usalama, umekuwa unashirikiana kwa karibu sana na Umoja wa Afrika na ushirikiano wa kikanda na hata nchi moja moja katika kutafuta suluhisho kwa matatizo ya Afrika.

Mheshimiwa Spika, migogoro ya Angola, Comoros, Sierra Leone, Madagascar, Mauritania na Sao Tome na Principe inaelekea kuwa sasa imekwisha. Kwa ajili hiyo, Madagascar imeweza kuruhusiwa kukalia tena kiti chake katika Umoja wa Afrika baada ya kusimamishwa uanachama kwa muda kufuatia migogoro ya uchaguzi nchini humo. Uasi wa kijeshi nchini Sao Tome na Principe umemalizika na Rais Fradige de Menezes wa nchi hiyo amerejea madarakani. Hali ya kivita iliyokuwepo kati ya Eritrea na Ethiopia sasa haipo tena. Kinachosubiriwa sasa ni kuanza kwa zoezi la kurekebisha mpaka baina ya nchi hizo Oktoba, 2003.

Mheshimiwa Spika, katika visiwa vya Ngazija *(the Comoros)* mgogoro wa kimsingi uliohusisha kujitenga kwa Kisiwa cha Anzuani sasa umemalizika. Comoros ni Taifa moja tena. Kazi kubwa iliyopo sasa ni kuimarisha muundo wa Serikali ya Shirikisho. Maendeleo ya mazungumzo ya kutatua mgogoro wa zaidi ya miaka 40 wa Sudan yanatia matumaini. Katika mazungumzo hayo, yanayoongozwa na Kenya, pande zinazohasimiana zimeshaelewana kimsingi kuacha mapigano na kuunda Serikali ya Shirikisho kati ya Sudan ya Kaskazini na Kusini. Wamekubaliana kuwa baada ya miaka sita Wananchi wa Kusini watakuwa huru kuamua kama wanataka kujitenga au kubakia sehemu ya Sudan.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Somalia mazungumzo yanaendelea vizuri Mjini Nairobi, Kenya. Kuna matumaini kuwa baada ya muda si mrefu makubaliano yatafikiwa juu ya kuunda Serikali ya Mpito ya Umoja wa Kitaifa. Katika Jamhuri ya Afrika ya Kati, utawala mpya wa kijeshi unaoongozwa na *General* Francois Bozize umetakiwa na Umoja wa Afrika kurejesha nchi hiyo kwenye utawala wa kidemokrasia haraka iwezekanavyo. Kwa sasa uanachama wa nchi hiyo katika Umoja wa Afrika umesitishwa mpaka masharti hayo yatakapotekelezwa.

Mheshimiwa Spika, hali ya nchini Liberia bado ni kitendawili. Baada ya makubalino ya kuacha mapigano yaliyofikiwa Accra, Ghana chini na uongozi wa *General* Abdulsalim Abubakar tulipata matumaini kuwa vita baina ya waasi na Serikali vitaisha. Kufuatia ziara ya hivi karibuni ya Rais Olusegun Obasanjo wa Nigeria nchini Liberia na Rais Charles Taylor kukubali kwenda kuishi uhamishoni nchini Nigeria tulidhani kuwa mgogoro huo umepatiwa ufumbuzi wa kudumu. Inaelekea mambo bado ni magumu na mapigano yanaendelea kwa kasi sana. Tanzania inaamini kuwa mpango wa *ECOWAS* wa kumaliza mgogoro huo bado ni sahihi. Tunatoa wito kwa umoja huo kuharakisha utekelezaji wake na kwa Marekani kufanya uamuzi thabiti kuhusu mchango wake katika mpango huo. Pia tunaziomba pande zinazohusika kuacha mapigano na kutoa nafasi kwa mpango wa amani wa nchi yao ukatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo tunaanza kuiona nuru mpya ya matumaini ikichomoza. Baada ya kusuasua kwa miezi kadhaa tumefurahi kuwa hatimaye Serikali ya Mpito yenye Rais na Makamu wa Rais wanne na Mawaziri wapatao 60 imeanza. Tanzania inawapongeza Wakongomani kwa hatua waliyofikia na kuwatakia kila la heri na kuihakikishia Serikali ya Kongo na Wananchi wa Kongo kuwa tutakuwa pamoja nao kwa hali na mali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali mbaya ya usalama na utulivu huko Mashariki ya Kongo hususan katika Jimbo la Kivu na Wilaya ya Ituri inatusikitisha sana. Tunafurahishwa na hali ya utulivu Mjini Bunia baada ya Majeshi ya Kulinda Amani yanayoongozwa an Wafaransa kuingia.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena, tunatoa wito kwa Wanamgambo wa Kihema na Kilendu kuacha mapigano na kuheshimu mikataba waliyotiliana saini mara mbili Mjini Dar es Salaam. Kadhalika tunapenda kurudia kauli aliyotoa Rais wetu Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, wakati alipotembelewa na Ujumbe wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa tarehe 14 Juni, 2003 ya kutaka kuongezwa ukubwa wa Jeshi la *MONUC* na madaraka yake. Jeshi la sasa la *MONUC* nchini Kongo ni dogo na madaraka yake ya kulinda amani tu ni hafifu. Inatakiwa Jeshi hilo liongezwe na madaraka yake yawe ni ya kuleta amani badala ya kulinda amani tu. *(Increase the size of force and upgrade its mandate to that of peace-enforcement rather than peacekeeping).*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Burundi nako dalili za matumaini zinajitokeza pamoja na magumu yote yaliyopo na kuashiria kuwa safari bado ndefu. Juhudi kubwa iliyofanywa na nchi jirani na marafiki wa Burundi ya kutafuta kupatikana makubaliano ya kuacha mapigano kati ya waasi na Serikali hatimaye zilifanikiwa. Mwezi Oktoba, 2002 makubaliano yalifikiwa kati ya Serikali na vikundi vidogo vidogo vilivyojitenga na makundi makubwa ya waasi yaani vya Bwana Jean Bosco Ndaikengurukie wa *CNDD-FDD* na Bwana Alain Mugabarabona wa *FNL*. Tarehe 2 Desemba, 2002 Serikali ilitiliana saini Mkataba wa kuacha uhasama na mapigano na kundi kubwa la *CNDD-FDD* linaloongozwa na Bwana Pierre Nkurunziza.

Mheshimiwa Spika, kutiwa saini kwa mikataba hiyo kulileta matumaini kuwa mambo sasa yatakuwa mazuri. Lakini mambo hayajawa shwari! Kutokuaminiana kuliendelea na mapigano ya hapa na pale yaliendelea kutokea. Mapigano makali zaidi ni yale ya hivi karibuni yaliyotokea Mjini Bujumbura yaliyofanywa na *FNL* ya Agathon Rwasa ambapo watu kadhaa wamepoteza maisha.

Mheshimiwa Spika, katika mkutano wao wa dharura Mjini Dar es Salaam tarehe 20 Julai, 2023. Viongozi wa Uganda, Tanzania na Afrika Kusini walitoa wito kwa waasi wa *FNL* kuacha mapigano na kuanza mazungumzo na Serikali ya Burundi. Mkutano huo pia umesaidia sana kupunguza tofauti na kutokuelewana kati ya *CNDD-FDD* ya Peter Nkurunziza na Serikali ya Burundi.

Hivi sasa mazungumzo yanaendelea baina ya pande hizo mbili kuhusu kugawana madaraka katika Jeshi la kushirikisha *CNDD-FDD* katika utawala wa mpito. Mazungumzo yanayoendelea sasa Mjini Dar es Salaam kati ya Serikali ya Burundi na kikundi kikubwa cha *CNDD-FDD* ya Peter Nkurunziza, huenda yakasaidia kuliwezesha hilo kuwa. Tunatoa wito kwa kikundi cha *FNL* cha Agathon Rwasa kuacha mapigano na kujiunga na mazungumzo, tunasubiri majibu yao kwa hamu.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ingependa kuona moyo mpya, ari mpya na kasi kubwa zaidi ya kutekeleza Mkataba wa Arusha na kuacha mapigano. Tanzania inaamini kuwa kama pande hizo zitakuwa

makini na Viongozi wake kuwa waaminifu na wakweli kwa dhamira ya kupata suluhisho la amani, safari hii nafasi ya Burundi kupata amani ipo.

Mheshimiwa Spika, nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Tanzania imeombwa na imekubali kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Maziwa Makuu mwezi Juni, 2004. Huu ni mkutano wa kwanza wa aina yake kufanyika duniani. Unatayarishwa na Umoja wa Mataifa na utazihuisha nchi sita za Maziwa Makuu yaani Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo pamoja na majirani zao, washirika wao na marafiki zao. Miongoni mwa marafiki zao ni pamoja na nchi za Umoja wa Ulaya na nchi Wanachama wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa. Tunadhani karibu nchi 40 zitashiriki.

Mheshimiwa Spika, mkutano huo ni wa Wakuu wa Nchi na Serikali na utatanguliwa na mkutano wa matayarisho wa Mawaziri utakaofanyika Kigali Rwanda. Ni heshima kubwa kwa nchi yetu, Rais wetu na Wananchi wote kwa jumla hivyo hatuna budi kuhakikisha kwamba ufanisi wa hali ya juu unakuwepo. Tanzania haitachoka kutoa mchango wake katika kutafuta ufumbuzi wa migogoro ya Maziwa Makuu kwani ni kwa manufaa yetu pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la Mashariki ya Kati limeendelea kuwa eneo la migogoro ya kivita na mapigano hususan Israel, Palestina na Iraq. Mpango wa Kuleta Amani *(Road Map)* kati ya Wapalestina na Wayahudi umetangazwa. Mpango huo uliotayarishwa na Mataifa makubwa manne duniani yaani Marekani, Urusi, Uingereza na Ufaransa unataka hatimaye kuundwa kwa Taifa la Wapalestina ifikapo mwaka 2005. Bahati nzuri pande zote mbili zimeukubali mpango huo ingawaje Israel imeelezea mashaka yake kwa baadhi ya vipengele.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mpango umeanza na una mwelekeo mzuri ingawaje bado kuna matatizo kadhaa. Jambo moja kubwa linalotia faraja ni kule kukubali kwa vikundi vya Wanamgambo wa Kipalestina, kusitisha mashambulizi dhidi ya Wayahudi. Uamuzi huo utasaidia sana kuimarisha amani ya eneo hilo matumaini yetu kuwa upande wa Israel nao utasitisha mashambulizi ya kuwahi *(pre-emptive strikes)* ambayo mara kwa mara kila yanapofanywa huchochea mashambulizi ya kulipiza kisasi kutoka upande wa Wapalestina.

Mheshimiwa Spika, Tanzania inawapongeza Wayahudi na Wapalestina kukubali mpango huo na kuanza kutekeleza. Tunawasihi washikilie uzi huo. Tuko pamoja nao. Tanzania inaunga mkono mpango huo kwani wakati wote nchi yetu imekuwa inaamini kuwa jawabu la kudumu la mgogoro huo upo katika kuundwa kwa Taifa la Palestina litakaloishi pamoja na Israel kwa amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwezi Machi, 2003 dunia imeshuhudia vita ya pili nchini Iraq vilivyoongozwa na Marekani na Uingereza dhidi ya Kiongozi wa Iraq Bwana Saddam Hussein. Tofauti na vita vya kwanza vilivyopata ridhaa ya Umoja wa Mataifa, safari hii Umoja wa Mataifa haukufanya hivyo kwa sababu ulitaka wachunguzi wake waliokuwa Iraq kutafuta silaha za maangamizi zilizodaiwa kuwepo waongezewe muda wa kukamilisha kazi yao.

Mheshimiwa Spika, Marekani na Uingereza walipinga rai ya kuwaongeza muda wachunguzi wa silaha nchini Iraq kwa madai kufanya hivyo ni kupoteza wakati na kwamba kutamfanya Saddam Hussein aendelee kuihadaa dunia. Walipendekeza kutumia nguvu kuwa ndiyo njia pekee iliyo bora. Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa halikuafikiana nao hata hivyo waliamua kuendelea na vita ambavyo matokeo yake sote tunayajua. Uamuzi huo wa Marekani na Uingereza umezua mjadala mkali sana duniani hasa kuhusu maana na umuhimu wa Umoja wa Mataifa.

Mheshimiwa Spika, Tanzania haina shaka na umuhimu wa Umoja wa Mataifa, pamoja na yote yaliyotokea. Hatumsikitii Saddam Hussein, wala hatuichukii Marekani wala Uingereza, ila kimsingi Tanzania inaamini kuwa siyo sawa na tena ni hatari kwa amani ya dunia kwa Mataifa kupuuza mamlaka na ridhaa ya Umoja wa Mataifa. Sote, wadogo kwa wakubwa, hatuna budi kuheshimu Mamlaka ya Umoja wa Mataifa kwa mujibu wa mkataba wake ambao kila mwanachama ameukubali na kutia sahihi. Kufanya hivyo kutaashiria dunia amani iliyotazamiwa wakati wa kutengeneza mkataba ulioanzisha Umoja wa Mataifa mwaka 1945. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kasoro zote zilizotokea lakini Dikteta Saddam Hussein, keshaondoshwa na hatarudi tena! Suala muhimu sasa ni kushughulikia hatma ya baadaye ya Iraq na watu wake. Tanzania inaamini kuwa bado Umoja wa Mataifa una wajibu mkubwa. Unastahili kupewa majukumu na nafasi kubwa zaidi katika maamuzi ya kuweka utawala wa muda, ujenzi wa Asasi mpya za utawala na mpango mzima wa kuirejesha Iraq katika utawala wa kidemokrasia. Ni maombi na matumaini yetu kuwa mapema iwezekanavyo, Iraq itarejea katika hali ya kawaida, ya amani na utulivu na utawala wa kidemokrasia.

Mheshimiwa Spika, ugaidi umeendelea kuwa tishio duniani. Taarifa za matukio ya ugaidi au hofu ya kuwepo tishio la ugaidi mahali fulani zimekuwa zinasikika mara kwa mara. Katika mwaka mmoja uliopita dunia imeshuhudia matukio makubwa ya kigaidi huko Indonesia, Saudi Arabia, Kenya, Israel na Chechnya ambapo mamia ya watu walipoteza maisha na wengine wengi kujeruhiwa na mali kuharibiwa.

Mheshimiwa Spika, kuendelea kuwepo matukio ya kigaidi kunaimarisha haja ya dunia kuendeleza mshikamano wake dhidi ya uovu huu. Wakati huo huo dunia haina budi kuendelea kuyashughulikia kwa dhati matatizo au mazingira yote yanayokuwa mboji ya kumea mbegu za ugaidi.

Mheshimiwa Spika, Tanzania inaamini kuwa tukifanikiwa kufanya hivyo, dunia itajihakikishia usalama wa kweli.

Mheshimiwa Spika, napenda kuitumia nafasi hii kuihakikishia Jumuiya ya Kimataifa kuwa, Tanzania itaendelea kushirikiana na yo katika kupambana na ugaidi. Tumefanya hivyo tangu Agosti 7, 1998 wakati wa shambulio la kigaidi dhidi ya Ubalozi wa Marekani Mjini Dar es Salaam, tumeendelea kushirikiana baada ya Septemba 11, 2001 na tutaendelea kushirikiana hivyo hivyo siku za usoni.

Katika miezi ya hivi karibuni nchi yetu imekuwa inafadhaishwa sana na taarifa kuwepo tishio la ugaidi nchini mwetu zilizokuwa zinatolewa na baadhi ya washirika wetu Wakuu katika vita hivi. Kinachotusikitisha sisi ni jinsi taarifa hizo zinavyotolewa na hasa kule kukosekana kwa ushirikiano katika utoaji wa taarifa zenyewe. Mara kwa mara hata siye wenzao huzisoma tu kwenye vyombo vya habari bila ya ilani yoyote kutolewa kwetu mapema. Ni vyema marafiki zetu wakajua kuwa kauli zao zinatuumiza sana hasa kwa upande wa utalii.

Mheshimiwa Spika, hali ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii duniani ni suala kubwa na *agenda* muhimu katika mikutano na kijumuiko mbalimbali ya Kimataifa. Umaskini uliopo duniani miongoni mwa watu na Mataifa ni suala linalozua mjadala mkali kwa sababu ni hali isiyokubalika hata kidogo. Idadi ya watu maskini na Mataifa maskini duniani inazidi kuongezeka badala ya kupungua.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa inakadiriwa kuwa kuna watu wapatao bilioni moja ambao wanaishi katika hali ya umaskini uliokithiri *(abject poverty)* yaani wanaishi kwa pato la chini ya Dola moja kwa siku. Bahati mbaya sana watu wengi walio maskini na nchi nyingi zilizo maskini sana zipo katika nchi zinazoendelea.

Mheshimiwa Spika, jambo linalozua mjadala ni ule ukweli kwamba hivi leo duniani kuna utajiri mkubwa sana mikononi mwa watu na miongoni mwa baadhi ya Mataifa hasa ya kundi la Kaskazini. Vile vile, kuna maendeleo makubwa sana ya sayansi na teknolojia, hivyo basi binadamu amejenga uwezo mkubwa wa kutawala na kutumia mazingira ya kujiletea maendeleo. Kwa hiyo, umaskini kuendelea kuwepo na hata kuongezeka duniani ni jambo lisiloeleweka wala kuelezeka. Ni hali isiyokubalika hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, zipo sababu kuu mbili zinazoelezea kwa nini hali iko hivyo ilivyo na inaendelea kuwa hivyo. Kwanza kabisa ni mfumo wa uchumi na biashara duniani unaozipendelea nchi zilizoendelea na kuzikandamiza nchi maskini. Pili, ni utashi wa kisiasa wa kusaidia maskini wajikwamue kutokuwa wa kiwango muafaka miongoni mwa Mataifa yaliyoendelea.

Mheshimiwa Spika, ninaposema hivyo sina maana ya kutotambua au kutothamini misaada na michango inayotolewa na nchi zilizoendelea kwa nchi zinazoendelea. Najua wanachangia sana na tunawashukuru sana kwa hilo. Hata hivyo, nataka kusema au kusisitiza kuwa wangeweza kufanya zaidi ya wafanyavyo sasa.

Mheshimiwa Spika, sisi tunaamini kwamba Mataifa tajiri yangeweza kufuta madeni yote wanayozidai nchi maskini bila ya uchumi wa nchi zao kutetereka. Aidha, nchi zilizoendelea zingeweza kuongeza misaada ya maendeleo kwa nchi maskini bila ya bajeti za nchi zao kuvurugika.

Mheshimiwa Spika, nchi maskini zikifutiwa madeni na misaada ya maendeleo kuongezwa kasi ya maendeleo itaongezeka na tofauti yake itaonekana. Tanzania ni mfano dhahiri wa ukweli huu. Kufuatia nafuu kiasi ya kufutiwa madeni tuliyopata chini ya mpango wa *HIPC* na nyongeza kidogo ya misaada ya maendeleo nchi yetu imeweza kuongeza bajeti za Sekta za elimu, maji, afya, barabara na kadhalika. Matokeo yake yamekuwa mazuri kwa kuboreshwa kwa elimu ya msingi na huduma za maji, afya na barabara Vijijini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo uchumi mkuu *(macro-economy)* umeimarika zaidi sasa kuliko wakati mwingine wowote katika historia ya nchi yetu. Laiti kama msamaha wa madeni ungekuwa mkubwa zaidi na misaada ya maendeleo kuongezwa maradufu mambo yangekuwa mazuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua ukweli huo ndiyo maana Rais wetu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa na Serikali yake hatuachi kujisemea na kuzisemea nchi zetu kupatiwa nafuu kubwa zaidi ya madeni na kuongezewa misaada ya maendeleo yenye masharti nafuu. Naomba kuitumia fursa hii kutoa pongezi maalum kwa Rais wetu kwa kazi nzuri na hasa kwa uongozi thabiti anaoutoa kwa Tanzania na duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, sasa amekuwa Kiongozi wa kutumainiwa duniani wa kuwasemea wanyonge na maskini na wapenda maendeleo wote. Kauli zake za kijasiri katika majukwaa ya Kimataifa zinahesabiwa kuwa ni kauli thabiti zinazowakilisha watu wengi hasa wa dunia ya tatu. Tanzania, siku hizi ni nchi inayosifiwa sana na kupigiwa mfano wa mafanikio iliyopata katika nyanja mbalimbali. Inasifiwa kwa sera nzuri na utekelezaji mzuri wa sera zake kwa mambo kama vile sera za uchumi, sera za Bajeti, sera za fedha na sera za uwekezaji. Pia tunasifiwa kwa utekelezaji wa masuala muhimu kwa mujibu ya Kitaifa na Kimataifa. kwa mfano, kwa mujibu wa masharti ya *HIPC*, tunasifiwa kwa sera za kupambana na Ukimwi na sera za maendeleo ya jamii kwa jumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tanzania sasa imejitokeza kuwa nyota inayong'ara ktika Bara la Afrika ambalo mtazamo potofu wa dunia huliona kuwa ni Bara la matatizo mengi na kukatisha tamaa. Wapo ambao wamediriki hata kuliita Bara la Giza. Wahenga wamesema mcheza kwao hutunzwa. Hatuna budi kumpongeza na kumshukuru nahodha wetu, Baba yetu, Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, kwa kazi nzuri aliyoifanyia nchi yetu na anayoendelea kuifanyia. Wajibu wetu sisi sote Serikalini, Bungeni na nchini ni kuendelea kumuunga mkono na kumsaidia ili nuru inayoangaza sasa izidi kuang'ara na kamwe isififie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaendelea kuyaomba Mataifa tajiri kufuta madeni kwa nchi maskini na kuongeza misaada ya maendeleo kwa nchi zetu. Ahadi nyingi zimetolewa na Mataifa hayo kuonyesha utayari wao kusaidia nchi maskini na chi zinazoendelea. Walifanya hivyo miaka ya nyuma na hata miaka ya hivi karibuni katika mikutano na mijumuiko mbalimbali ya Kimataifa. Sasa ni wakati muafaka kabisa kwa Mataifa tajiri kuonyesha ithibati ya kauli zao kwa kuheshimu na kutekeleza ahadi zao hizo.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa bado wengi hawajatekeleza ipasavyo ahadi zao na kwa sababu hiyo lengo la kupata Dola za Kimarekani bilioni 50 kila mwaka za kutekeleza malengo manane ya Milenia halijafanikiwa.

Kwa upande wa ahadi nyingine muhimu za huko nyuma, moja ni ile ya nchi tajiri kutoa asilimia 0.7 ya Pato la Taifa kwa ajili ya misaada ya maendeleo. Mpaka sasa ni nchi za Norway, Sweden, Denmark,

*The Netherlands* na Luxembourg tu ndizo zimeshatimiza ahadi hiyo. Wakati tunazipongeza nchi hizo tunazisihi nchi zilizosalia nazo kuongeza kasi ya kutekeleza ahadi hiyo.

Mheshimiwa Spika, nchi zinazoendelea hazina budi kuendelea kupigania mageuzi katika mfumo wa uchumi wa biashara duniani ili uwe wa haki, unaotujumuisha sote na kutunufaisha sote. Hatuna budi kuendelea kudai katika Shirikal la Biashara la Dunia *(WTO)* na majukwaa mengine ya Kimataifa kanuni za biashara zitakazojali maslahi ya nchi maskini na zile zinazoendelea. Hususan kanuni ambazo zitatambua ukweli kuhusu hali yetu ya maendeleo na unyonge wetu na kutupa fursa ya kukua na kuendelea. Tuendelee kuyakumbusha Mataifa tajiri kuhusu ahadi walizotoa Doha, Novemba 2001 kuhusu kuweka maslahi ya nchi maskini katika kila hatua zitakazochukuliwa kujenga mfumo wa biashara wa dunia.

Mheshimiwa Spika, Septemba, 2003, Mjini Cancun, Mexico kutafanyika Mkutano wa Shirika la Biashara Duniani utakaohudhuriwa na Mawaziri wa Biashara wa nchi Wanachama wa *WTO*. Ni matumaini yetu pia kwamba Mawaziri wa Biashara wa Nchi zinazoendelea wataitumia nafasi hii kuyakumbusha Mataifa tajiri kutekeleza ahadi walizotoa Doha, Qatar. Pia waendelee kudai wakubwa wafungue masoko yao kikweli kweli, kwa bidhaa, hasa za kilimo kutoka nchi zetu. Hivi sasa masoko hayo hayajawa huria hasa kwa mazao ya kilimo kutokana na ruzuku kubwa inayotolea kwa wakulima wa nchi zao na masharti mengine mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa ajili hiyo, nchi zetu haziwezi kuuza mazao ya kilimo wala mifugo katika nchi tajiri kwa sababu bei za wenzetu ziko chini kuliko zetu kwa sababu ya ruzuku. Wanazuia kilimo cha nchi zetu kukua, kwa mfano, wafugaji wa nchi za Ulaya, Marekani na Japan wanapata ruzuku ya Dola 3 za Kimarekani mpaka Dola 7 kwa ng'ombe kwa siku, wakati watu bilioni 1.5 duniani wanaishi kwa chini ya Dola 1 ya Kimarekani kwa siku au watu bilioni 2.5 wanaishi kwa chini ya Dola 2 za Kimarekani kwa siku. Kwa jumla Mataifa tajiri ya Ulaya na Marekani yanatoa ruzuku ya Dola za Kimarekani bilioni 1 kwa siku kwa wakulima wao jambo ambalo linafanya bei ya mazao yao ya kilimo kuwa ndogo kuliko zetu isivyostahili! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ama kweli maskini hana haki mbele ya mwenye nacho. Wakubwa hao ambao ni hodari wa kuhubiri sera za biashara huria hawako tayari kuruhusu mazao ya kilimo kutoka nchi zetu kuingia katika masoko yao. Haya yote yanatukumbusha umuhimu kwa nchi zetu kushirikiana zaidi katika kudai haki zetu.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni mwanachama wa ushirikiano wa kanda wa aina tatu. Kwanza kabisa ni mwanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika *(SADC),* pamoja na nchi nyingine 13. Pili, ni mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC)* pamoja na wenzetu wa Kenya na Uganda. Tatu ni mwanachama wa Umoja wa Nchi zinazopakana na Bahari Kuu ya Hindi *(Indian Ocean Rim Association of Regional Cooperation – IOR-ARC)* unaojumuisha nchi 19.

Mheshimiwa Spika, Jumuiya ya nchi zinazopakana na Bahari Kuu ya Hindi inaendelea na mikakati ya kukuza biashara na uwekezaji katika nchi Wanachama. Pia umoja huo unaendelea kuimarisha Sekretarieti yake iliyoko Mauritius ili kuongeza ufanisi.

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya kutia moyo yamefikiwa katika ujenzi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Ushirikiano baina ya nchi zetu unazidi kuimarika. Sekretariati, Bunge na Mahakama vimeendelea kuimarishwa kwa kuongezewa watendaji. Maslahi ya Wabunge na Majaji yameboreshwa. Mishahara ya Wabunge imeongezwa kutoka Dola 1,000 kwa mwezi na kuwa Dola 2,000 kwa mwezi. Posho za Majaji zimeongezwa na kuwa Dola 250 kwa siku kwa Rais wa Mahakama, Dola 225 kwa Makamu wake na Dola 200 kwa Majaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati za Kisekta zimeendelea kukutana na maamuzi muhimu kuchukuliwa. Kunako Aprili, 2003 Mkutano Maalum wa Nchi Wanachama na Wahisani kuhusu Sekta ya Mundombinu ulifanyika Mjini Arusha. Mkutano huo uliofunguliwa na Rais Benjamin William Mkapa wa Tanzania ulifanya tathmini ya maendeleo ya utekelezaji wa mradi wa Barabara ya Afrika Mashariki tangu mwaka 1998 hadi sasa na kuangalia ushirikiano katika Sekta ndogo za reli, usalama wa anga na simu. Matokeo

yake yalikuwa ya kutia moyo. Wahisani walionyesha nia ya kuendelea kutusaidia katika kuimarisha miundombinu.

Mheshimiwa Spika, tarehe 20 Juni, 2003 kikao cha dharura cha Wakuu wa Nchi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kilifanyika Mjini Nairobi, Kenya. Kikao hicho cha kwanza kufanyika tangu Rais Mwai Kibaki achukue uongozi wa Kenya kiliongozwa naye. Kikao hicho kilifanya kazi tatu. Kwanza kilifanya uamuzi kuhusu Uenyekiti wa Jumuiya baada ya Rais Daniel arap Moi wa Kenya aliyekuwa Mwenyekiti kwa kipindi kirefu kustaafu. Viongozi wetu walikubaliana kufuata utaratibu wa mzunguko na kwamba Rais Yoweri Museveni wa Uganda ataanza na kufuatiwa na Rais Benjamin William Mkapa wa Tanzania. Baadaye atafuata Rais Mwai Kibaki wa Kenya.

Mheshimiwa Spika, katika kikao hicho pia, Wakuu wa Nchi walifanya uamuzi wa mwisho kuhusu kiwango cha juu cha ushuru wa forodha kwa bidhaa zitakazotoka nje ya Jumuiya kuwa asilimia 25. Uamuzi huo umekamilisha zoezi la kufanya maamuzi ya msingi kuhusu kuanzishwa kwa Umoja wa Forodha wa Afrika Mashariki. Hivyo basi, ushuru wa forodha chini ya umoja huo utakuwa 0, 10 na 25. Kabla ya hapo majadiliano ya nchi Wanachama yalikamilisha maeneo yote muhimu kuhusu Umoja wa Forodha kama vile utaratibu wa kupunguza ushuru mpaka kufikia 0 na uasili wa bidhaa.

Baada ya uamuzi wa Nairobi, kazi iliyo mbele yetu sasa ni kukamilisha rasimu ya itifaki ya kuanzisha umoja huo. Kazi hiyo itakamilika ifikapo Novemba, 30, 2003 ambapo wakuu wa nchi zetu watatia saini makubaliano ya itifaki hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulikwishakubaliana huko nyuma kuwa bidhaa za kutoka Tanzania na Uganda zitaingia katika soko la Kenya bila kutozwa ushuru. Lakini bidhaa kutoka Kenya zitakapoingia katika soko la Tanzania na Uganda zitatozwa ushuru kwa kipindi cha miaka mitano kabla ya kuingizwa bila ushuru. Hii imewekwa ili kulinda bidhaa na viwanda vya Tanzania na Uganda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kadhalika tumeshaelewana juu ya bidhaa zipi za Kenya, zitakazoanza mara moja na ushuru wa sifuri na bidhaa zipi zitalipiwa ushuru kwa hiyo miaka mitano. Vile vile, tumekubaliana kuhusu kanuni zitakazotumika kutambua uasili wa bidhaa. Shabaha ya utaratibu huu ni kuzuia wanachama kudhulumiana na kudanganyana kuhusu bidhaa zilizozalishwa nje ya Afrika Mashariki na kuzifanya zao wakati zitakuwa zinapitia tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kazi ya kufanya mabadiliko ya muundo wa *SADC* Makao Makuu imekamilika. Idara mbili zaidi zimeshaundwa katika Sekretariati ya *SADC*. Vile vile, Kamati Maalum ya Mawaziri *(Integrated Committee of Ministers)* imeshazinduliwa Machi, 2003 Mjini Luanda, Angola. Hapa nchini, Kamati ya Kitaifa ya *SADC* ya kuratibu shughuli zote za Jumuiya hiyo imekwishaundwa na ilizinduliwa rasmi na Waziri Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha tarehe 16 Agosti, 2002. Wadau wote kutoka Sekta zote, jinsia zote Bara na Visiwani wamejumuishwa katika Kamati hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kazi ya kutayarisha Mkakati wa Maendeleo ujulikanao kama *The Regional Indicative Strategic Plan* inafikia ukingoni. Rasimu imekamilika na inatarajiwa kuamuliwa na kuzinduliwa rasmi wakati wa vikao vitakavyofanyika Dar es Salaam, Agosti, 2003.

Mheshimiwa Spika, katika mkutano uliopita wa Wakuu wa Nchi ulifanyika Luanda, Angola Oktoba, 2002, Tanzania iliteuliwa kuwa Makamu wa Mwenyekiti badala ya kuwa Mwenyekiti wa Chombo cha *SADC* cha Siasa, Ulinzi na Usalama kama ilivyoamuliwa hapo awali. Kwa mujibu wa utaratibu huo basi Tanzania inatarajiwa kuwa mwenyeji wa Mkutano wa *SADC* mwaka huu wa 2003. Kwa mujibu wa utaratibu huo basi, Tanzania itakuwa na Mwenyekiti wa *SADC* kwa kipindi cha mwaka mmoja kuanzia Agosti mwaka huu 2003 hadi Agosti, 2004. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kupokea uamuzi huo tulianza kazi ya maandalizi ya Mkutano huo ambao kwa kawaida hutanguliwa na Mkutano wa Maafisa Waandamizi na Mkutano wa Baraza la Mawaziri. Vikao hivyo vimepangwa kufanyika Dar es Salaam kuanzia Agosti 19 mpaka 26, 2003. Matayarisho yanaendelea vizuri na ni dhamira yetu kuhakikisha kuwa mkutano unakuwa wa mafanikio ya

hali ya juu. Ni heshima kubwa sana kwa Rais wetu na nchi yetu hii kwa kupewa dhamana hii. Ni heshima pia kwa Tanzania na Watanzania kufikiriwa kupewa jukumu hilo hivyo hatuna budi kuenzi matumaini hayo. Sina shaka kuwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu na Watanzania wote kwa jumla tutaendelea kumuunga mkono na kumsaidia Rais wetu kufanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uhusiano na ushirikiano wa Tanzania na nchi nyingine katika mabara yote duniani ni mzuri. Ni dhamira ya Wizara yangu na Wanabalozi wetu wote kuidumisha hali hiyo na hasa kuifanya iwe bora zaidi. Kiwango cha uhusiano na ushirikiano kinatofautiana kati ya nchi na nchi hata hivyo hakuna nchi yoyote duniani ambayo tunaweza kusema ni adui wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, uhusiano na ushirikiano wetu na nchi jirani ni mzuri sana. Sera ya ujirani mwema imefanikiwa. Hata Burundi ambayo baadhi ya nyakati husikika vijineno vinavyoleta sura ya kuwepo tatizo nadiriki kusema kuwa hali si mbaya kama inavyodhaniwa. Kuna mawasiliano mazuri baina ya Serikali za nchi zetu na ushirikiano wa kiuchumi na kibiashara unaendelea vema. Kama ilvyo kwa nchi zote jirani uhusiano na ushirikiano wetu na nchi za kanda zetu za ushirikiano wa kiuchumi ni mzuri.

Mheshimiwa Spika, katika mkakati wetu wa kuendeleza na kuimarisha uhusiano na ushirikiano na nchi mbalimbali duniani tumekuwa tunatumia njia kuu tatu. Nji ya kwanza ni kuwa na uhusiano wa Kibalozi na Mataifa duniani na kuwa na Ofisi za Kibalozi katika baadhi ya nchi hizo. Wakati mwingine pia tumetumia Makonseli wa Heshima. Njia ya pili ni kuwa na makubaliano na Mikataba ya Ushirikiano kama vile utaratibu wa mashauriano kwa nyakati maalum *(Regular consultations)* na Tume za Pamoja za Ushirikiano *(Joint Permanent Commissions of Cooperation).* Tatu, ni ziara za viongozi wa nchi zetu kutembeleana.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ina uhusiano wa Kibalozi na zaidi ya Mataifa 150 duniani na makusudio yetu ni kufanya hivyo kwa Mataifa yote duniani. Tunazo Ofisi za Ubalozi 28 kote duniani. Kati ya hizo 12 zipo Afrika, 8 zipo Ulaya, 3 ziko Marekani, 3zipo Asia na 2 zipo Mashariki ya Kati. Idadi ya Balozi itaongezeka kufuatia uamuzi wa hivi karibuni uliofanywa na Rais wetu wa kufungua Ubalozi nchini Malawi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uamuzi huo wa busara umerekebisha kasoro iliyokuwa inajitokeza ya Malawi kuwa nchi pekee katika nchi zinazopakana na Tanzania ambako hatukuwa na Ubalozi. Pia unatuongezea uwezo wetu wa mawasiliano na ushawishi hasa wakati huu ambapo nchi zetu mbili zina mashauriano ya kina kuhusu kuimarisha uhusiano wetu na kutatua matatizo ya kimsingi kuhusu mpaka baina ya nchi zetu.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana nililiarifu Bunge lako Tukufu kuhusu uamuzi wa kufungua tena Ubalozi wetu nchini Uholanzi. Kama nilivyokwishaeleza huko mwanzoni, tuliahirisha kufanya hivyo kwa sababu ya tatizo maalum tulilolipata la kukosa fedha za kuendeleza ujenzi uliokuwa umeshaanza na unaendelea katika Chuo cha Diplomasia na kwa maelewano na wenzetu wa Hazina tulihamisha fedha hizo na kuzipeleka katika kukamilisha kazi hiyo kule chuoni. Tunatarajia mwakani tunaweza kufungua Ubalozi huo. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa, bado dhamira yetu ya kufungua Ubalozi Oman, Malaysia na Brazil haijabadilika. Tutaitekeleza katika miaka ijayo kutegemea upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Tume za Kudumu za Ushirikiano, nchi yetu ina mikataba na ina utaratibu huo na nchi zaidi ya 18 duniani nyingi zikiwa Barani Afrika. Tume za Ushirikiano zimekuwa chombo muhimu cha kupanga na kuratibu ushirikiano kati ya nchi yetu na Mataifa rafiki. Zimesaidia sana kuendeleza maslahi ya kisiasa, kiuchumi na kiusalama ya nchi yetu. Tutajitahidi kurekeibsha kasoro zilizopo sasa ili tuweze kutumia kwa ukamilifu manufaa ya utaratibu huu. Katika mwaka wa fedha uliopita tulifanya mikutano ya Tume hizo na Botswana, Zambia, Yemen, India na Malawi. Mwaka huu tunapanga kufanya mikutano na Afrika Kusini, Cuba na Nigeria.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka uliopita Rais wetu Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, alifanya ziara rasmi mbili nchini India na Malawi. Pia ameshafanya ziara za kikazi Afrika Kusini, Uswiss, Italia, Ufaransa, Angola, Uganda, Kenya na Burundi. Makamu wa Rais Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein amefanya ziara ya kikazi Lesotho kuhudhuria Mkutano wa *SADC* wa kudhibiti Ukimwi. Waziri

Mkuu Mheshimiwa Frederick Sumaye, alifanya ziara ya kikazi huko Venice Italia kuhudhuria Mkutano wa *UNIDO*.

Mheshimiwa Spika, Rais wa Zanzibar Mheshimiwa Amani Abeid Karume, alitembelea China kwa ziara rasmi na Malaysia kwa ziara ya kikazi. Katika kipindi hicho hicho nchi yetu ilibahatika kutembelewa na Marais sita kwa ziara rasmi nao ni Rais Festus Mogae wa Botswana, Rais Joachim Chissano wa Msumbiji, Rais Daniel arap Moi wa Kenya, Rais Tarja Harlonen wa Finland, Rais Mwai Kibaki wa Kenya na Rais Bakili Muluzi wa Malawi. Marais wa Afrika Kusini, Uganda, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Ethiopia na Rwanda, wamefanya ziara za kikazi nchini. Kadhalika Makamu wa Rais wa Afrika Kusini na Gabon nao wamefanya ziara za kikazi nchini.

Mheshimiwa Spika, aidha, tulibahatika kutembelewa na Mawaziri wa nchi mbalimbali duniani na Mawaziri wetu wamefanya ziara katika nchi mbalimbali. Hivi karibuni nilitembelea Urusi kwa mwaliko wa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje wa nchi hiyo Mheshimiwa Igor Ivanov. Ilikuwa ziara ya mafanikio makubwa. Tulikubaliana kufufua uhusiano wa miaka mingi baina ya nchi zetu ambao ulikuwa unaelekea kusinzia. Walikubali kutufutia sehemu kubwa ya deni lao kwa karibu asilimia 67. Walikuwa wanatudai karibu Dola milioni 129, ukitoa sehemu ambayo tutalipa, sasa deni letu litabakia kuwa Dola milioni 20. Pia walikubali kutuongezea nafasi zaidi za masomo ya juu na kukuza biashara kati yetu, kwani wanataka tuwauzie matunda, samaki, kamba, kahawa, chai na korosho. Kwa ajili hiyo tumekubaliana Vyama vya Wafanyabiashara wa nchi zetu washirikiane kwa karibu zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni mwanachama wa Mashirika na Asasi mbalimbali za Kimataifa kama vile Umoja wa Afrika, Umoja wa Mataifa, Jumuiya ya Madola, Umoja wa Nchi Zisizofungamana na Upande wowote, Kundi la 77, Tume ya Ushirikiano wa Nchi za Kusini na mengine mengi. Tanzania itaendelea kuwa mwanachama wa Mashirika na Asasi hizi muhimu kwani zinatoa nafasi muhimu ya kutetea na kuendeleza maslahi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Umoja wa Afrika umetimiza mwaka mmoja tangu kuasisiwa kwake huko Durban, Afrika Kusini tarehe 9 Julai, 2002. Kazi ya kuijenga kimuundo inaendelea vizuri. Katika kikao cha pili cha Wakuu wa Nchi za Umoja huo kilichofanyika Maputo, Msumbiji tarehe 10 mpaka 12 Julai, 2003 kazi ya kuunda Kamisheni yake imekamilika kwa kuwachagua watendaji wake wakuu. Mheshimwa Alfa Omar Konare, Rais wa zamani wa Mali alichaguliwa kuwa Mwenyekiti na Mheshimiwa Patrick Mazimhaka wa Rwanda, alichaguliwa kuwa Makamu wake. Kadhalika uchaguzi wa Makamishna wa Kamisheni za umoja huo ulifanyika. Tunawapongeza wote waliochaguliwa na kuwahakikishia ushirikiano wetu.

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri Mtanzania mwenzetu Mama Rosebud Kurwijila alichaguliwa kuongoza Kamisheni ya Uchumi Vijijini na Kilimo *(Rural Economy and Agriculture).* Katika mkutano huo pia Tanzania ilipata ushindi mwingine mnono kufuatia Ndugu Tom Nyanduga kuchaguliwa kuwa Mjumbe wa Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu yenye makao yake makuu nchini Gambia. Napenda kuitumia nafasi hii kwa mara nyingine tenaa kuwapongeza Mama Rosebud Kurwijila na Ndugu Tom Nyanduga, kwa ushindi wao. Mafanikio yao hi ushindi wetu sote na heshima kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haikuwa kazi rahisi kufanikisha ushindi huu kwa sisi tuliohusika moja kwa moja na shughuli ya kuwaombea kura. Juhudi, maarifa na uhusiano mzuri na Mawaziri wenzetu vimesaidia sana. Napenda kutumua nafasi hii kuwashukuru Wajumbe wote wa Ujumbe wa Tanzania tuliohangaika nao katika harakati hizo.

Napenda pia kutambua mchango wa Wabunge wenzetu wawili tuliokuwa nao Maputo wakati huo yaani Mheshimiwa Dr. William Shija, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nchi za Nje na Mheshimiwa Ali Ameir, Mjumbe wa Kamati hiyo. Ushauri wao na busara zao vimechangia kwa kiasi kikubwa katika ushindi huu. Shukrani maalum zimwendee Rais wetu kwa kuiweka nchi yetu katika hadhi ya kukubalika na hivyo kuwezesha Watanzania wenzetu hao kuchaguliwa.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Januari, 2003 Mjini Addis Ababa, Ethiopia kilifanyika kikao cha dharura cha Wakuu wa Nchi wa Umoja wa Afrika. *Agenda* kuu ya

kikao hicho ilikuwa kujadili mapendekezo ya marekebisho ya Katiba ya Umoja huo. Miongoni mwa marekebisho muhimu yaliyofanywa katika Katiba hiyo ni kuingiza rasmi lugha za Kiswahili na Kihispania kuwa lugha rasmi za Umoja wa Afrika pamoja na Kiarabu, Kifaransa, Kiingereza na Kireno.

Hivyo basi mtu sasa anaweza kutumia lugha ya Kiswahili katika vikao ya Umoja wa Afrika. Changamoto kubwa iliyo mbele yetu ni kufanya matayarisho ya kuwezesha lugha hiyo kutumika. Wizara yangu inashirikiana na Wizara husika, *BAKITA* na Taasisi ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Taasisi ya Kiswahili na Lugha ya Kigeni huko Zanzibar kufanikisha jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kikao cha Maputo taarifa ya maendeleo ya uundaji wa Asasi nyingine muhimu za Umoja wa Afrika ilitolewa. Kwa mujibu wa taarifa hiyo kasi hairidhishi kwa upande wa uridhiaji wa Itifaki zinazounda Bunge la Afrika na Baraza la Amani na Usalama la Afrika. Nchi wanachama zimehimizwa kuridhia itifaki hizo muhimu ili ziweze kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri sisi tumesharidhia Itifaki ya Bunge la Afrika na ni Wajumbe wa *Steering Committee* ya kuanzisha Bunge hilo kupitia kwa Spika wetu. Waliniambia kwamba wangependa sana Spika wetu awe Mwenyekiti wa hiyo *Steering Committee*, lakini inaonekana anakataa kataa na nimeombwa rasmi nije nimuombe akubali. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Afrika Kusini imejitolea kuwa mwenyeji wa Bunge hilo Mjini Cape Town. Hatua muhimu za kufikisha Bungeni Itifaki ya Baraza la Amani na Usalama la Afrika kwa ajili ya kuridhiwa zimekamilika. Inayosubiriwa ni siku muafaka.

Mheshimiwa Spika, Tanzania inathamini sana uanachana wake katika Umoja wa Mataifa na tutaendelea kuunga mkono. Tunafanya hivyo kutokana na kutambua umuhimu wa Umoja wa Mataifa kwa nchi yetu na kwa Mataifa yote duniani. Tanzania imenufaika sana na uanachana wake katika umoja huo. Kupitia Mashirika yake nchi yetu imepata misaada mingi ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Kupitia Shirika lake la Wakimbizi, Tanzania imeweza kusaidiwa katika kubeba mzigo mzito wa majirani zetu wanaozikimbia nchi zao. Tunaahidi kuendelea kuwa wanachama waaminifu kuutetea Umoja wa Mataifa.

Mheshimiwa Spika, Tanzania pia itaendelea kudai marekebisho ya Mkataba wa Wakimbizi wa mwaka 1961 ili uweze kuziwajibisha ipasavyo nchi zinazotoa wakimbizi na Jumuiya ya Kimataifa kwa jumla. Kwa jinsi ulivyo sasa, Mkataba huo umezielemea sana nchi zetu zinazopokea wakimbizi. Tunadhani hii siyo sawa na haifai kuendelea hivyo ilivyo. Tunafurahi kuwa rai hiyo ya Tanzania imekopekelewa vizuri katika Shirika la Wakimbizi na inaungwa mkono na nchi kadhaa duniani. Tunaomba kasi iongezwe ili marekebisho yafanywe mapema iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu wakimbizi walioko nchini, napenda kutumia nafasi hii kuomba Jumuiya ya Kimataifa kutatua haraka tatizo la kupungua sana kwa huduma hasa ya chakula kwa wakimbizi. Ni hali inayosikitisha sana. Kuna wakati huduma hiyo ilishuka na kuwa asilimia 65 tu ya stahili yao na baadaye baada ya kupiga kelele ikaongezwa hadi kufikia asilimia 72. Ni vema Jumuiya ya Kimatafia ikatambua kuwa kuwapunguzia wakimbizi stahili yao ni kichocheo kikubwa kwa wakimbizi kutoka nje ya kambi na kufanya vitendo vya uhalifu ambavyo vinatuudhi na kutukera sana.

Mheshimiwa Spika, sote tunakumbuka mchango wa Jumuiya ya Madola katika kusaidia kupatikana kwa Muafaka wa kwanza kuhusu mzozo wa kisiasa Tanzania Zanzibar. Jumuiya ya Madola iliahidi kuisadiia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuapata fungu la kulipa fidia kwa watu waliobomolewa nyumba zao huko Zanzibar.

Katika Muafaka wa Pili, Jumuiya ya Madola imeahidi kusaidia Kamati ya Pamoja ya Muafaka na kuimarisha Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar. Lakini bahati mbaya bado hawajafanya hivyo. Wizara yangu imekuwa inafuatilia kwa karibu sana kwa Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Madola kuhusu utekelezaji wa ahadi hizo ili kuhakikisha kwamba zinatimia. Wakati wote Katibu Mkuu, Don Macknnon amekiri kutambua ahadi hizo na kuahidi kuwa watazitekeleza. Mimi na wenzangu Wizarani hatutachoka kufuatilia ili kuhakikisha kwamba ahadi hiyo inatimia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Tanzania kama zilivyo nchi nyingine wanachama, tunaendelea na maandalizi ya kushiriki mkutano ujao wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Madola utakaofanyika Desemba 2003 huko Abuja, Nigeria. Pamoja na *agenda* za kawaida na mambo mengine kikao hicho kitapokea na kujadili taarifa na mapendekezo ya Kamati ya Utatu (Troika) iliyokuwa inashughulikia suala la Zimbabwe. Ni matumaini ya Tanzania kuwa suala hilo litashughulikiwa vizuri ili lisije likawa chanzo cha kuleta mpasuko katika umoja na mshikamano wa Jumuiya ya Madola.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ilishiriki katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi Zisizofungamana na Upande Wowote uliofanyika Mjini Kuala Lumpur, Malaysia Februari, 2003. Ujumbe wa Tanzania kwenye mkutano huo uliongozwa kwa umahiri mkubwa na na Rais wa Zanzibar; Mheshimiwa Amani Abeid Karume. Mafanikio makubwa yalipatikana katika mkutano huo katika masuala mbalimbali ya maendeleo na mshikamao wetu. Mkutano huo pia ulidhihirisha kuwa umoja huu bado ni imara na ni muhimu kwa maendeleo na maslahi ya nchi wanachama. Kadhalika ushirikiano wa nchi maskini ulitiwa mkazo bila ya kupuuza ushirikiano wa nchi hizo na nchi jirani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mkutano huu Tanzania ilisisitiza umuhimu wa kuendelza mshikamano wetu ili kufanikisha malengo yake. Kadhalika tulitahadharisha juu ya pendekezo la kutaka kuwa na Sekretarieti ya Kudumu ya *NAM*. Tulishauri tujipe muda wa kutosha ili tutafakari vizuri.

Mheshimiwa Spika, tarehe 5 mpaka 7 Agosti, 2002 Tanzania ilishiriki kwenye mkutano wa Mawaziri wa Nchi Maskini sana Duniani uliofanyika Cotonou, Benin. Mkutano huu ulifanya tathmini ya utekelezaji wa mpango wa kuondoa umaskini kwa nchi hizo yaani *Programme of Action on Poverty Eradication.*

Vile vile uliangalia mafaniko ya kupunguza umaskini na kuziandaa nchi maskini kushiriki katika mikutano ya Kimatafia. Kwa kiasi fulani mkutano uliweka msingi mzuri wa kufuatilia utekelezaji wa ahadi za Jumuiya ya Kimatafia kuhusu kupambana na umaskini na maendeleo duni kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu ilishiriki katika mkutano wa Baraza la Wawakilishi wa Tume ya Ushirikiano wa Nchi za Kusini *(South Centre)* kuanzia tarehe 22 hadi 23 Juni, 2002, Geneva, Switzerland.

Mkutano huo uliitishwa kutafuta mikakati ya kupata fedha za kuendesha kituo kwa miaka mitatu tangu 2003 hadi 2005. Mkutano ulikubaliana kuzihimiza nchi wanachama kutimiza wajibu wao wa kugharamia kituo hicho. Pia, uliuona umuhimu wa kutafuta njia nyingine za kuchangia fedha za kuendesha kituo, mbali na michango ya Wanachama, Tanzania imekwishatoa mchango wake wa Dola 100,000 na tutaendelea kushirikiana na wenzetu kuhakikisha kuwa kituo hicho ambacho Baba wa Taifa letu, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, alikuwa Muasisi na Kiongozi wake kinaendelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Mahakama ya Kimataifa ya Makosa ya Jinai imeanza kazi zake rasmi Machi, 2003. Tanzani imeshiriki katika vikao viwili cha mwezi wa Februari mwaka 2003 ambacho pia kiliwachagua Majaji 18 wa Mahakama hii. Ni matumaini yetu kwamba Mahakama itasaidia katika kulinda amani, usalama na utawala wa sheria duniani kote.

Mheshimiwa Spika, kama Waheshimiwa Wabunge wenzangu watakavyokumbuka tarehe 27 Februari, 2002, Rais wetu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa na Rais wa Jamhuri ya Finland, Mheshimiwa Tarja Halonen wakiwa na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Kazi Duniani *(ILO),*Bwana Juan Somavia, walizindua rasmi Tume ya Kimataifa kuhusu Masuala ya Kijamii na Utandawazi. Mpaka sasa Tume hiyo imefanya kazi yake vizuri na inatarajiwa kuikamilisha mwezi Agosti, mwaka huu 2003.

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia nafasi hii kumpongeza kwa dhati kabisa Rais wetu kwa kazi nzuri aliyoifanya. Imemjengea jina zuri katika medani ya Kimatafia na ameleta heshima kubwa kwa Taifa letu. Yeye na Rais wa Finland, watakumbukwa daima katika historia ya dunia yetu.

Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa ushirikiano waliompa Rais wetu katika jukumu lake hilo zito. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kufuatia kazi nzuri aliyofanya Rais wetu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, nchi yetu imepewa heshima nyingine katika nyanja za Kimataifa. Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa wa Tanzania ameteuliwa kuwa Mwenyekiti Mwenza pamoja na Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje wa Finland Mheshimiwa Errki Tuomioja kuongoza *High Level Goup on Global Governance and Democracy.*

Mheshimiwa Spika, jopo hilo linalojumuisha watu mashuhuri duniani kutoka Serikali, Mashirika ya Fedha ya Kimataifa (Benki ya Dunia na *IMF*) Umoja wa Mataifa, *WTO*, Wasomi na Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali linatarajiwa kuanza kazi yake Septemba, 2003 kwa miaka miwili. Kwa namna yake jopo hili pia litasaidia kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo ya Tume ya Rais Mkapa na Rais Halonnen watakapomaliza kazi mwezi Agosti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 2000 Tanzania ilitia saini Mkataba wa Kimataifa dhidi ya mabomu ya ardhini. Mkataba huo ulikuwa unazitaka nchi kuacha kutumia kutengeneza na kuhifadhi mabomu ya kutega ardhini. Mabomu ya kutega ardhini yamekuwa chanzo cha watu wengi kupoteza maisha na mamilioni kuwa walemavu wa kukosa baadhi ya viungo mwilini.

Nafurahi kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa nchi yetu imeanza kutekeleza wajibu wake na kwamba tayari tumeshaharibu mabomu 9,837 na imeazimia kumaliza yaliyosalia katika kipinidi cha miaka miwili ijayo. Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi ataelezea kwa upana zaidi kesho.

Mheshimiwa Spika, mikakati ya kudhibiti kuenea na matumizi ya silaha ndogo inaendelea kutekelezwa. Silaha hizo ndizo zinazochochea na kuendeleza vita baina ya mataifa, ndani ya nchi na pia hutumika katika mashambulio ya uhalifu.

Mheshimiwa Spika, Tanzania iko mstari wa mbele katika udhibiti wa silaha hizi na mpango wake kwa ajili hiyo umepongezewa na kupigiwa mfano. Bahati mbaya sana ushiriki wa nchi zinazotengeneza silaha hizo bado hauridhishi na hivyo kuleta kasoro kubwa kwa mafaniko ya mpango mzima wa kupunguza kuenea kwa matumizi ya silaha ndogo duniani.

Mheshimiwa Spika, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba uchapishaji wa vitabu vya Sera ya Mambo ya Nje vya lugha ya Kiingereza umekamilishwa na kila Mbunge atagaiwa nakala yake. Sasa hivi tunaendelea kushughulikia Kitabu cha Lugha ya Kiswahili.

Napenda pia nieleze kuwa Wizara imekwishaandaa mkakati na mwongozo wa utekelezaji wa sera hiyo. Mjadala kuhusu mkakati na mwongozo huo vitakuwa ni moja ya agenda kuu katika Kikao cha Mabalozi kilichopangwa kufanyika robo ya mwisho wa mwaka huu. Mwongozo wa utekelezaji utakuwa kigezo muhimu cha kupima utekelezaji wa sera ya Mambo ya Nje na majukumu mbalimbali ya Balozi zetu na Wizara yangu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, tumekamilisha zoezi la kutazama upya muundo wa Wizara Makao Makuu na katika Balozi zetu nchi za nje na kufanya marekebisho muafaka. Katika mabadiliko hayo shughuli zote za ushirikiano wa kanda kama vile Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika na Umoja wa Nchi zinazopakana na Bahari Kuu ya Hindi zimeunganishwa chini ya Idara mpya ya Ushirikiano wa Kiuchumi wa Kikanda *(Directorate of Regional Co-operation).* Aidha katika Idara ya Habari, Sera na Mipango sehemu ya Habari imeondolewa na hivyo sasa tunakuwa na Idara ya Sera na mipango pekee. Kimeundwa kitengo kipya cha Habari, Elimu na Mawasiliano. Pia kimeundwa Kitengo cha Sheria ambacho zamani kilikuwa sehemu ya Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa. Muundo huo umeanza kutumika tangu Julai 1, 2003.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inakabiliwa na upungufu mkubwa wa watumishi kutokana na kuongezeka kwa majukumu na kupanuka kwa uwakilishi wetu nje. Katika kukabiliana na tatizo hilo tutaajiri watumishi wapya 10 katika mwaka huu wa 2003/2004. Lengo letu ni kuajiri watumishi wapya thelathini ifikapo mwaka 2005/2006 wakati huo huo tunakusudia kuomba Serikali itukubalie kupata

watumishi wenye uzoefu wa masuala ya Habari, Uchumi, Biashara, Sheria na Mazingira kutoka Wizara nyingine kwa njia ya uhamisho.

Mheshimiwa Spika, wakati huo huo tutaendelea na mpango wetu wa kuwaendeleza watumishi waliopo kwa kuwapa mafunzo zaidi vyuoni na kwa njia za semina na kuwapatia nafasi ya kushikizwa katika Wizara ya Mambo ya Nje za Nchi rafiki. Wizara pia itaendelea kuwapatia watumishi wake vitendea kazi vilivyo bora na vya kutosha. Kwa ajili hiyo tunao mpango wa kumpatia kila Afisa Wizarani na Balozini kompyuta mezani kwake na kumuwezesha kuitumia.

Mheshimiwa Spika, kuboresha maslahi ya watumishi ni muhimu sana kwa morali na utendaji kazi. Wizara itawathibisha kazini watumishi 11 na kuwapandisha vyeo watumishi 93 waliotimiza masharti ya miundo ya utumishi Serikalini. Tunakusudia kuziangalia upya Kanuni za utumishi na Mambo ya Nje na kuzirekebisha ipasavyo ili zikidhi matakwa ya wakati tulionao. Aidha Wizara itaangalia upya viwango vya posho za utumishi wa nje *(Foreign Service Allowances)* na kufanya marekebisho muafaka ili vilingana na hali ya maisha yaliyopo kwenye Balozi zetu.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Diplomasia kimeendelea kuimarisha kwa mitaala, wafanyakazi, vitendea kazi na majengo. Aidha, Chuo kimeshirikiana na vyuo vingine vya nje katika nyanja mbalimbali za kitaaluma za ufundishaji na utafiti. Katika mwaka wa fedha uliopita Chuo kimeweza kufanyiwa matengenezo makubwa ya majengo yake. Kazi hiyo hiyo, itaendelezwa mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, Bodi mpya ya Magavana imeteuliwa na kupewa jukumu la kukipa Chuo mwelekeo mpya wa kisasa. Lengo letu ni kukifanya chuo kiwe cha hadhi ya juu ili kiweze kuwa na mitaala ya stratejia na mafunzo mengineyo muhimu kwa uhusiano wa kimataifa kama vile uandishi wa hotuba na kadhalika. Kama vile uandishi wa hotuba na kadhalika. Aidha, tunataka chuo chetu kijengewe uwezo wa kuwa kituo cha ubingwa na ushauri kwa Serikali kwa masuala ya diplomasia na ushirikiano wa kimataifa.

Mheshimiwa Spika, *AICC* ndilo shirika pekee chini ya Wizara yangu. Ni shirika linaloendeshwa kwa ufanisi mkubwa na hali yake ya ukwasi ni nzuri. Shirika hilo halitegemei ruzuku kutoka Serikalini. Katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, kituo kimeweza kuwa mwenyeji wa wastani wa mikutano 120 kwa mwaka na kuleta wageni 14,000. Kati ya mikutano hiyo asilimia 40 ni ya kimataifa na asilimia 60 ni ya Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, matarajio yetu ni kuendelea kuboresha huduma na kujitangaza zaidi ili kuvutia mikutano mingi zaidi kila mwaka. Menejimenti na Bodi imeandaa mpango wa maendeleo wa muda mrefu ambao Serikalini tumeuafiki. Kwa niaba ya Wizara yangu, napenda kuitumia nafasi hii kuwapongeza Wafanyakazi, Menejimenti na Bodi ya Wakurugenzi wakiwemo baadhi ya Wabunge wenzetu kwa kazi nzuri waifanyayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa muhtasari miongoni mwa kazi muhimu tulizopanga kufanya katika mwaka 2003/2004 ni kuandaa mpango kamambe wa utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje na majukumu mengine ya Wizara, kutengeneza mwongozo wa kazi na masharti ya sifa za kuwa Mwakilishi wa Heshima wa Tanzania, kushiriki katika kutangaza vivutio vya uwekezaji, utalii na kutafuta masoko ya bidhaa zetu nje, kushiriki katika utatuzi wa migogoro hasa ya nchi jirani na kushiriki katika mikutano na majumuiko muhimu ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, pia kuratibu ziara za nje za viongozi wa Kitaifa na za viongozi wa nchi za nje wanapotembelea Tanzania, kuimarisha uwakilishi wetu nje ya nchi, kutoa huduma mbalimbali kwa wafanyakazi, kurekebisha Kanuni za Utumishi wa maofisa wa mambo ya nje pamoja na kuangalia upya maslahi yao na kushirikiana na Idara Kuu ya Utumishi kuandaa mpango wa kuboresha utendaji kazi Wizarani.

Mheshimiwa Spika, tayari tumeshaandaa mpango kamambe wa maendeleo wa miaka 15 wa kununua na kujenga majengo katika Balozi zetu nje. Bahati mbaya Wizara haikupatiwa fedha za maendeleo katika bajeti mwaka huu. Tumeahidiwa kufikiriwa kwa huruma mwakani. Tumeelewa na tunaendelea kuvuta subira kwani wakati wote Mungu yuko pamoja na wenye subira.

Mheshimiwa Spika, ili Wizara yangu iweze kutekeleza majukumu na malengo yake ya mwaka 2003/2004 kama nilivyoeleza katika hotuba hii, sasa naomba Bunge lako Tukufu litafakari, lijadili na kisha liidhinishe jumla ya shilingi 32,079,101,100/=. Kati ya fedha hizo shilingi 1,156,330,700/= tunaziomba kwa ajili ya mishahara na shilingi 30,922,768,400/= kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. DR. WILLIAM F. SHIJA - MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NCHI ZA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni Na. 92 (2) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2003, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje, baada ya kupitia, kuchambua na kujadili utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa mwaka wa fedha uliopita 2002/2003 na mipango ya matumizi kwa mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nichukue fursa hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati kwa ushirikiano wao wakati wa kuchambua taarifa ya utekelezaji wa kazi za Wizara hii kwa mwaka uliopita na mipango ya Wizara kwa mwaka 2003/2004 mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, Wajumbe wa Kamati hii ni Mheshimiwa Peter Kabisa, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Balozi Ahmed Hassan Diria, Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mheshimiwa Ussi Yahya Haji, Mheshimiwa Rhoda Kahatano, Mheshimiwa *Capt.* Theodos Kasapira, Mheshimiwa Hassan Kigwalilo, Mheshimiwa Parseko Kone, Mheshimiwa Hadija Kusaga, Mheshimiwa Bernard Membe, Mheshimiwa Profesa Juma Mikidadi, Mheshimiwa Adelastella Mkilindi, Mheshimiwa Ali Ameir Mohamed, Mheshimiwa Benson Mpesya, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimwia Khadija Saleh Ngozi, Mheshimiwa Paul Ntwina, Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, Mheshimiwa Mwaka Abrahaman Ramadhani, Mheshimiwa Hashim Saggaf, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa ambaye ni Msemaji wa Upinzani kwa Wizara hii na mimi Mheshimiwa Dr. William Shija, Mwenyekiti wa Kamati hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje, napenda kutoa pongezi kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliochaguliwa hivi karibuni. Wote hawa tunawapongeza kwa ushindi wao na tunawatakia kazi njema za uwakilishi wao hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje ilipata nafasi ya kuchambua Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya mwaka 2002/2003 ya Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, wakati ilipokaa Mjini Dar es Salaam kuanzia tarehe 5 hadi 6 Juni, 2003.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji jukumu hili Kamati ilizingatia maeneo muhimu kama ambavyo yameonyeshwa katika taarifa yangu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji wa maagizo ya Kamati katika kikao chake cha mwezi Juni, 2002 Kamati ya Kisekta ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ya wakati huo ilitoa maagizo kadhaa ambayo yanahitaji kufanyiwa kazi li kuongeza ufanisi na kuboresha utendaji wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeweza kutekeleza na kutoa maelezo ya kina kama ilivyoagizwa na hivyo kamati kuridhika na utekelezaji huo. Kwa kifupi Kamati iliagiza Wizara kutekeleza mambo yafuatayo:-

Kwanza, Serikali iandae mkakati wa kudumu ili kuondoa kero ya mishahara kwa wafanyakazi wenyeji wa Balozi zetu *(Local Staff)* ikiwa ni pamoja na kulipa madeni kwa kuwa matatizo hayo yalikuwa yanalitia aibu Taifa letu.

Pili, kwa kuwa dunia sasa imekuwa na tatizo la ugaidi wa Kimataifa, Kamati ilishauri Serikali iandae na kuimarisha ulinzi wa kuaminika katika Balozi zetu.

Tatu, katika kutekeleza Diplomasia ya kiuchumi, Kamati ilishauri kuwa kuwe na mkakati madhubuti katika Balozi zetu nje ya nchi kwa kuvutia watalii na wawekezaji katia sekta mbalimbali za uchumi wetu.

Nne, kuendelea kufungua Balozi zetu nje ya nchi. Kwa taarifa tulizozipata na jinsi hotuba Mheshimiwa Waziri, ilivyoonyesha, utekelzaji wa maelekezo haya umeanza kuzaa matunda katika viwango na ngazi mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati vile vile ilielezwa kuwa hadi kufikia tarehe 30 Machi, 2003 jumla ya shilingi bilioni 3.96 zilikuwa zimekusanywa na Wizara. Ilikisiwa kuwa ifikapo mwezi Juni 2003, kiasi cha shilingi bilioni 3.927 zingekusanywa na kuvuka lengo lililokusudiwa la kiasi cha shilingi bilioni 3.57.

Katika hotuba yake, Waziri ameonyesha kwamba ukusanyaji wa maduhuli umefikia shilingi bilioni 5.57 na hivyo kuvuka lengo kwa takribani asilimia 150 lililokusudiwa. Kwa hiyo, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na watendaji wa Wizara yake, hususan Waheshimiwa Mabalozi wetu wote nchi za nje, kwa kazi nzuri ya kusimamia mapato ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Kamati kushiriki katika Mikutano ya Kimataifa, pamoja na mapendekezo mengine yaliyofanywa na Kamati miaka ya nyuma, Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa imeanza kuishirikisha Kamati yangu kwa Mikutano ya Kimataifa.

Kwa mfano, Kamati ilishirikishwa kwa mkutano wa Wakuu wa Nchi za *OAU* na kuingia *AU* mwaka 2002, uliofanyika huko Durban, Afrika Kusini na ule wa Wakuu wa Nchi za Umoja wa Afrika *(African Union)* mwaka huu Julai 1 hadi 12, 2003 huko Maputo, Msumbiji. Mikutano ya Wakuu wa Nchi kwa kawaida hutanguliwa na vikao vya wataalam na Baraza la Mawaziri. Tunapenda kushukuru sana kwa mpangilio huo wa Wizara na tunapenda uendelee. *(Makofi)*

Kwa kawaida Wabunge hushiriki kama wasikilizaji katika mikutano hii wakiwa sehemu ya Ujumbe wa Rais. Kwa kuangalia kwetu si nchi nyingi ambazo zinafanya utaratibu huu. Kwa mipango yetu Tanzania kwa mwaka huu hata mmoja wa viongozi wa Vyama vya Upinzani alikuwa sehemu ya Ujumbe wa Rais wa Tanzania. Hilo yeye mwenyewe aliyeshiriki alikuja akatoa pongezi nyingi sana kwa kushiriki katika mkutano huo wa Msumbiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inapenda kumpongeza sana Waziri kwa kufanikisha utaratibu huu wa kushiriki kwa Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo ambayo yametajwa na Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa katika hotuba yake, kuna masuala matano makubwa tuliyojifunza katika mkutano huo wa Maputo Msumbiji.

Kwanza, Tanzania bado ina marafiki wengi wanaoikumbuka na kuheshimu Uongozi wa Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere. Hiyo, ilionekana mnapokutana na Wajumbe mbalimbali, ukisema natoka Tanzania, wanasema ahaa! Nchi ya Mwalimu Nyerere, huo ndio unakuwa usemi wa mara kwa mara. Kwa sababu hiyo, kwa juhudi za viongozi wetu wa sasa na hasa Rais wetu Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, ndiyo pengine tukafanikiwa kupata Watanzania wawili kuchaguliwa kuingia katika uongozi wa Umoja wa Afrika*(AU),* yaani mwanaume mmoja na mwanamke mmoja. *(Makofi)*

Pili, viongozi wa Afrika bado hawajaafikiana vizuri kuhusu dira ya maendeleo ya Afrika na namna ya kuweka kipaumbele chini ya Umoja wa Afrika *(AU*). Ndiyo maana wengi wa viongozi hao waliona umuhimu wa kufanya kikao maalum kuzungumzia suala hilo hapo baadaye.

Tatu, programu ya *NEPAD* bado haijawekwa vizuri chini ya Umoja wa Afrika. Umetolewa muda wa miaka miwili kwa sekretarieti ya *NEPAD* kuoanishwa kwenye programu za Umoja wa Afrika (*AU).*

Nne, baada ya kufanyika mkutano wa maandalizi ya Bunge la Afrika *(The Meeting of African Parliaments on The Pan African Parliament)* huko *Cape Town*, Afrika Kusini tarehe 30 Juni – 1 Julai 2003, Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya Bunge la Afrika, Dr. Frene Ginwala, ambaye pia ni Spika wa Bunge la Afrika Kusini, alitoa taarifa kwenye Mkutano wa Wakuu wa Nchi huko Maputo Msumbiji. Katika taarifa hiyo aliwaomba Wakuu wa Nchi na Serikali za Umoja wa Afrika kufanya maamuzi juu ya Makao Makuu ya Bunge la Afrika na tarehe ya kuanza Bunge hilo.

Mkutano maandalizi ulikuwa umetoa wito kwamba nchi wanachama zikamilishe zoezi la kuridhia itifaki ya kuanzishwa kwa Bunge la Afrika ifikapo tarehe 31 Desemba, 2003, ili tarehe ya kuzinduliwa kwa Bunge hilo ipangwe. Idadi ya chini ya kuridhia inayotakiwa kwa Bunge la Afrika kuanza ni nchi 27. Katika Mkutano huo wa *Cape town* ndipo pale ambapo ulikuwa unatafutwa sana ili uweze kushiriki katika maandalizi hayo.

Tano, nchi wanachama wa Umoja wa Afrika ziliombwa kuridhia mapema iwezekanavyo itifaki ya kuanzisha Baraza la Ulinzi na Usalama la Afrika kama Mheshimiwa Waziri ambavyo ametaja *(Peace and Security Council).* Itifaki hiyo kwa sisi imekwishafikishwa mbele ya Kamati yangu na inaweza kuletwa Bungeni wakati wowote.

Mheshimiwa Spika, maoni, mapendekezo na ushauri wa Kamati. Baada ya kupitia na kuchambua kwa makini taarifa ya Wizara hii, yafuatayo ni maoni, mapendekezo na ushauri wa kamati ambao tunapenda ufanyiwe kazi katika kuboresha zaidi utendaji wa Wizara hii.

Kwanza, kwa kuwa Balozi zetu nje ya nchi zimekuwa na madeni mara kwa mara na kwa kuwa mfumo wa mgao wa fedha ulivyo sasa *(Cash Budget)* unapunguza kasi ya kazi za Balozi zetu, Serikali iangalie uwezekano wa kuipa Wizara hii fedha za robo mwaka. Suala hili linaonekana muhimu zaidi hasa kwa tatizo la kulipia pango kwa Balozi zetu ambapo pango huwa linatakiwa kulipiwa kwa mwaka mzima. Hii ni pamoja na kuruhusu matumizi ya maduhuli yanayotokana na pasi na viza. *(Makofi)*

Pili, Serikali ifanye uamuzi wa kuipa Wizara hii ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, fedha za maendeleo kila mwaka ili mipango yake ya maendeleo ifanyike kwa utaratibu unaofahamika. Kwa mfano, ni wajibu wa Tanzania kumiliki majengo yake ya Balozi zetu huko nje kama Mheshimiwa Waziri alivyoeleza. Lakini ni muda mrefu tumekusudia kujenga nyumba za Balozi zetu huko India, Kenya na sehemu zingine, lakini hatujatekeleza. Uwezekano wa kushirikisha mashirika yetu yaliyo na uwezo kama vile *NSSF* na *PPF* uangaliwe kwa kina.

Tatu, ili kutekeleza kikamilifu sera ya Diplomasia ya kiuchumi, Serikali ipanue wigo wa makundi ya kushirikisha kwa mfano, wafanyabiashara, Watanzania walio nje ya nchi na kadhalika. Hii ni pamoja na kuimarisha mawasiliano kati ya Serikli yetu na watu wanaotafuta taarifa za nchi yetu. Ni mara nyingi mno na nasema hapa wazi kwamba malalamiko yametolewa na watu walio nje, zikiwemo balozi zetu, kwamba barua zinazoandikwa Tanzania hazijibiwi upesi au hazijibiwa kabisa. Wanaoshiriki katika mikutano mbalimbali Waheshimiwa Wabunge, walioko hapa wengine ni mashahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nne, Wizara indelee na mipango ya kutaka kufungua Ubalozi wetu huko The Hague, Uholanzi na maeneo mengine duniani hususan Uarabuni, Asia na Amerika ya Kusini hasa Brazili. Hali kadhalika, tunaipongeza Serikali kwa uamuzi wa kufungua Ubalozi wetu nchi Malawi.

Tano, kwa kuwa Chuo cha Diplomasia cha Dar es Salaam kilikuwa kinamilikiwa na kinaendeshwa na nchi mbili yaani Tanzania na Msumbiji na kwa kuwa nchi ya Msumbiji imesitisha utoaji huduma na uendeshaji wa chuo hicho, Serikali ifanye juhudi za makusudi kuhakikisha kwamba hati miliki ya chuo hicho inawekwa mikononi mwa Tanzania. Aidha, Serikali ikamilishe mpango wa kuinua hadhi ya chuo hicho na kuwa cha mambo mengi ya diplomasia pamoja na kufanya utafiti.

Sita, Serikali iangalie upya sababu zilizopelekea Kituo cha Kimataifa cha Mikutano ya Arusha *(AICC)* kunyimwa na *PSRC* umiliki na uendeshaji wa Hoteli ya *Mount Meru*, kitendo ambacho tulidhani ni

kuwanyima Watanzania, nafasi ya kuendesha asasi zao na kuonyesha uwezo tulionao ndani ya nchi. *(Makofi)*

Saba, Tanzania iendeleze maamuzi ya kukaribisha Mikutano ya Kimataifa kama ule utakaofanyika hapa Tanzania wa Wakuu wa Nchi za *SADC* mwezi ujao na hivyo kuanza kujenga uwezo wa miundombinu itakayotegemewa katika maandalizi na matumizi ya rasilimali hizo kwa kazi zingine za Kimataifa.

Nane, Tanzania iendelee kutumia kikamilifu programu mbalimbali zinazoendeshwa na Balozi za nje hapa nchini na Mashirika ya Kimataifa yaliyopo hapa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, tisa, Wizara ifanye juhudi kuwasaidia Watanzania wengi zaidi kupata kazi kwenye Taasisi za Kimataifa. Hii ni pamoja na mbinu na maandalizi ya kupata sifa zinazotakiwa kwa mfano kama Mheshimiwa Waziri, alivyotaja kuanza mafunzo ya lugha mbalimbali za kimataifa kikiwemo Kifaransa, Kispaniola na kadhalika. *(Makofi)*

Kumi, Tanzania ifanye jitihada za makusudi za kuwa kiongozi katika Lugha ya Kiswahili Barani Afrika na Duniani. Tunadhani tusikubali Tanzania rasilimali hii ituponyoke kwa sababu matumaini ya kuwa na Afrika moja katika miongo mingi ijayo ni kwa Waafrika kutumia Lugha ya Kiswahili. Tuna sisitiza hivyo kwa sababu wenzetu Kenya na Sehemu nyingine wameanza kuzatiti zaidi katika kuonyesha kwamba wana uwezo wa kutumia Lugha ya Kiswahili kuliko Tanzania kitu ambacho tunafikiri tofauti. *(Makofi)*

Kumi na moja, Tanzania iendelee kushirikiana na nchi zingine wanachama wa Umoja wa Mataifa katika kurudisha hadhi na matumizi ya Umoja huo ili sauti ya wanyonge na wadogo iweze kusikika wakati wote. Hii nakubaliana na Mheshimiwa Waziri alivyotaja kwamba Mheshimiwa Rais wetu anaifanya kazi mara kwa mara na baada ya tukio la Iraq tunadhani kwamba umoja wa Mataifa umeteteleka Tanzania lazima iendelee na juhudi za kuonyesha kwamba umoja huo hauachwi pembeni bali unaendelea kuimarishwa.

Kumi na mbili, kwa kutambua umuhimu wa utalii hapa nchini ambao ni moja ya vyanzo vikubwa vya mapato katika nchi yetu, Wizara kupitia Balozi zetu, ifanye juhudi za makusudi za kuutangaza utalii na rasilimali zilizoko nchini. Fedha za maduhuli zitakazotumika kwa kazi ya kutangaza utalii zihesabike kama fedha za ziada kwa fungu la Wizara hii namba 34 jambo hili tunalitaja makusudi.

Kumi na tatu, kwa kuwa Sera ya Mambo ya Nje ya Diplomasia ya kiuchumi ni suala pana sana katika dhana nzima ya kupambana na umaskini, basi Wizara iongeze juhudi za kushirikiana na kushirikisha Wizara zingine kama vile Maliasili na Utalii, Viwanda na Biashara, Mawasiliano na Uchukuzi nakadhali ili kufikia lengo lililokusidiwa. Juhudi hizi ziwe ni pamoja na kulishirikisha zaidi Bunge lako tukufu.

Kumi na nne, kwa kuwa sera ya diplomasia ya kiuchumi ni dhana mpya katika jamii ya Watanzania walio wengi Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itoe elimu ya kutosha kwa wananchi, wakiwemo wafanyabiashara na makundi mengine nchini. Hii ni pamoja na kutafuta masoko na namna nzuri zaidi ya kushirikisha wageni katika kuendesha ushumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, Kamati inapenda kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, kwa kazi na juhudi kubwa alizofanya za kuondoa migogoro Afrika au kushughulikia usuluhishi wa migogoro hiyo, kushirikiana na majirani zake na kushiriki katika harakati za kisiasa na kiuchumi Kimataifa kwa ujumla. Rais ndiye msimamizi Mkuu wa Sera ya Mambo ya Nchi za Nje kama ilivyoainishwa na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili kwa mara nyingi tena, napenda kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Kikwete, Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na Mbunge wa Chalinze, Mheshimiwa Dr. Abdulkader Shareef, Naibu Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Ndugu Philemon Luhanjo, Katibu Mkuu wa Wizara yote kwa pamoja na watalaam wake, wakiwemo Waheshimiwa Mabalozi wetu nchi za nje kwa kazi nzuri ambayo wamefanya ya kuandaa kwa

makini na kwa ufanisi mkubwa mpango na bajeti hii na yale ambayo wanakusudia kutekeleza kwa mwaka ujao wa 2003/2004. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda niwashukuru sana na kuwapongeza Makamu Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Peter Kabisa, Mbunge wa Kinondoni na Wajumbe wote wa Kamati kwa ushirikiano wao katika kazi za Kamati ambazo mara nyingi huwa tunaitana mara nyingi na bila taarifa za awali, lakini huwa wanashiriki kwa moyo mkunjufu. Lakini tunampongeza vile vile Bwana Kheri Maulid ambaye ni Katibu wetu kwa juhudi zake na kwa kumudu pamoja na uchanga wake kazi za kuratibu vizuri wakati wa maandalizi ya taarifa hii na mambo mengine ya Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile Kamati yangu inakushukuru sana wewe pamoja na Tume ya Bunge kwa kukubali pendekezo la Kamati tulilotoa karibu miaka miwili iliyopita la kuwepo bendera mahsusi ya Bunge na Wabunge. Hiyo nakumbuka ilitokana na kazi uliyotutuma ya kutafuta au kuangalia itifaki ya Wabunge na Bunge kwa ujumla na kazi hiyo tulipoikamilisha tuliwasilisha taarifa kwako hatimaye imezaa matunda. Hatua hii Wabunge na Bunge kuwa na bendera yake tunadhani ni kubwa na muhimu sana katika kuliimarisha Bunge kama moja ya nguzo zetu tatu za uongozi na utawala Kitaifa. Tunakushukuru sana kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho baada ya uchambuzi uliofanyika na mapendekezo yaliyotolewa, Kamati kwa ujumla imekubaliana na mpango wa makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa mwaka wa fedha wa 2003/2004 na kuyakubali kama yalivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri Jakaya Kikwete, pamoja na kiasi cha fedha zilizoombwa katika Fungu Na. 34 Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ambazo ni jumla ya shilingi 32,079,101,100/=.

Mheshimiwa Spika, naomba kwasilisha na naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Waheshimiwa Wabunge wanne wafuatao ndiyo watakuwa wasemaji baada yake yeye. Mheshimiwa Mwadini Abass Jecha, Mheshimiwa Freeman Mbowe, Mheshimiwa Lazaro Nyalandu na Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Spika, naomba kukushukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani, kuhusu Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, kwa mwaka wa fedha 2003/2004 kwa mujibu wa kifungu cha 43(5) (b) (c) cha Kanuni za Bunge, Toleo la 2003. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge wote wapya katika Bunge hili tukufu kutokea vyama vyote. Vile vile nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri Jakaya Kikwete na Naibu wake Mheshimiwa Dr. Abdulkader Shareef, kwa ushauri na msaada wao mkubwa ambao umenisaidia sana katika kutayarisha Hotuba hii. Nachukua fursa hii tena kutoa salaam nyingi za pole kwa Waheshimiwa Wabunge, wenzetu waliopatwa na misiba. Naamini sote tunajua kuwa sisi ni wa Mungu na kwake tutarejea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana wananchi wote wa Jimbo la Gando, Pemba, kwa kunichagua kwa kura nyingi kuwa Mbunge wao. Kura zao walizonipa ni changamoto kubwa sana kwangu mimi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naishukuru sana Kambi nzima ya Upinzani Bungeni, chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, kwa kuniona kwamba nafaa kuwa Msemaji Mkuu katika Wizara hii. Naishukuru pia Kambi yote ya Upinzani na Waheshimiwa Wabunge wote kwa ujumla wao kwa ushirikiano wanaonipa kama Naibu Mnadhimu Mkuu wa Kambi ya Upinzani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nafasi ya diplomasia na umuhimu wake kwa taifa. Hakuna Taifa lolote duniani linaloweza kuishi bila ya kushirikiana na Mataifa mengine au vyombo fulani vya Kimataifa, kwa mfano Umoja wa Mataifa na Mashirika yake. Yapo matatizo mengi yanayoweza kuikabili nchi moja, lakini athari zake zinaweza kusambaa katika Mataifa mengine na kwa hali hiyo, ni lazima ufumbuzi wake uwe ni wa Kimataifa. Hakuna Taifa lolote duniani ambalo liko *self-contained* kiuchumi na kisiasa na ndiyo maana duniani kuna biashara ya Kimataifa na siasa za mataifa.

Mheshimiwa Spika, Mataifa yote duniani huingia katika ushirikiano wa kidiplomasia kwa sababu za kimaslahi, hasa yale ya kiuchumi, kiulinzi, kibiashara na kisiasa na si vinginevyo. Urafiki au uadui kati ya Taifa na Taifa daima huongozwa na maslahi ya mataifa husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inaeleweka wazi kabisa katika taaluma nzima ya uhusiano wa Kimataifa kwamba hakuna marafiki wala maadui wa kudumu, kilicho cha kudumu ni maslahi ya Taifa husika tu. Katika diplomasia, baniani mbaya kiatu chake kinaweza kuwa dawa na si mwiko kunywa dawa chungu sana kwa kupoza maradhi. Ni kutokana na ukweli huo, ndiyo maana Jenerali Musharaff wa Pakistan, aliwatupilia mbali Watelaban wa Afghanistan pamoja na kwamba ni yeye aliyeshiriki kuwaweka madarakani na haraka haraka aliwakumbatia *Northern Alliance* na Marekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika diplomasia huwa ni mwiko kushikilia kuti kavu. Ni kile kinacholipa tu kimaslahi ndicho kinachofanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika karne hii na katika mazingira ya sasa hivi ya kiuchumi, kisiasa, kisayansi na kiteknolojia, ni Mataifa yale tu yenye uwezo mkubwa wa ubunifu, hujipenyeza, huchakarika, hujitafutia uongozi katika mambo badala ya kufuata mkondo, kubadilika haraka haraka kila mazingira yanapobadilika, kujenga hoja zenye ushawishi na mvuto kwa Mataifa mengine na hata kukita chini kwa vishindo vinavyotetemesha, ndiyo pekee yatakayopiga hatua kwenda mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hizi ni nyakati za kutomsubiri anayejibakiza nyuma. Hizi si nyakati za kusubiri gari kituoni, bali ni nyakati za kulifuata gari huko huko linakotokea. Hizi ni nyakati za ubabe na vikumbo na kamwe si nyakati za kujikunyata kwenye kona na kusubiri. Hizi kamwe si nyakati za kusubiri kuletewa kwenye kisahani cha dhahabu, ni nyakati za kunyakua. Hizi ni zama za waanzishaji mambo na siyo wafuataji wa mambo au waigaji wa mambo, bali ni zama za kushiriki au kujishirikisha katika mambo mbalimbali. Utandawazi maana yake hasa ni zile sheria za mwituni, kwamba ni wenye mabavu tu na wenye vishindo vizito ndiyo wanaoweza kula na kuishi na hufanya hivyo kwa gharama ya walionyong'onyea au kujikunyata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mazingira haya ya kidunia yanayotawaliwa zaidi na sheria za nguvunguvu na ambazo utekelezaji wake unasimamiwa vikali na Mataifa makubwa ya Magharibi, pamoja na mtandao mzima wa mashirika ya kifedha ya kimataifa kama Mfuko wa Sarafu wa Kimataifa *(IMF)* na Benki ya Dunia, ni lazima Tanzania ijiangalie ndani na nje na ni lazima pia Tanzania ijipime vizuri ubavu wake na ijipange kisawasawa ili kuchukua nafasi yake kama ipo katika mazingira hayo ya kibabe. Kuchelewa kujipenyeza na kujishirikisha kunaalika hatari ya kuenguliwa kabisa na kutupwa nje kabisa ya uwanja wa mchezo, au kusukumizwa pembezoni kabisa mwa uwanja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Jumuiya ya Afrika Mashariki, Kambi ya Upinzani inaamini kuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki inaweza kusaidia maendeleo ya kiuchumi ya Tanzania, hasa kama mambo yafuatayo yatazingatiwa.

Kwanza, Tanzania iinue uwezo wake wa kuzalisha vidhaa za viwandani ndani ya nchi yetu bidhaa hizo pia ni lazima ziwe na ubora wa hali ya juu ili kuumudu ushindani. *(Makofi)*

Pili, Tanzania ijipenyeze kimkakati katika masoko ya wenzetu wa Kenya na Uganda. Ni lazima bidhaa za Tanzania zijazane kwenye maduka ya mitaa ya Nairobi, Kenya na kule Kampala katika Uganda. Kwa sasa maduka ya Tanzania yamejaa bidhaa za Kenya na hata Afrika ya Kusini. Si rahisi kabisa kuziona bidhaa za Tanzania katika maduka ya nchi hizo. *(Makofi)*

Tatu, utulivu mpya wa kisiasa katika nchi ya Kenya kufuatia ushindi wa *NARC*, chini ya Mzee wa Mageuzi, Mheshimiwa Rais Mwai Kibaki wa Kenya, una maana kubwa kwa Tanzania. Kwa miaka mingi tangu Uhuru, Kenya imekuwa ndiye kinara wa uchumi katika Afrika ya Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya mparaganyiko wa kiuchumi katika miaka ya themanini na tisini, sasa Kenya iliyo na demokrasia zaidi, inaanza kujipanga upya ili kukamata upya usukani wa kiuchumi katika Afrika ya Mashariki.

Pamoja na faida za ushirikiano wa kikanda wa kiuchumi, Tanzania ni lazima iwe macho ili uhusiano huo usiwe *one-way traffic*, ambapo bidhaa za Kenya zinajazana katika maduka ya Tanzania, wakati hakuna bidhaa yoyote ya Tanzania katika duka lolote la Kenya. Uzalendo wa kiuchumi *economic nationalism* unazo faida zake na ndiyo maana pamoja na kuwa Mwanachama wa Jumuiya ya Ulaya *(EU),* Uingereza bado inatumia sarafu yake ya *Pound Sterling* badala ya sarafu ya *Euro* kama ilivyo kwa nchi nyingine za jumuiya hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nafasi ya Zanzibar katika Jumuiya ya Afrika Mashariki inahitaji kuwekwa wazi zaidi. Zanzibar nje ya Tanzania Bara, ina maslahi yake muhimu ya kiuchumi na kibiashara ambayo yanaweza kuathirika au kutengemaa zaidi kupitia Jumuiya hiyo. Tangu enzi na enzi, Zanzibar imekuwa kituo kikubwa cha kibiashara katika ukanda huu wa Afrika Mashariki. Ni vizuri Zanzibar ikawa mshirika aliye huru zaidi katika Jumuiya hiyo, baada ya kuwa *sandwiched* ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Yapo maslahi makubwa zaidi ya kiuchumi ambayo ni maalum kwa Zanzibar kama nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uzoefu unaonesha kuwa hili linawezekana kwani Zanzibar ilikuwa Mwanachama wa *East African Community* pamoja na kuwa tayari tulikuwa na Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa moja ya Jumuiya inayotoa ushirikiano mkubwa na misaada kwa wanachama wake ni Jumuiya ya Nchi za Kiislamu *(OIC)* na kwa kuwa ipo ahadi ya nchi yetu kujiunga nayo; Je, ni lini Tanzania itajiunga na Jumuiya hiyo kama ambavyo wenzetu wa Msumbiji na Uganda walivyokwishajiunga? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tanzania imeendelea kuiunga mkono Serikali ya Rais, Robert Gabriel Mugabe, kuhusiana na suala la mgogoro mkubwa wa ardhi na Walowezi wa Kizungu. Hatua hiyo ni nzuri sana. Lakini yaelekea pia Tanzania haikubaliani sana na harakati za wana-mageuzi wa Zimbabwe wakiwa na umoja uitwao *Movement for the Democratic Change*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni lazima Tanzania icheze karata zake vizuri katika suala la Zimbabwe ili isionekane kujitambulisha na wale wote wanaopinga wimbi la demokrasia katika Afrika yawezekana Mugabe na wenzake katika *ZANU-PF* ni makomredi na wapigania uhuru wa zamani tunaowafahamu na ambao Tanzania chini ya Marehemu Rais wa Kwanza Mwalimu Julius Nyerere, aliwasaidia kwa hali na mali. Lakini hayo yote hayatoshi kutufanya eti tuwavumilie na tuwalinde kwa gharama yoyote ile akina Mugabe wanapokwamisha demokrasia.

Mheshimiwa Mandela wa Afrika ya Kusini alisumbuka zaidi kwa mapambano ya kuleta uhuru na haki katika Afrika ya Kusini, lakini kamwe hakuikumbatia Ikulu bali aling'atuka kwa heshima ilhali anatakiwa. Mfano mwingine hai kabisa ni huu wa ndani ya nchi yetu. Tunakumbuka alichokifanya Marehemu Mwalimu Nyerere. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kupigania uhuru msituni hakutoi tiketi kwa Rais Mugabe na wenzake kufia madarakani. Inafahamika duniani kote kwamba Serikali ya Rais huyu inakandamiza upinzani katika Zimbabwe na inatawala kwa ubabe na vishindo. Demokrasia imeendelea kuminywa katika Zimbabwe kwa visingizio vya kutetea ardhi ya wazawa wa Zimbabwe. Ni lazima Tanzania ianze kuitazama upya sera yake kuhusu Zimbabwe ili kuepuka kujiweka karibu na madikteta waliojivisha ngozi za kondoo. Zimbabwe si mali ya Robert Mugabe na makomredi wenzake tu katika *ZANU,* ni mali ya wananchi wote wa Zimbabwe, ikiwa ni pamoja na wale wote walio na mawazo tofauti na yale ya Serikali ya *ZANU.* Hali hii ni somo kubwa kwetu sisi Tanzania kama nchi na Afrika kwa jumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mgogoro wa Zimbabwe ni funzo kubwa kwa Waafrika wote na pia Watanzania wote. Baadhi ya Viongozi wa kiafrika wamekuwa wakilewa mno madaraka na matokeo yake wanachokwa na wananchi na kupoteza mvuto wa kiuongozi. Wanafikia hatua ya kukosa mawazo mapya na namna mpya za kukabiliana na matatizo mapya, na matokeo yake wanaanza kulazimisha kuwepo madarakani kwa ghilba na kunyanyasa wapinzani wao wa kisiasa. Ni aibu kubwa sana hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa ni kuchelewa mno kung'atuka madarakani *(Overstaying)* kwa kisingizio cha kuendelea kuhitajika na wananchi na kumalizia kazi nzuri iliyokwishaanza. Kwa ukweli ni kitendo cha kuwapuuza wananchi kulazimisha mtu mmoja aendelee kuwatawala watu wote kwa muda usioeleweka utakwisha lini kwa kisingizio cha eti kazi nzuri ya kiongozi mhusika. Je, tunauliza, Tanzania, kama Taifa imeshindwa kuishi na kwenda mbele eti kwa sababu Baba wa Taifa alistaafu na baadaye kututangulia mbele ya haki? Si kweli.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana kumaliza muda kwa Mheshimiwa Rais wetu, Benjamin William Mkapa mwaka 2005, hakutakuwa mwisho wa Tanzania na ndiyo maana yeye, Rais Mkapa, kwa kujua Taifa limekomaa kisiasa na lina nguzo imara, hana wasiwasi na kumaliza muda wake. Yeye anafahamu Watanzania wanaofaa kushika nafasi ya Urais baada na badala ya yeye wapo wengi tu, tena bila ya kujali wanatokea Vyama vipi. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kukwepa yale yaliyoisumbua Kenya kabla ya *NARC* na Rais Mwai Kibaki na ili kukwepa matatizo makubwa yanayoikabili Zimbabwe, tusiwashawishi viongozi wetu kuahirisha au kujicheleweshaa kung'atuka madarakani kwa visingizio vilivyofilisika, kama eti kuendeleza kazi nzuri iliyokwishaanza. Kambi ya Upinzani inampongeza sana Rais Benjamin William Mkapa wa Tanzania na Rais Joachim Chisano wa Msumbiji kwa kusema wazi kwamba wao ni lazima wang'atuke baada ya vipindi vyao kwisha. Huu ndiyo utamaduni bora wa kisiasa wa kuigwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inalaani vikali harakati zote za wanaoogopa mabadiliko na maadui wote wa demokrasia na maendeleo, wanaowang'ang'aniza viongozi wenye nia safi na wanaoona mbali kama Rais Benjamin Mkapa na Rais Joachim Chisano, kuendelea kubakia madarakani baada ya muda wao kwisha, kupitia ukunjaji wa Katiba. Tabia hii ni mbaya kama *cancer* katika siasa na demokrasia ya karne hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika miaka ya karibuni, na hasa tangu 1985, Tanzania yetu imetokea kuwa na msimamo ambao umekaa kimchecheto kidogo kila linapokuja suala la uhusiano na Mataifa makubwa ya Magharibi. Ni kweli Tanzania ni Taifa masikini sana likilinganishwa na wakubwa hao. Lakini kinyume na miaka ile ya Utawala wa Marehemu Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, Tanzania imetokea kuwa Taifa la kuchagizwa na kuamrishwa na Mataifa makubwa kila kukicha! Maamuzi mengi ya kiuchumi na kisiasa katika Tanzania ya leo ni chagizo za wakubwa wa Magharibi na wengineo katika *IMF* na Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Spika, pamoja na umasikini uliopo, ni lazima Tanzania kama Taifa huru, liachane na hii tabia mpya ya kupokea amri kila kukicha kutoka Washington na New York. Tukiendeleza sera za kufyata mkia kila wakubwa wakikohoa London na Paris, badala ya kujikaza na kuwa ngangari, viongozi wetu wataendelea kuonekana ni viranja tu, huku Urais wa nchi zetu *technically* ukiwa mikononi mwa Mataifa makubwa. Ni lazima Taifa lirejeshe heshima yake duniani kwa kukataa kuamrishwa ovyo. Leo tungeni Sheria ya Ugaidi na kesho uzeni Benki ile na keshokutwa fungeni kiwanda fulani. Tunaiomba Serikali yetu ichukue misimamo thabiti katika mambo mengine muhimu kama ilivyofanya kwa ujasiri mkubwa katika kupinga vita dhidi ya Iraq. Tunampongeza sana Rais Mkapa na Serikali kwa ujumla kwa msimamo wao juu ya jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa moja ya tatizo kubwa linaloikabili dunia hivi sasa ni Ugaidi, lakini tatizo kubwa zaidi ni kutafsiri huyo gaidi ni nani na ugaidi ni upi. Vitendo vya Kibabe vinavyofanywa na Mataifa makubwa duniani hivi sasa siyo tu vinachochea ugaidi bali pia vyenyewe ni ugaidi mbaya zaidi katika historia ya dunia yetu yaliyofanyika na yanayoendelea kufanyika Iraq na kwingine ni kielelezo halisi cha hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika miaka hii inayohitaji diplomasia ya kiuchumi na kama mwelekeo mkuu wa Sera ya Mambo ya Nchi za Nje, ni vizuri pia Watanzania wakawa na uhakika kwamba Mabalozi wetu huko nje ni watu wa kisasa na wanaoyajua vyema matakwa ya nyakati hizi mpya za utandawazi na kutamba kwa teknolojia ya habari na mawasiliano. Ubalozi sasa hivi ni lazima umaanishe upeo mkubwa wa kuelewa uchumi wa kimataifa, biashara za Kimataifa na uwekezaji, teknolojia ya habari, sheria za Kimataifa na Mikataba mbalimbali, diplomasia ya kisasa na mambo mengi ya aina hiyo. Je, Serikali inao uhakika kwamba Mabalozi wetu wote, popote walipo duniani ni watu wenye fikra mpya zinazotakiwa na dunia hiyo tuliyoizungumza? Tuachane mara moja na Mabalozi wote ambao ni *liability* kwa Taifa kwa sababu wameachwa na wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wapo Mabalozi ambao wamekwishakaa mno katika Ubalozi, ukiondoa kukaa muda mrefu katika utumishi wa umma. Ubalozi ni kufanya kazi kwa nguvu na kwa saa nyingi. Ubalozini si mahali pa watu kupumzikia na kuzeeka taratibu. Mabalozi walio *overstay* na hata kujichokea kiumri warejeshwe nyumbani kwa heshima, wapewe viinua mgongo vyao na waendelee kufaidi pensheni zao. Serikali itafute Mabalozi ambao wana nguvu za afya na kufikiri na pia watu ambao ni *aggressive*, kwani ni watu wa aina hiyo tu ndiyo walio na uwezo wa kuifanya nchi ifaidi chini ya diplomasia ya kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yeyote anayeujua uwezo wa Bwana Juma Volter Mwapachu, hapati wasiwasi akisikia mtu huyo ni Balozi wa Tanzania katika nchi fulani. Mtu huyo kwa usomi wake, uzoefu wake, usasa wake na hata umri wake, anafanana kabisa na dhana mpya ya diplomasia ya kiuchumi. Swali je, Mabalozi wetu wote wana sifa kama zake? Tusieleweke kumpigia debe Bwana Juma Mwapachu, bali tunajaribu kujenga hoja ya mfano wa Balozi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaunga mkono harakati za Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa na viongozi wengine katika Afrika za kuwapatanisha wenzetu hao wa Burundi, lakini bila ya kuwadekeza mno. Kama karoti inashindwa kuwafanya wapatane, basi si vibaya kujaribu shubiri! Ni lazima Warundi waelewe kwamba mzozo wao usioisha ni mzigo mkubwa kwa majirani. Wakimbizi wanaojazana Tanzania huleta matatizo makubwa kama kuharibu mazingira na kuongezeka sana kwa vitendo vya uhalifu.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inampongeza sana Rais Joseph Kabila wa *DRC* kwa kukubali kwa roho nyeupe kushirikiana na Wapinzani wakubwa kama akina Pierre Bemba, kuendesha Serikali kwa pamoja kwa manufaa ya raia wote wa nchi yao. Ushujaa wa Rais Kabila umeruhusu kuanza kwa kipindi cha mpito kuelekea katika Uchaguzi Mkuu. Ni uchaguzi huo ndio utaamua watu wa *DRC* wanataka nani awaongoze.

Katika *DRC,* diplomasia imechukua mkondo wake na raia wa nchi hiyo wanaanza kuonja amani. Tunatoa mwito kwa baadhi ya majirani wa nchi hiyo, kuacha mara moja chokochoko zao dhidi ya *DRC* na kuacha kuumezea mate utajiri mkubwa wa madini muhimu na mazao ya misitu minene ya ki-ikweta unaopatikana katika nchi hiyo kwa wingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani imeendelea kufurahishwa na namna demokrasia inavyozidi kushamiri katika Nigeria, hasa kufuatia kufanikiwa kwa Uchaguzi Mkuu wa hivi karibuni. Zile zama za Wanajeshi kuendesha maisha ya kisiasa katika nchi hiyo zinaonekana kutoweka polepole, tena kwa kiuhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kutia moyo kwamba sasa amani imejikita katika Angola baada ya kuacha malaki ya watoto yatima, walemavu, wajane, na kadhalika, katika Angola ya sasa, *UNITA* ya Hayati Jonas Savimbi inashirikiana vema kabisa na *MPLA* ya Eduardo José dos Santos kudumisha amani na kuwaletea maendeleo watu wa Angola. Mwafaka kati ya *UNITA* na *MPLA* ni ushindi mkubwa kwa watu wa Angola. Ni ushindi wa amani na ni ushindi wa maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali ya mambo si shwari kabisa katika nchi zilizo majirani za Liberia na Sierra Leone kule Afrika ya Magharibi. Nchi hizo zina vita vya wenyewe kwa wenyewe kwa miaka mingi

sasa. Raia wameendelea kuuawa, kupata vilema na kurudi nyuma kimaendeleo. Jumuiya ya kimataifa inashauriwa kulishikia bango suala zima la mizozo katika nchi hizo mbili kwa lengo la kuleta amani ya kudumu. Umoja mpya wa *Africa Union* ni lazima uchukue hatua zaidi kwa kushirikiana na Umoja wa Mataifa *(UN)* ili kuleta amani katika eneo hilo la Afrika. Amani ndio hazina pekee muhimu ya Taifa lolote duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maelewano ya kisiasa kati ya CCM na *CUF* kupitia muafaka wa mwaka 2001 yameipigia debe Tanzania duniani kote kama nchi ya watu wastaarabu na waliokomaa kisiasa na wenye uwezo wa kusuluhisha migogoro yao wao wenyewe. Serikali yetu ya Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa pamoja na SMZ zote zina heshima kubwa duniani kwa sababu ya muafaka huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Muafaka huo pia umemaanisha kuanza kumiminika kwa misaada ya Wahisani mbalimbali, sio tu kwa Serikali ya Muungano, bali hata kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliyokuwa imesusiwa karibu na Wahisani wote wa Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Muafaka huo unaimarisha jina la Tanzania nje ya nchi yetu na unaongeza sana imani ya Wawekezaji kwa Tanzania. Muafaka huo pia umevutia sana Wafadhili wa Kimataifa na kwa hali hiyo kuchangia sana katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii ya Watanzania. Muafaka huo ni hazina muhimu ya Kitaifa na yeyote anayejaribu kuuhujumu kwa namna yoyote ile, ni adui mkubwa wa Watanzania na aogopwe kama Ukimwi. Muafaka ni lulu ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais Amani Abeid Karume, kwa hatua alizochukua za utekelezaji wa Muafaka. Kama Burundi na *DRC* wameweza kufanya mambo makubwa kujiletea amani, hivi Rais wetu wa Zanzibar na Mwana-Mapinduzi shupavu, Mheshimiwa Karume anashindwa nini kuteua hao Wawakilishi wawili sasa hivi, ilhali anajua ni takwa muhimu la Muafaka wetu? Kama nia ni njema tu ya kujenga maelewano mema, kinachogomba ni nini? Kwa nini jambo jema lingoje kesho?

Nina hakika Mheshimiwa Rais Amani Abeid Karume, anao uungwana wa kisiasa wa kuutekeleza Muafaka wote kwa sababu yeye ni Mzalendo wa Zanzibar, ni mzalendo wa Tanzania na ni sehemu muhimu ya huo Muafaka wenyewe. Sisi Kambi ya Upinzani tuna hakika kabisa kuwa utekelezaji mzuri wa Muafaka utakaofanywa na Mheshimiwa Karume, sio tu utamjengea mwenyewe heshima lakini na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin Mkapa, ambaye alichukua ahadi kubwa ya kuusimamia Muafaka huu mbele ya macho ya dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kugharamia uimarishaji wa Chuo hiki kwa kusaidia ukarabati wa majengo, uongezaji wa majengo mengine, vifaa mbalimbali na kadhalika. Naupongeza pia Uongozi wa Chuo hicho kwa kupanua shughuli za Chuo ikiwa ni pamoja na uanzishaji wa kozi mpya za aina mbalimbali. Hata hivyo bado Chuo hicho kinayo nafasi ya kujiimarisha zaidi na kuwa moja kati ya Taasisi zinazoongoza katika Afrika, hasa katika eneo la diplomasia na uhusiano wa Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Chuo hiki kijitwishe haraka jukumu la kuichanganua Mikataba mbalimbali ambayo huridhiwa na Tanzania. Mikataba hiyo iwekwe katika lugha rahisi kabisa itakayomfanya mwananchi wa kawaida, mwenye Elimu ya Msingi tu, aielewe vizuri. Chuo hicho pia kinalo jukumu la kufafanua kwa manufaa ya wananchi, maamuzi na masuala mbalimbali ya Kimataifa ambayo yana maslahi au athari fulani kwa Watanzania. Chuo kijitahidi kueleweka kwa mwananchi wa kawaida na kijitahidi kuthibitisha umuhimu wake kwa kila mlipa kodi wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni lazima Tanzania iendelee kuwa sehemu muhimu ya Jumuiya ya Kimataifa. Ni lazima ishiriki katika uhusiano wa Kimataifa na ikwepe kuwa mtazamaji au msindikizaji. Ni muhimu Tanzania yetu ikwepe kuenguliwa katika siasa za Kimataifa kwa kufanya maamuzi sahihi, mahali sahihi na kwa wakati sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii si dunia ya kubweteka, ni dunia ya kupambana vikali katika uwanja wa uchumi na ni dunia ya kila Taifa makini kuhakikisha linaonekana lipo na linashiriki katika michezo na siyo

kuwatazama na kuwashangilia wengine wakicheza. Hii ni dunia ya kuchangamka na hata kuwapiga vikumbo wengine ili uende mbele kama Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa kazi muhimu za kimaendeleo za Wizara ya Mambo ya Nje unategemea sana kupatiwa hilo fungu lenyewe la maendeleo na kwa bahati mbaya sana Wizara hii haikupewa fungu hilo la maendeleo katika bajeti hii. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ilitizame upya jambo hili kwa haraka sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru tena kwa mara ya pili kwa kunipa fursa hii, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaanza mjadala wa jumla. Mheshimiwa Mwadini Abass Jecha, mfungua dimba. Yuko wapi? Amekwenda Mtera! Mheshimiwa Freeman Mbowe, yuko wapi mbona hanyanyuki? *(Kicheko)*

**WABUNGE FULANI:** Yupo!! *(Kicheko)*

**SPIKA:** Ooh, sawasawa. *(Kicheko)*

**MHE. MWADINI ABASS JECHA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii nami kuchangia katika hotuba ya Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Aidha, pia niungane na wenzangu kumshukuru Mheshimiwa Waziri Jakaya Kikwete, pamoja na Naibu wake na Watendaji wote wa Wizara kwa uandaaji wa hotuba iliyo nzuri, iliyojengeka vizuri na ambayo inaelekea katika kuleta Mapinduzi katika diplomasia ya kilimwengu na ya dunia kwa ujumla. *(Makofi)*

Aidha, nichukue nafasi hii kuipongeza Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje, kwa hotuba yake nzuri ambayo nia yake kubwa ni kuiboresha hotuba ya Mheshimiwa Waziri katika kutekeleza wajibu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimpongeze pia Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa hotuba yake nzuri yenye kusisimua na ambayo kama ile ya Kamati, nia yake kubwa ni kuiboresha hotuba ya Mheshimiwa Waziri ili afanikishe shughuli zake za kiutendaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ya Mambo ya Nchi za Nje ni miongoni mwa Wizara ambazo ni za Muungano, Muungano uliofanyika kutokana na nchi mbili huru, nchi ya Zanzibar na Tanganyika na kwa muda mrefu tangu Muungano huu umeanza, basi siasa zetu zimejikita zaidi nchi za nje hasa katika shughuli za ukombozi wa Afrika na katika shughuli za kupiga vita ubaguzi wa rangi. Naweza kusema kwamba shughuli za Kibalozi za miaka ya nyuma hazikujikita zaidi katika shughuli za kiuchumi na kwa hiyo maendeleo ya kiuchumi katika nchi hii hayakutegemea kabisa au kwa kiasi kidogo tu imetegemea shughuli za Kibalozi nchi za nje.

Kutokana na hali hiyo hata uteuzi wenyewe wa hao Mabalozi wa nchi za nje ulikuwa zaidi unazingatia mahusiano ya kisiasa kuliko ya kiuchumi kwa nchi zile ambazo tulikuwa tunapeleka Mabalozi wetu. Tunashukuru kwa mafanikio yaliyopatikana hasa katika ukombozi wa Afrika na pia katika kutokomeza ubaguzi wa rangi katika Afrika. Lazima tukiri sasa kwamba dunia inabadilika, siasa imekuwa ni uchumi na uchumi umekuwa ni biashara.

Sasa kutokana na muktadha huo na hata utaratibu wetu wa kuteua Mabalozi wetu nchi za nje, basi uzingatie dhana hii kwamba siasa ni uchumi na uchumi ni biashara. Kwa maana hiyo hata Mabalozi wetu walioko nchi za nje sasa wabadiliike kujielekeza zaidi katika kukuza uchumi wa Tanzania na kiasi kidogo labda katika shughuli za kisiasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi kama ya Kenya ni nchi ambayo imefanikiwa sana kiuchumi kwa kutumia Mabalozi wake wa nchi za nje. Sasa ili nasi tufanikiwe ninaishauri Serikali sasa tubadilishe utaratibu wa kuteua Mabalozi wetu wa nchi za nje. Tuandae sifa maalum iwe labda kama ni lugha, elimu, uzoefu na mambo mengineyo na baadaye pafanyike usaili ili tuibue wanadiplomasia walio mahiri.

**MBUNGE FULANI:** Na umri.

**MHE. MWADINI ABASS JECHA:** Na umri nao pia nimekumbushwa, ili tuwe na wanadipolomasia walio mahiri ambao wataiwezesha nchi yetu kuikomboa kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama tunavyojua kwamba shughuli ya Kibalozi ni utumishi wa kiserikali. Si shughuli ya kisiasa. Kwa maana hiyo, kwa yeyote yule atakayekuwa na sifa zitakazopangwa ambaye atakubalika kwa mujibu wa vigezo vilivyowekwa, basi awe na nafasi ya kuwa Balozi wa nchi hii kwa nchi za nje bila kuzingatia mtu itikadi yake au hali yake ilivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata huu Ubalozi wenyewe nao unatakiwa uwe na muda maalum. Kama ambavyo Msemaji wa Upinzani alivyosema hapa kwamba, tusiwaachie watu wanazeekea kule ikawa ndio ni mahali pa kupumzikia kusubiri mwisho wa kufikia maisha yao. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kidogo nizungumzie kuhusu *NEPAD,* wanaita *New Partnership Africans Development.* Juzi, nilikuwa nasikiliza mahojiano ambayo Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, alikuwa anahojiwa na Waandishi wa Habari na alikuwa anazungumzia maendeleo yaliyopatikana kupitia hii *NEPAD.* Amezungumza mengi, lakini katika yale aliyozungumza, kwa bahati mbaya pengine labda hakuwahi kusema au pengine pia yalinipita tu, lakini sikusikia hata moja ambalo limeleta maendeleo katika upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano kule Zanzibar. Sasa sijui Zanzibar haihusiki, Zanzibar haina nafasi au kuna nini mpaka hii miradi ambayo inazungumziwa katika hii *NEPAD* ikawa Zanzibar haijafaidika lolote. Katika hili naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anapofanya *winding-up* labda na mimi anieleze kuna nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *East African Community*, kuna miradi mingi ambayo inatekelezwa sasa hivi, miradi ya njia, Bandari, Viwanja vya Ndege na tumekuwa tunaelezwa mara kwa mara ndani ya Bunge hili kwamba kuna baadhi ya njia za Tanzania ambazo zimeteuliwa kutengenezwa au kujengwa kwa mantarafu ya kukuza mawasiliano baina ya nchi hizi tatu. Zanzibar nayo ina Bandari na Zanzibar ina viwanja vya ndege. Kuna Bandari nne nazo zimetolewa rasmi kuwa ni Bandari za Kitaifa, Bandari ya Zanzibar, Bandari ya Mkokotoni, Bandari ya Mkoani na Bandari ya Wete.

Hizi ni miongoni mwa Bandari ambazo zilikuwa zinashirikishwa katika hili suala la biashara ya *East Africa* na Afrika kwa jumla ikikumbukwa nyuma kwamba Zanzibar ilikuwa ni kitovu kikuu cha biashara. Kwa sababu bandari hizi zilikuwa zinatumika ipasavyo. Sasa mimi nilidhani labda katika miradi hii ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, basi Bandari hizi nazo zingeimarishwa na zile ambazo zinajengwa upya zijengwe upya ili kuimarisha shughuli za biashara ndani ya nchi hizi tatu. *(Makofi)*

Kuna Viwanja vya Ndege. Zanzibar kuna uwanja ule wa Zanzibar pale na Pemba kuna Karume *Airport*. Uwanja huu umepewa jina la Muasisi wa nchi, Mwanamapinduzi aliye mahiri, lakini kwa bahati mbaya uwanja huu umedharauliwa, umetupwa, hauulizwi; sijui kwa nini? Tunadharau jina mpaka la ule uwanja ambao ni jina la Muasisi wa nchi ile, hii ni hatari kubwa. Sasa ili kukuza hii biashara baina ya Tanzania na nchi za Uganda na Kenya ni pamoja pia na kukuza biashara ndani ya ile Pemba yenyewe. Uwanja wa Zanzibar tunashukuru kwamba unafanyiwa matengenezo mara kwa mara na hivi karibuni nasikia amejitokeza Mfadhili kuupanua ule uwanja. Lakini sisikii kama kuna mtu anayeufadhili uwanja wa Karume kuupanua hata kuutengeneza. Sasa nadhani Mheshimiwa Waziri ajaribu kuliona hili katika haya mashirikiano ya *East African Community* kukuza biashara ndani ya nchi hizi, basi na uwanja huu wa Pemba unajengwa upya ili kukuza biashara katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mimi kidogo nigusie suala la *OIC.* Miaka ya nyuma ile ya themanini, hali ya ulimwengu ilibadilika, biashara zikaporomoka na uchumi wa Afrika nao ulitetereka kwa sababu Afrika uchumi wake hasa wakati huo ulikuwa unategemea zaidi mazao ya kilimo. Mazao ya kilimo yaliathirika kwanza

kutokana na ukame; lakini la pili na bei ndogo ya mazao ambayo tulikuwa tunasafirisha kupeleka nchi za nje. Sasa kwa sababu kilimo ni uti wa mgogo wa nchi yetu, nchi ya Afrika ikaanguka kiuchumi. Kila nchi iliandaa mipango yake mahususi ya kujaribu kujikwamua kiuchumi. Hapa Tanzania kwa sababu ni miongoni mwa nchi za Afrika nayo pia ikaandaa utaratibu ambao ungewawezesha kujikwamua kiuchumi na kuleta maendeleo ya wananchi wake.

Kwa upande wa Zanzibar nako kule, Serikali ilichukua hatua ya kuimarisha viwanda vidogo vidogo, ikatafuta wawekezaji, ikafungua milango ya kibiashara na ikawa inaomba misaada, karadha, mikopo na kadhalika. Katika kutekeleza hayo, Serikali ya Zanzibar iliamua kujiunga na ile *OIC* kwa nia moja tu nayo ni kutafuta misaada ya kimaendeleo. Sote tunakumbuka yaliyotokea Bungeni. Dhahama ilikuwa kubwa, vibiriti vikatingishwa, matokeo yake kuna kibiriti kikaonekana hakina njiti na hatimaye Zanzibar ikalazimika kujitoa katika *OIC. (Kicheko/Makofi)*

Lakini tuliahidiwa kwamba Tanzania kama Jamhuri ya Muungano itachukua hatua ya kujiunga na hiyo *OIC* ili kuiruhusu Zanzibar kuweza kupata misaada katika Shirika hili. Sasa sijui kwa nini mpaka leo tumekuwa hatuelezwi hatua hii imefikia wapi au sijui kuna nini, lakini mimi nadhani ile kuifanya Zanzibar itoke katika *OIC* tuliangalia zaidi upande wa kisiasa na yale mazoea tuliyokuwanayo zamani ya diplomasia ya kisiasa kwa nchi za nje, lakini hatukuangalia zaidi masuala ya kiuchumi. Suala la kukosa misaada Zanzibar ni hatari tukijua wazi kwamba Zanzibar ni nchi ambayo kilimo chake bado hakijakua vizuri, tunategemea zao moja tu la biashara na kwa maana hiyo uchumi wake unakuwa ni mdogo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi naishauri Serikali kwamba ichukue kila juhudi kuona kwamba ile azma ya Serikali ya Mapinduzi kujiunga na hili Shirika inatimia ili nayo Zanzibar iweze kupata misaada kutoka nchi za nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache, nimalizie kitu kidogo cha mwisho. Ningemwomba Mheshimiwa Waziri, atueleze hii nafasi ya Zanzibar katika *East African Community,* naona kama tunawekwa wekwa nyuma sana. Hatujioni kama sisi tunashirikishwa ipasavyo, siyo kushiriki kwamba kwenda katika vikao, lakini kushirikisha nchi katika kupata maendeleo, ndiyo ambalo naliulizia hapa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hotuba ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na Wataalam wote wa Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje, kwa kuendelea kuiweka Tanzania katika picha nzuri inayokubalika katika jamii ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, leo mchango wangu katika hotuba hii ya Bajeti nitajielekeza kwenye suala moja ambalo ni Sera mpya ya Mambo ya Nchi za Nje. Napenda nichukue fursa hii vile vile kwa mara nyingine tena, kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Wataalam wote wa Wizara yake, kwa kutayarisha Sera nzuri na nafikiri Sera hii kwa kweli pamoja na kwamba vitabu hivi vya Sera tumepata sasa hivi, nimeweza kuipitia kwa haraka haraka na ninapenda niwapongeze sana. Mimi binafsi na ninaamini wenzangu wengi ambao wanaitakia nchi yetu mema, hawatakuwa na tatizo katika kuwapongeza wenzetu kwa Sera nzuri sana ambayo kweli inatoa mwelekeo sahihi kwa siasa zetu za nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo kwa Mheshimiwa Waziri, Sera nzuri ni kitu kimoja lakini utekelezaji wa Sera ni suala lingine. Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake alibainisha kwamba, unaandaliwa mwongozo na mkakati wa utekelezaji wa Sera. Nafikiri hili ni suala la msingi sana.

Mheshimiwa Spika, ningependa nitahadharishe kwamba, utekelezaji wa mpango wowote wa Sera, nina imani kabisa kabisa kwamba, ni mpango wa maendeleo. Kwenye upande wa pili, Wizara hii ambayo ni Wizara nyeti ambayo ni kiungo muhimu kati ya nchi yetu ya Tanzania na jamii ya Kimataifa, hasa

tukizungumzia kipindi hiki ambacho ulimwengu umekuwa kijiji, yaani umekuwa *global village* na Sera za Uchumi na Biashara ndiyo Sera ambazo zina-*determine direction* ya uchumi wa nchi yeyote ile.

Wizara hii kwa kweli haijapewa meno ya utekelezaji wa Sera yake mpya. Hapa napata wasiwasi kidogo kama kweli nia njema ya kuandaa Sera nzuri sana ya nje itatekelezwa vipi kama Wizara hii haikuweza kupatiwa fungu hata moja la maendeleo. *(Makofi)*

Wizara nzima inapokuwa haipati fungu lolote la maendeleo, ina maana mikakati yote ya utekelezaji wa Sera mpya pengine huenda ikabidi kusubiri mwaka ujao wa fedha ili ianze kutekelezwa. Hili mimi kidogo linanitatiza sana na ningeomba Serikali, kwa makusudi kabisa ifikirie utaratibu wowote ambao utaiwezesha Wizara hii kupata fedha za dharura kwa shughuli zake za maendeleo na katika suala hili la maendeleo likiwemo utekelezaji wa sera hii.

Mheshimiwa Spika, Sera mpya ya Mambo ya Nje imezungumzia kwa kina sana suala la *Economic Diplomacy*. Nafikiri ni suala la msingi ambalo sasa lazima tuambiane ukweli tusaidiane kwamba, pamoja na Sera nzuri je, Ofisi zetu za Ubalozi, Wanadiplomasia wetu katika Ofisi zetu za Ubalozi, kweli wana uwezo na utashi wa kusimamia Sera Mpya ya Mambo ya Nje. Hili ndiyo suala la msingi sana ambalo lazima sasa tuweze kuli-*address, other wise* hii Sera itabaki kwenye makabati lakini utekelezaji wake utakuwa wa mashaka makubwa.

Mheshimiwa Spika, labda kwa kulizungumzia zaidi suala la *Economic Diplomacy,* ningependa kulielekeza kwenye upande wa biashara na hasa kwenye upande wa masuala ya *Balance of Payment,* yaani nchi yetu inaagiza kiasi gani kutoka nje na nchi yetu inauza kiasi gani katika nchi za nje. Kwa makusudi kabisa katika kulizungumzia hili, ningependa ninukuu mifano michache kutoka kwenye *Economic Bulletin* ambayo inatolewa na Benki Kuu ya Tanzania, hasa kwa kulenga zile nchi ambazo nchi yetu ina Ofisi za Ubalozi ndani yake na nitatoa mifano michache tu kuonyesha jinsi ambavyo kwa bahati mbaya sana kumekuwa kuna tofauti kubwa sana ya biashara ambayo inafanyika baina ya nchi na nchi, hasa mali tunazoagiza kutoka katika nchi hizi na mali ambazo tunauza katika nchi hizi.

Mheshimiwa Spika, katika kutoa mifano hii, nitaweza kubainisha kwa urahisi kabisa kwamba, huenda katika nchi hii Ubalozi unafanya kazi ya msingi ama Ubalozi haufanyi kazi ya kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ukweli kwamba, Balozi ana kazi nyingi zikiwemo za masuala ya kisiasa na uhusiano wa kisiasa, kijamii na hata kiutamaduni, suala la uchumi ni suala ambalo limepewa *priority* kubwa sana katika *Foreign Policy* yetu. Lakini hili limejitokeza kabisa kabisa kwamba, *objectives* yaani malengo ya Sera Mpya ya Uchumi, ambayo imeainisha malengo matano katika malengo yote matano yote yamezungumzia kwa kina kabisa suala la uchumi.

Mheshimiwa Spika, kwa faida ya wale ambao bado hawajapata nafasi ya kupitia Sera Mpya ya Mambo ya Nje, ukurasa wa 12 kifungu cha 26, naomba ninukuu: "The objectives of the new United Republic of Tanzania Foreign Policy shall be:-

(a) To promote and protect United Republic of Tanzania political, economic, social and cultural interest through active and sustainable economic policy;

(b) To ensure that, United Republic of Tanzania relations with other nations and international entities are also driven inline with the economic interests;

(c) To build a self sustain economic, preservation of national peace and security as well as supporting regional and international endeavor for the creation of a better and peaceful world;

(d) To accelerate the political and social economic integration of the region; and

(e) To create the necessary condition which shall enable United Republic of Tanzania to participate effectively in the regional and global economies and international negotiation".

Mheshimiwa Spika, hayo ndiyo malengo yetu ya *Foreign Policy.* Malengo ambayo yamelenga na yameelekeza kabisa kabisa sasa mtazamo wetu katika *Foreign Policy* unaangalia masuala ya kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ina Ubalozi nchini Nigeria. Pamoja na mahusiano mazuri sana ambayo tumekuwanayo na wenzetu wa Nigeria kwa muda mrefu, tumekuwa na uhusiano wa kisiasa na Nigeria. Hatujawa na uhusiano wa kiuchumi na Nigeria, wala hatujawa na uhusiano wa kiutamaduni na Nigeria.

Mheshimiwa Spika, nalizungumza hili kwa sababu Nigeria ni uchumi muhimu katika Afrika. Lakini kwa mujibu wa takwimu ya nchi yetu na takwimu zinazotolewa na *Bank of Tanzania,* hatujawahi kufanya biashara yoyote na Nigeria na bado tuna Ubalozi ndani ya Nigeria. Tatizo ni nini? Ni chaguo letu la kuwa na uhusiano na Nigeria ama tatizo ni watumishi walioko katika Ofisi yetu ya Ubalozi Nigeria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kwamba, kwa mujibu wa takwimu za Benki ya Tanzania kwa miaka 20 iliyopita, hatuna rekodi ya ku-*export* mazao ama chochote angalau kwa dola moja kwenda Nigeria. Wala hatujawahi ku-*import* chochote kutoka Nigeria. Katika hali kama hii kidogo inanitatiza, ni nini kweli *priority* yetu ya kuacha Ubalozi wa Nigeria tukafunga Ubalozi wa *The Hague*, Uholanzi, Ubalozi ambao ulikuwa unaipatia nchi hii zaidi ya dola milioni 150 kila mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili nitaomba Mheshimiwa Waziri, ajaribu kutu-*enlighten* kidogo kuhusu nini *priority* yetu katika nchi ambazo tunakuwa tuna uhusiano nao wa Kibalozi.

Mheshimiwa Spika, kwa haraka haraka nizungumzie nchi pekee ambayo tumekuwa tuna uhusiano wa Kibalozi ambao inaonekana kuna uwiano wa biashara tunaoagiza na kuuza kwao ni India, ambayo katika mwaka 2001 tumeweza kuuza India bidhaa za thamani ya shilingi bilioni 72 na wakati huo huo tuliweza kuagiza kutoka India mali za bilioni 76. Unaweza kuona hapa kwamba, mahusiano ya kibiashara kwa kweli yalikuwa mazuri na hapa pengine hata Ubalozi ulihusika.

Tukirudi nchi ya France ambayo tumesikia sifa za Mheshimiwa Balozi Juma Mwapachu, ukiangalia takwimu za miaka mitatu iliyopita, Ufaransa ni nchi ambayo tumeuza mali nyingi sana katika mwaka wa fedha wa 2001 na kumekuwa na ongezeko kubwa sana kati ya mwaka 2000 mpaka 2001, ambapo fedha ya Kitanzania shilingi milioni 29 kwenda milioni 119, kumekuwa na ongezeko la zaidi ya asilimia 400 na kwa kweli tungeomba tujue ni kwa nini kumekuwa na ongezeko kubwa kiasi hiki, *whether* kweli ni *performance* ya Balozi au Ofisi ya Ubalozi ama labda kulikuwa kuna kitu ambacho kina siri katika hili.

Mheshimiwa Spika, nikija kwenye mahusiano ya kibiashara na nchi ya Kenya, wenzetu wa Kenya tunauza kwao shilingi bilioni 33 kwa mwaka, lakini wao wanatuuzia mali ya shilingi bilioni 84. Sasa ambayo ni mbaya zaidi ni uhusiano wetu wa kibiashara na *Republic of South Africa,* wenzetu wa *South Africa* tumeweza kuuza kwao, kwa takwimu za mwisho zilizotoka Benki Kuu tumeweza kuuza kwao mali ya pesa ya Kitanzania shilingi bilioni 7.6 wakati tumeagiza kwao shilingi bilioni 178. Hapa kwa kweli *balance of payment* haiwezi ikapatikana na ni masuala ambayo sasa Wizara yetu ya Mambo ya Nchi za Nje kama Wizara inayo-*coordinate* masuala yote yanayohusu nchi yetu na nchi za nje ikawa ina mkakati maalum wa kufanya *analysis* ya hizi *import and export* za nchi yetu na hizi nchi mbalimbali katika kuainisha mahusiano na utekelezaji wa *Foreign Policy.*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kwa haraka haraka kwa sababu muda unanipiga chenga, nini hasa tunashauri kifanyike katika utekelezaji wa Sera Mpya ya Mambo ya Nchi za Nje.

Mheshimiwa Spika, Balozi zetu zina wastani wa watu wanne katika kila Ubalozi, *staff* ambao wanatoka Tanzania. Ni kiwango kidogo mno kuweza kusimamia maslahi ya nchi katika nchi ile, tunafanya hivyo kwa sababu ya kupunguza gharama za uendeshaji wa Ofisi zetu za Ubalozi na ufinyu wa Bajeti. Lakini tuna ulazima wa kujua kwamba, kama tunataka kufanikiwa katika biashara za Kimataifa na kama tunataka kushiriki kikamilifu katika mkakati mzima ama mpango mzima au kuingia katika mfumo wa *globalization*, ni lazima sasa kama nchi, tukubali kabisa kuwekeza katika Wizara yetu ya Mambo ya Nchi

za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na sasa tuwekeze kwa dhati kabisa katika Ofisi zetu za Ubalozi na Ofisi hizi ziwe na watu ambao ni *committed and competent. (Makofi)*

Tunataka katika mkakati wa utekelezaji wa Sera wa Mambo ya Nchi za Nje. Mheshimiwa Waziri na Timu yake na Serikali kwa ujumla, ifanye *total overhaul* ya Ofisi zetu za Ubalozi kama walivyozungumza wenzangu. Ofisi hizi zipewe watu ambao ni *competent*, watu ambao wana uzoefu wa kiuchumi. Tunahitaji wachumi katika Ofisi zetu za Ubalozi.

Tunahitaji watu ambao wana uzoefu wa masuala ya biashara za Kitaifa na za Kimataifa na kwa kweli sasa ule muda wa kupeana nafasi katika Ubalozi kama sehemu ya shukrani ama ya kupumzikia, ni vema sasa tukaisimamisha haraka sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Balozi zetu za *South Africa, Washington DC,* New York, London, Beijing na Japan zinahitaji kuimarishwa. Hatuwezi tukawa na *short cuts* zaidi ya kuimarisha Balozi zetu hizi. Lakini vile vile ni lazima kama nchi, tuangalie *world economic trends* kwamba, ni nini kinaendelea katika uchumi wa Kimataifa. Hatuwezi tukapuuza *presence* yetu katika nchi za *South East Asia*, kama Korea, Thailand, Singapore, Vietnam na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, hizi ni nchi ambazo tunaweza tukafanya nazo biashara kwa urahisi zaidi kuliko hata nchi za Uingereza, nchi za Ulaya na nchi za Marekani. Lakini tumekuwa wazito sana kuingia katika nchi za *South East Asia,* kwa sababu labda tunaogopa hatutaki kufanya *investment* katika nchi hizi. Wenzetu wa Kenya ambao wana mfano mkubwa sana wanafanya kazi kubwa sana katika Ofisi zao za Ubalozi katika nchi hizi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuongea hayo kwa kweli sina sababu hata moja ya kutokuunga mkono hoja na namtakia Mheshimiwa Waziri kila la kheri. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Spika na mimi naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi niungane na wenzangu katika kuchangia hoja hii ya Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Nachukua nafasi hii kumpongeza sana Waziri, Mheshimiwa Jakaya Kikwete, kwa hotuba yake nzuri. Nachukua nafasi hii kwa moyo wa dhati, kumpongeza Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote katika Wizara hii ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. *(Makofi)*

Naamini baada ya kuona hii Sera Mpya ya Mambo ya Nje, hatimaye mwelekeo wetu katika masuala ya nchi za kigeni utaendelea kuboreshwa zaidi kwa sababu mkakati huu ambao Wizara imetuandalia ni mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo tulilonalo duniani ni kwamba, kuna kasheshe nyingi sana na kwa sababu asilimia 20 ya wanadamu wote duniani ndiyo ambao wanakula na wanamiliki mali asilimia 80 ya utajiri uliopo duniani na kwa sababu *resources* za dunia sasa badala ya kupambana na umaskini na magonjwa zimeelekezwa kupambana na matatizo mapya kama ugaidi wa Kimataifa. Kwa hiyo, *shift* ya *focus* ya misaada ya Kimataifa inabadilika kwa sababu ya mambo ya wakati huu tulio nao.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu tatizo tulilonalo ambalo ni vita na wakati mwingine ni kubwa kuliko vita vya bunduki ni tatizo la UKIMWI, ambalo sasa dunia inapambana nayo. Kwa sababu Umoja wa Mataifa ni chombo ambacho kinamilikiwa na wakubwa wachache na wale ndiyo watu ambao wamekuwa wakiamua tufanye nini kwa wakati gani na wanyonge mara zote wamekuwa wa mwisho katika Umoja wa Mataifa.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba, Tanzania sambamba na nchi zingine katika Jumuiya za Kimataifa, ndani ya Umoja wa Mataifa tungeweza kutumia neno *numbers,* kwa sababu maamuzi kama kuna tatizo Somalia halipewi uzito kama tatizo la Bosnia, kama tatizo la watu la maangamizi ya Rwanda halipewi umuhimu kama tatizo lingine lingetokea Ulaya. Sasa linakuja suala la ushindani wa *resources* ndogo duniani, namna gani sisi tunaweza tukanyang'anyana na wengine kwa sababu mahitaji ni mengi *resources* ni kidogo na wakubwa wanavi-*shift* kutokana na mwelekeo wa dunia unavyotokea.

Naomba nizungumzie mambo mawili, Wahenga walisema "kupanga ni chagua". Itakuwa ni kosa kwa nchi yoyote duniani kuamua kuipa Wizara ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa pesa kidogo na hasa pesa ambazo Wizara hii ingeweza kutumia kwa ajili ya *research and development* wajue katika mikakati ya mabadiliko waongeze nguvu wapi kuinusuru nchi yetu. Asilimia 45 ya pesa ambazo tunazihitaji nchi hii zinatoka nje ya nchi yetu. Kwa sababu ya ukosefu sana wa huruma kama hatutaipa Wizara hii fedha za kutosha, naomba niseme kwamba, katika Bajeti zinazofuata, Wizara ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ipewe pesa inayostahili. *(Makofi)*

Tunapozungumzia *lobbying*, wanapokaa wakubwa katika *Paris Club,* maamuzi yanakuwa yamefanyika jana, watu wanapokutana ni kwa sababu wamekwisha kubaliana mbele ya *camera* watakapotazama waandishi wa habari watazungumzia nini. Hiyo ndiyo *function* ya watu tunaowatuma wafanye *lobbying. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kumtuma Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, ku-*lobby* na mkono mtupu. Mataifa yote yana-*lobby* kwa kutumia pesa. *(Makofi)*

Mwaka huu Taifa la Marekani pekee wanatoa shilingi bilioni 15 kwa ajili ya kusaidia UKIMWI duniani, wa Kenya tayari wameshafika kuomba Makao Makuu ya zile *fund* yawe Nairobi. Naomba nikuulize kama shilingi bilioni 15 zingeenda katika *Banking System* ya Tanzania, Dar es Salaam, kazi ngapi zingeanza leo? *(Makofi)*

Hadi kufikia jana Serikali ya Marekani ilishatangaza kutoa shilingi milioni 7 kwa ajili ya kumsaidia mwanamke mwenye UKIMWI aliye mjamzito, mtoto wake asipate UKIMWI katika nchi ya Uganda. Maamuzi haya ni *result* ya *lobbying.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Balozi zetu zina kazi ya kuangalia nini kinasemwa, wapi, katika nchi wanazotuwakilisha. Mabunge yanazungumza habari nyingi na muhimu ambazo zingeweza kuisaidia nchi hii. Tatizo tulilonalo ni kwa sababu Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, haina uwezo *(Financial Capability)* ya kuweza ku-*capture* habari zote ambazo zina maslahi ya Tanzaia. *(Makofi)*

Wainong'oneze Wizara waseme jamani kinaendelea hiki katika Bunge hili, katika nchi hii *response* yetu iwe hii. Kuna Wabunge wawili katika Bunge la Uingereza. Mbunge wa kwanza anaitwa Mheshimiwa Caroline Spelman, ameuliza maswali matatu katika Bunge la Uingereza. Yeye ni Waziri wa Mambo ya Nje ya nchi Kivuli, ameuliza swali linalohusu Serikali ya Uingereza inafahamu nini kuhusu tatizo la njaa la Tanzania na akauliza *specifically,* wanajua nini kuhusu tatizo la njaa la Singida na wanajiandaa kufanya nini?

Mheshimiwa Spika, kwa kumbukumbu za *Hansard,* Mbunge Caroline Spelman, ambaye ni Waziri Kivuli, yeye ni Mbunge wa Jimbo la Mariden. Mbunge mwingine ambaye ameuliza kuhusu njaa ya Tanzania katika Bunge la Uingereza anaitwa Mheshimiwa Gerry Stretor.

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa, Gerry yeye ni Mbunge wa Jimbo la *South West Gethern* katika Bunge la Uingereza na yeye ameuliza juu ya tahadhari ya njaa Tanzania na Waziri alipojibu akasema, "Tunasubiri maelezo kutoka Serikali ya Tanzania na sisi tutakuwa tayari kusaidia kama tukiulizwa".

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu gani? Kwa sababu kama Wizara hii itawezeshwa wapate kujua habari ambazo zimeulizwa ndani ya Bunge la nchi, ingempa nguvu sana Waziri anayehusika ama Rais, kupeleka ombi maalum kwa ajili ya mustakabali wa Taifa letu la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili ni suala la *priority*, kipaumbele kiko wapi katika kupanga mipango yetu. Naomba nirudie Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje ya nchi yoyote ile inashughulikia mustakabali wa usalama wa nchi inayohusika. Inashughulikia maslahi ya mahusiano ya nchi zote duniani, kwa ajili ya manufaa na ustawi wa Taifa linalohusika.

Mheshimiwa Spika, jambo langu la mwisho, kwa miaka mingi tumekuwa tukifuatilia matatizo yaliyowakumba ndugu zetu wa nchi ya Palestina na naomba nitoe masikitiko yangu na rambi rambi zangu

nyingi kwa wananchi wote wa Palestina ambao wamepoteza maisha yao katika vurugu ambazo zimeendelea miaka mingi nenda rudi. Naomba niipongeze sana Serikali ya Tanzania kwa kila wakati kwa kulisemea suala la mustakabali wa Taifa la Palestina. *(Makofi)*

Kufikia mwaka huu kabla ya mpango wa *Road Map* ambao umedhaminiwa na Serikali za *EU*, Marekani na Urusi, tayari Mataifa makubwa yalishasema sasa tunakubali kuwepo kwa Taifa la Palestina. Ninaunga mkono na ninaamini msimamo wa Tanzania miaka nenda rudi umesaidia sana kuwaletea Wapalestina heshima ya kuwa na Taifa lao na tuendelee kupambana mpaka wapate Taifa lao huru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hiyo, itakuwa ni suala la kuinyima Tanzania haki kama Sera yetu ya Mambo ya Nje inaweza isitilie maanani kuwepo kwa Taifa la Israel. Uhusiano wa Tanzania na Israel uliingia dosari mwaka 1967 baada vita vya siku sita ambayo vilipiganwa kati ya Mataifa ya Kiarabu na Israel.

Mheshimiwa Spika, tunafahamu kwamba, baada ya makubaliano ya *Camp David*, nchi nyingi duniani ziliweza kurejesha tena uhusiano wake na Taifa la Israel na mustakabali wa Taifa la Israel utakuwa ni muhimu kwa nchi ya Tanzania kama tunataka tuwasaidie Wapalestina kwa sababu tutawakumbuka Wapalestina, tutazungumzia na suala la Israel. Ukienda Dar es Salaam bendera ya Palestina inapepea, ningependa bendera ya Israel ipepee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi ya Kenya wana Ubalozi wa Israel. Ukitaka kwenda Israel unakwenda Kenya unachukua *Visa*. Ukitaka kwenda Brazil unakwenda Nairobi unachukua *Visa*. Ukitaka kwenda Canada, Australia na nchi nyingine hatujaweza kuwa na mvuto ama kujitahidi kuvuta nchi hizi zilete Balozi zao hapa. Lakini kingine hatujaweza sisi kwenda *reaching out.*

Mheshimiwa Spika, baada ya Vita vya Pili vya Dunia, Wayahudi zaidi ya milioni 6 waliuawa na wao ni watu ambao wamepita katika misukosuko ya maisha na siasa zote za dunia katikati yake ni pale Jerusalem.

Tunapozungumzia Jerusalem, nchi ya Tanzania haina sababu ya kuona haya kwenda kuweka bendera ya nchi hii katikati ya Jiji la Jerusalem kama walivyofanya nchi zingine. *(Makofi)*

Ukienda Abuja sasa hivi Ubalozi wa Israel unapepea. Hatuna sababu na narudia, hatuna sababu ya Tanzania kutokuwa na uhusiano wa Kibalozi moja kwa moja na Taifa la Israel.

Mimi nasema wengi wanakumbuka wakati wa *Operation Thunderbolt* ilipofanyika kuwaokoa mateka wa Kampala, mateka wa Entebe wale waliotekwa wakati wa utawala wa Amin na ile filamu inajulikana kama *90 Minutes to Entebe,* makomdandoo wa Israel walitua Entebe kwa kupitia Bonde la Ufa, wakatokea kuwaokoa wenzao waliokuwa wametekwa. Baadhi ya watu wakasema angalieni Israel imevamia anga la Uganda.

Mheshimiwa Spika, Tanzania na Uganda wakati ule tulikuwa kwenye vita na tuliwashinda. Tulimshinda Nduli Iddi Amin, kwa sababu wananchi wa nchi hii walikuwa na *determination* na tunaweza tukashinda *diplomatic impasse* isiyo na sababu kwa sisi ku-*embrace the Palestinian case at the same time, to embrace* kuwepo, thabiti kwa Taifa la Israel.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema haya, naomba kwa moyo mkunjufu na kwa dhati kuunga mkono hoja hii kwa asilimia 100. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. KILONTSI M. M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia machache niliyonayo.

Mheshimiwa Spika, naomba niende moja kwa moja kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na viongozi wengine katika Wizara, kwa hotuba nzuri ambayo imetolewa mbele yetu asubuhi hii ya leo. Napenda kuwapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia nitoe pongezi zangu kwa Balozi zetu, kwa kazi nzuri ambayo wameifanya, kwa kuitangaza nchi yetu nchi za nje kiuchumi, kibiashara na katika nyanja za utalii kama Mheshimiwa Waziri alivyosema. Balozi zetu wanafanya kazi kubwa sana, wanajitahidi katika mazingira magumu waliyonayo. Sisi lazima tuendelee kuihakikishia Jumuiya ya Kimataifa kwamba, Tanzania ni nchi salama na hata pale nchi mbalimbali kama Uingereza na nchi nyingine ziliposema kwamba iko hatari ya uvamizi katika nchi za Kenya na Tanzania. Naomba nisisitize kwamba, ni lazima tuendelee kuihakikishia Jumuiya ya Kimataifa kwamba, Tanzania ni nchi salama na wanaweza kuja bila wasiwasi katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama alivyotamka Mheshimiwa Waziri mwenyewe kuwa lazima tuendelee pia kuwahakikishia raia wetu wa nchi yetu na wageni wanaoingia katika nchi yetu juu ya usalama wa nchi yetu. Kwa kweli Watanzania wengi tungependa kuishi hivyo lakini bahati mbaya uko uchokozi unaotokana na nchi za jirani na ambao uchokozi huu kwa kweli umekuwa hautuachi katika amani hasa sisi tunaoishi katika mipaka na nchi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, sasa napenda nizungumzie juu ya matatizo yaliyoko mpakani mwa Tanzania na nchi jirani ya Burundi. Watanzania wengi wanaoishi mpakani pale wamekuwa wakishirikiana sana na wananchi wa Burundi kwa nia njema tu. Masoko yako karibu na wao wamekuwa wanakwenda na pia wanashirikiana kwa kufanya kazi pamoja, upande mwingine wanakwenda kwenye masoko ya upande mwingine na vivyo hivyo wengine wanakwenda kwenye masoko ya upande mwingine, tumekuwa tukifanya hivyo kwa muda mrefu sana.

Mheshimiwa Spika, lakini siku za hivi karibuni hali imeendelea kuwa mbaya na ndiyo maana hata wakati mwingine tunapokuja hapa Bungeni, tumelazimika kuuliza maswali mbalimbali yanayohusu jinsi gani sasa tunavyoendelea kuishi na hawa jirani zetu ambao kwa kweli ni ndugu zetu, maana hata misaafu ya dini inasema, "mpende jirani yako kama nafsi yako". Sisi Watanzania tumeendelea kuwapenda jirani zetu kama ndugu zetu na kama jirani zetu na kama sisi wenyewe tunavyojipenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana kwa kauli hii tumekuwa tukiwachukua wale wakimbizi wote na kuwaweka katika makambi katika nchi yetu, kwanza watu wetu wanawahifadhi, wakishawahifadhi wanawapa chakula, wakiwapa chakula kisha wanawaelekeza njia ya kwenda ili wafike makambini ambapo wataweza kuhudumiwa na Jumuiya ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nimewahi kuzungumza ndani ya Bunge hili kwamba, tatizo la wakimbizi *can not be generalized as a National problem, can not be taken as a National problem, it is an International problem.* Sasa kwa mantiki hii kwa kweli lazima Jumuiya ya Kimataifa ituelewe katika utaratibu huu na kwa misingi ambayo Mheshimiwa Rais wetu ameizungumza na akasema, kwa kweli sisi tunapenda sana kuwahudumia wakimbizi lakini Jumuiya ya Kimataifa pia ituelewe. Hivi sasa wakimbizi walioko katika Mikoa ya Kigoma na Kagera hawapati chakula cha kutosha. Hii imekuwa vurugu kubwa maana wanaingia kwenye Vijiji wanawavamia wananchi kwa kuwanyang'anya au kwa kuua. Sasa hili limekuwa ni tatizo.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa upande mwingine nawaomba Waheshimiwa Wabunge, niwape taarifa kwamba, kuanzia mwaka 2002 mpaka hivi sasa tunapozungumza, kuna wananchi kadhaa ambao wamepoteza maisha yao kule mpakani hasa katika Jimbo la Kasulu Magharibi. Sasa ninayazungumza ya Kasulu Magharibi lakini iko Buyungu na pia iko Kasulu Mashariki, kuna watu wengi wamekufa katika Majimbo haya na tunazo taarifa za kuaminika kabisa kwamba, hawa wameuawa na wananchi wa Burundi lakini wale wa kwangu nitakaowataja wameuawa na majeshi ya Burundi.

Mheshimiwa Spika, sasa katika Vijiji vya Muyama, Kibande na Mkatanga kuna wananchi karibu saba waliouawa na majeshi ya Burundi. Wa kwanza ni Toke Mnoni kutoka Kijiji cha Muyama, mwingine ni Barapanzi Kisama kutoka Kijiji cha Kibande, mwingine ni Tito Abel kutoka Kijiji cha Kibande, Majaliwa Juma kutoka Mkatanga, Theodora Isidori kutoka Kijiji cha Kibande, James Mmena kutoka Kijiji

cha Kibande na Gracia Lameck ambaye anatoka pia Kijiji cha Kibande. Hawa wote wameuawa kati ya mwaka 2002 na Januari, 2003 na majeshi ya Burundi.

Mheshimiwa Spika, lakini hali ni mbaya zaidi kwa sababu wanajeshi wa Burundi wanaingia nchini wanawateka watu wetu na kwenda nao Burundi. Ninayo majina ya watu watatu ambao ni Joseph Eliya, Stephen Joseph na Neema Amosi, wote wa Kibande, Bweranka na Kijiji cha Kitambuka mpakani ambao walitekwa na wanajeshi wa Burundi. Wakapelekwa Burundi walipofikishwa kule wakaingizwa katika makambi ya jeshi kisha wakaambiwa wasaini makaratasi yanayoonyesha ya kwamba, wao walikwenda kuleta vurugu nchini Burundi au walikwenda kuiba nchini Burundi. Lakini napenda kuwaelezeni kwamba, vijana wetu walikataa katakata kwamba, kwanza sisi hatujui kwa nini tulikamatwa, lakini pili sisi tulikamatwa kutoka nyumbani hatukukamatwa ndani ya Burundi, sasa mnatuambia tusaini uongo, makosa ambayo hatukuyafanya, sisi hatusaini mkitaka mtuue.

Mheshimiwa Spika, mwezi Januari wale vijana wote walirudishwa na Serikali ya Burundi. Viongozi wa Serikali ya Burundi walipowarudisha, mpakani tulipokuwa tunawahoji sababu za kuwakamata na kuwapeleka Burundi, walituambia hayo kwamba walikwenda kuiba na wengine walikamatwa wanaiba ng'ombe. Huyu binti alikamatwa yuko sokoni na pale sokoni yeye alikuwa amepeleka ndizi zake na soko lilikuwa limejaa. Lakini Gavana wa Burundi alituambia ya kwamba, siku hiyo kulikuwa hakuna soko, binti kama mwendawazimu alikwenda sokoni amebeba mkungu wake wa ndizi. Tulipowaita waingie ndani wote walikataa na binti akasema soko siku hiyo lilikuwa limejaa na watu walikuwa wamejaa na wanunuzi waliotaka ndizi siku hiyo walikuwa ni wengi lakini yeye alikamatwa, hakuruhusiwa hata kuingia sokoni.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, pamoja na haya na yale mengine ambayo nimewahi kuyataja nyuma, ya watu wetu kukamatwa ndani ya Tanzania, kupelekwa Burundi na kuchomwa moto, yote yanaashiria hali ambayo siyo salama kule mpakani.

Sasa tumekuja na hoja za aina mbalimbali hata juzi nimeuliza swali kwamba, sasa tutafanya nini katika hali ya watu wetu kupoteza maisha katika kiwango hiki? Hebu naomba nipatiwe maelezo ya Serikali ambayo ni sahihi siyo yale tu, jibu la kwanza lilisema, hatuwezi kudai fidia kwa sababu Burundi hakuna Serikali ya kuaminika. Hilo la kwanza. Lakini juzi mlisema, bado Serikali ya Burundi iko kwenye kipindi cha mpito sasa hatuwezi kudai chochote. Hivi haya ndiyo majibu sahihi ya Serikali ambayo inaweza kutuambia? Hayo tunayahitaji, nimekuja na maswali yote tuliyokwishauliza na majibu yote ambayo hayaridhishi ninayo pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba nizungumzie Balozi zetu katika nchi za nje. Balozi zetu nchi za nje zinafanya kazi kubwa sana kama nilivyosema, kazi za kiuchumi, kibiashara na kuitangaza biashara yetu ya utalii. Nami kusema kweli napenda kuwapongeza sana Mabalozi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini napenda niseme kwamba, mwaka huu kwa mfano, Tanzania ni Mwenyekiti wa *SADC,* Mabalozi wetu wanaoishi nje watakuwa ndio Wenyeviti wa *SADC* lakini *infrastructure* za Ofisi ya Balozi hizi hakuna, hakuna hata mahali pa kuwakaribisha kwenye vikao, Balozi nyingine zinawaita wanakwenda kwenye Maofisi yale, hawa hawawezi ni lazima wakakodi Ofisi sehemu nyingine. Kule Brussels lazima waende wakaombe kule *ACP House* ndio waende kuwakaribisha Mabalozi wenzao. Sasa wanawashangaa wanasema, nchi kubwa kama Tanzania mnatupeleka huko, hawaelewi hata kidogo. Tengenezeni basi hata ofisi ya kuweka *conference room* pale kwenye Ubalozi wetu wa Brussels. Nawapongeza kwa nia ya kufungua Ubalozi wetu wa Uholanzi maana nilitaka kuuliza kwamba, kwa nini hamfungui Ubalozi wa maana sana kama huo wa Uholanzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni kwamba naomba nizungumzie suala la Zimbabwe. Palitokea mzungumzaji alizungumzia suala la Zimbabwe, alizungumza maneno mengi sana, sasa hivi mimi sina muda, akasema hakuna demokrasia.

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, kwa kauli yake njema juu ya Zimbabwe. *Position* ya Tanzania *on Zimbabwe is quite clear, very clear.* Sisi hatuamini kama kuna *political crisis* ndani ya Zimbabwe, *it is exerce bated* na *land crisis.* Hii *land crisis* tunayoizungumza hivi Wazimbabwe kwa nini walipata uhuru? Tulielewe hili kama

Watanzania, sisi sio wageni katika siasa, tukishalielewa ndio tulichambue. Hivi demokrasia tunayoizugumza ni vurugu? Maana Zimbabwe kuna vurugu, hii vurugu siyo ya kuisaidia Zimbabwe kwenda kwenye demokrasia na ninyi mnajua demokrasia ni haki ya watu na matakwa ya watu, ndiyo tunayoitaka na siyo vurugu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwingine akazungumzia *East African Community,* akasema hivi sisi Wazanzibari mnatuwekaje kwenye hili? Mimi nafikiri ni lazima tuelewe kwamba, Wapinzani ni ndugu zetu na sisi tunawakubali katika haya, lakini tuzungumze lugha inayoeleweka. Tumewachagua Wajumbe wa kutuwakilisha ndani ya *Community* wote tukiwa hapa, wote tumewachagua, wapo wawakilishi watatu kule Zanzibar. Kuna Majaji wawili, mmoja wa Zanzibar na mmoja wa hapa, sasa kuna upungufu gani? Hayo mengine ni ya kukaa na kuyasahihisha lakini ni madogo na Tanzania ni nchi ya amani na ndio maana tuna Upinzani, unaweza kusimama ukazungumza tu. Lakini huo Upinzani ili tuuheshimu, basi uje na vitu venye mantiki sawa sawa ambapo ndani ya CCM tutavikubali tuseme sawa sawa. Lakini tunapinga hata Sera sahihi za Mheshimiwa Rais wetu, hapana hiyo hatutakubali. *(Makofi)*

Nimebakiwa na dakika chache lakini nilitaka kuzungumzia juu ya Mikataba ya Kimataifa. Mimi hapa sasa hivi nina Mikataba na *speech* za Waheshimiwa Mawaziri wa nchi za nje kama Kenya juu ya *coffee* na sehemu nyingine. Mikataba au *speech* za Waheshimiwa Mawaziri wetu mimi sina au Waheshimiwa Wabunge sisi hatuna, *we should be proud of what they present outside* ili na sisi tueneze hayo ili tuendelee nayo. Lakini kwamba tunakwenda nje tunatumia mambo ya wengine, nafikiri siyo sahihi. Waheshimiwa Mawaziri, watuonyeshe wanafanya nini kuhusiana na haya mambo ya mikataba ya nchi za nje na hiyo mikataba tunaitaka humu ndani tupewe sisi Wabunge kama wawakilishi wa watu ambao aidha tunawapeleka watu katika maendeleo au katika umaskini, maana haya ni yetu wote ili tukubaliane hapa. Sasa yote haya ni vema tukayafahamu. *(Makofi)*

Nilitaka nieleze baadhi ya mambo yanayoendelea katika nyanja mbalimbali katika utaratibu wa *negotiations,* niwaeleze nini kinafanyika na *Regional Authorizing Officers,* pamoja na *National Authorizing Officers* katika nchi zetu. Suala linalozungumzwa kubwa ni kwamba, hawana *capacity, forty years after independence* hatuna *capacity, can't we train our own people, yes we can, why don't we do it?* Ni matatizo yaliyoko ndani yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa na mengi lakini naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kwa hiyo, mengi yalete kwa maandishi basi, yatamsaidia Mheshimiwa Waziri. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. ANATORY K. CHOYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia machache katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile, napenda nimpongeze kabisa kwa namna ya pekee Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri na wataalam wake wote, kwa hotuba nzuri. Hiyo huwa ni kawaida yake Mheshimiwa Waziri, maana yake hotuba zake zote huwa zina mwelekeo safi na mara kwa mara huwa tunafarijika wakati anapokuwa anatoa hotuba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama kawaida ya Mheshimiwa Mbunge ni kuishauri na kuisimamia Serikali, hilo ni jambo la Kikatiba. Mimi hapa napenda kusema machache kama ushauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesoma katika ukurasa wa 28 ambao unaelezea namna nchi za wenzetu zinavyotoa ruzuku kwa wafugaji pamoja na wakulima. Hilo ni jambo sahihi na ni jambo zuri kabisa na la pekee.

Mheshimiwa Spika, mimi ushauri wangu na maoni yangu binafsi ni haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, napenda nijitolee mfano. Ni kwamba, kwa mfano mimi nakwenda kumtembelea Mbunge mwenzangu mahali popote pale, nawakuta watoto wake wamevishwa yaani wako *smart* na pia wanakula vizuri, lakini watoto wangu niliokwenda nao wanakwenda wakiwa wanaonyesha wana kwashakoo, nywele zimesimama, hawana viatu na pia wana matumbo makubwa, hivi mimi nitamwambia huyu Mbunge mwenzangu ambaye nimekwenda kumtembelea kwamba, bwana naomba usiwatunze watoto wako ili waje wafanane kama wa kwangu, nitafanya hivyo kweli? Haiwezekani.

Mheshimiwa Spika, mimi ninachokishauri ni kwamba, tumeshajua tatizo lililopo kwamba, wananchi wetu wanakosa ruzuku, tusije tukaangalia kile wanachokifanya na sisi tutafute ufumbuzi. Tutafute ufumbuzi maana yake matatizo haya yanafahamika kwamba wao wanawapa ruzuku, kama wanawapa hivi sisi tuwakataze wasiwape, tutafute ufumbuzi, haya maneno mengine *lamentations* huwa tunalalamika, hayatatufikisha mahali popote pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ruzuku ni lazima tuwape wananchi wetu, tutafute kila aina ya mbinu lakini haya ya kusema kwamba kwa kuwa Bush anawapa watu wake ruzuku eti hapo ndipo na sisi tudai haki, hapa amesema kwamba, ama kweli maskini hana haki mbele ya mwenyenacho. Tukumbuke kwamba, haki ya mnyonge ni hiyari ya mwenye nguvu, kama mwenye nguvu hatatuonea huruma, basi tutaendelea tu kulalamika. Kwa hiyo, sasa hatuna budi nchi zote za Kiafrika kukaa pamoja, wasomi tunao na pia watu ambao wamebobea kiuchumi, tuungane kwa pamoja ili tuhakikishe tunalitafutia ufumbuzi hili tatizo siyo kutoa malalamiko siku hadi siku hatutafika. Hilo nilikuwa napenda nilitoe kama ushauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, ningelipenda kuzungumzia suala la wakimbizi. Kwa ile Mikoa ambayo imekwishaathirika au ambayo inapokea wakimbizi ukiwemo Mkoa wa Kagera, Kigoma na Rukwa, kwa kweli sisi ndio tunaofahamu yanayotukuta huko. Tatizo kubwa ukimwambia mtu ambaye hajawahi kuishi pale utafikiri unaleta mzaha lakini nichukulie kama Mkoa wa Kagera, Wilaya ya Biharamulo, Tarafa moja inayoitwa Rusahunga, ambayo ndiyo iliyokuwa na Kambi ya Wakimbizi, tulikuwa tunatoa maji na kuni kwa wale wakimbizi, kwa kweli sisi tumeathirika kwa namna ya pekee.

Mheshimiwa Spika, hili nataka kulisema kwa utaratibu huu. Nchi za Rwanda na Burundi ni nchi ndogo sana kwa mfano, Rwanda ina *square meter* 27,830 na *population* yake ni 6,000,000. Sasa fikiria wale wanapokuwa wanapigania kule wanapigana ili kutafuta mahali pa kukimbilia, sasa wanapokuja huku wanatafuta mahali pa kuishi, huu siyo ukimbizi. Lazima tuhakikishe tunatafuta kiini cha ukimbizi, tangu miaka ya 50 ni wakimbizi, hivi hilo limekuwa ni donda ndugu, kwa nini tusilitafutie ufumbuzi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wanyarwanda na Warundi wazo lao kubwa na lengo lao kubwa wanasema kwamba, kwa kuwa wao wanauana kwa wingi basi ni lazima wazaliane. Ndivyo wanavyosema kwamba lazima tuzaliane ili tufidie hilo pengo ambalo linatokea baada ya mauaji. Juzi juzi tu mmeona mauaji yalivyotokea. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni lazima tutafute kiini cha kuhakikisha hili tatizo la wakimbizi linatoka, linakwisha. Mimi huwa napenda kusema kwamba, ni tofauti sana ninapowaona wakimbizi kutoka Rwanda na pia wakimbizi kutoka Burundi wanapewa uraia. Hawa ni majirani zetu, kila mara watakapokuwa wanapigana, watakapokuwa wanakuja huku tutawaonea huruma kwamba tuwape uraia lakini mara baada ya labda kutengemaa kwa nchi zao, itabidi warudi maana yake Waswahili wanasema: "maji yakichemka hayasahau kwao baridi". Kwa hiyo, watakuwa wanafanya mchezo wa mara kwa mara kwamba wanapokuwa wengi ni lazima wapigane halafu watafute mahali pa kukimbilia. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi nyingine ni nchi ya Rwanda. Rwanda ina *square meter.*

**WABUNGE FULANI:** *Kilometer.*

**MHE. ANATORY K. CHOYA:** Nasema nchi nyingine ni ya Rwanda.

**WABUNGE FULANI:** Burundi.

**MHE. ANATORY K. CHOYA:** Kama nimetaja Rwanda basi. Nchi nyingine ni ya Burundi ina *square meter. (Kicheko)*

**WABUNGE FULANI:** *Kilometer.*

**MHE. ANATORY K. CHOYA:** Mheshimiwa Spika, nchi nyingine ni ya Burundi. Burundi ina *square kilometer,* hebu sikilizeni kwa makini. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilifanya *vice versa* ni kwamba, Rwanda ina *square kilometer* 26,338 na *population* ni watu milioni 7.3. Kwa hiyo, hao mara kwa mara wamekuwa wakipigana wao kwa wao ili kutafuta mahali pa kukimbilia kutokana na zile nchi kwamba ni ndogo.

Mheshimiwa Spika, Burundi kama nilivyokuwa nimesema ina *square kilometer* 27,830 na *population* ni milioni 6.2. Kwa hiyo, basi hapo ni hali halisi kwamba, hawa wataendelea kupigana miaka nenda rudi kadri wanavyozaliana. Tunachokitafuta hapa ni kutafuta ufumbuzi wa uzazi wa mpango, tunapokuwa kwenye *roundtable* na pia tunapokuwa kwenye Mikutano ya Kimataifa, ni lazima sasa tuangalie ni namna gani hawa ndugu zetu wataendelea kuwa watu ambao kutokana na uchumi wao, kutokana na nchi zao na pia kutokana na uzalishaji wa vyakula, vyote vitahimiri ile *population* yao. Vinginevyo sisi tunaotoka katika Mikoa hiyo tutaendelea kuhangaika, kuumia na kuteseka na huku hakuna hata fidia ya kweli ambayo tunaipata sisi wananchi tunaotoka kwenye Mikoa hiyo inayoathirika, tumechoka ni lazima tuliseme hili. Vile vile, Jumuiya ya Kimataifa ihakikishe inawatengenezea maeneo kwamba wakae huko huko makwao *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda tena nijielekeze katika ukurasa wa 58, kifungu cha (ii): “Kutengeneza mwongozo wa kazi na masharti ya sifa za kuwa Mwakilishi wa Heshima wa Tanzania”, kifungu cha (v) ambacho kinasomeka: “Kushiriki katika mikutano na majumuiko muhimu ya Kimataifa” na kifungu cha mwisho cha (x) “Kushirikiana na Idara Kuu ya Utumishi kuandaa Mpango wa Kuboresha utendaji kazi Wizarani”.

Mheshimiwa Spika, ni kwamba, nakumbuka wakati Mkutano wa *SADC* ulipokuwa unafanyika pale *Golden Tulip*, wakati huo mkutano huo ulifunguliwa kama sikosei na Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Pale nilivyokuja kupata taarifa ni kwamba, wale washiriki walivilalamikia vyombo vilivyokuwa vinatumika. Vile vyombo vya ukalimani, ni vyombo vilivyotengenezwa mwaka 1969. Kwa hiyo, vile vyombo havina kabisa teknolojia ya kisasa ambayo inawawezesha watu kuwasiliana ndani ya ukumbi ule. Kwa hiyo, napenda kuwaomba Wizara ihakikishe kwamba, ina *moderate* vyombo vyake ili tuweze kukidhi hizi kazi ambazo Wizara imezitamka yenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halafu kwa upande wa Balozi zetu, mimi wakati nikiwa *Immigration Officer,* nilifanya kazi mpakani mwa Tanzania na Kenya, Rwanda na Burundi na Zambia, ni kwamba wananchi walikuwa wanalalamika sana. Walipokuwa wanafika kule wanapopatwa na matatizo, wanapohujumiwa Balozi zetu pamoja na kazi nzuri wanazozifanya za kutangaza utalii, biashara na kadhalika lakini Balozi zetu zinajiweka pembeni katika kuwatetea watu wetu. Lazima Balozi zetu ziwe mstari wa mbele katika kuhakikisha zinawatetea watu wetu, yule anayekwenda kule anakwenda kuhangaika, asitetee uhalifu, msimtetee mhalifu. Lakini kama ni mtoto wako hata kama anakimbizwa na jambazi, kabla hujajua ni kwa nini anamkimbiza, utamwambia si ni wa kwako. Inabidi Balozi zetu zifanye kila liwezekanalo ili kuhakikisha zinawatetea watu wetu kwa gharama yoyote ile kama Marekani wanavyofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, asubuhi nimesikia Russia inatoa *ultimatum* kwa Wasudan kwa ile *helicopter* iliyokamatwa kule kwamba, wanawataka watu wao. Sasa na Balozi zetu zihakikishe zinawatetea watu wetu, zisijiweke pembeni. Watu wetu ile ni nguvu kazi, ni Watanzania ambao wamekwenda kule kuhangaika kutafuta riziki. Sasa iwapo wewe unajiweka pembeni unamwogopa nani, yule ni mtu wako. Lazima uhakikishe na wewe unaonyesha kwamba, umekwenda kule kwa ajili ya maslahi ya Watanzania walio wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda niseme kwamba, naunga mkono tena hoja kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED ABDULLY ALLY:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa hakika sina mengi sana ya kuchangia lakini ninalo la muhimu kidogo. Kwa kusema hivyo napenda kuunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala langu la kwanza ambalo naomba kwa heshima na taadhima kulichangia, ni kuhusu uwiano wa Mabalozi wa Tanzania. Tanzania kwa mujibu wa kitabu hiki ina Mabalozi 28 lakini Mabalozi waliokuwepo hao ni kutoka nchi mbili zilizoungana yaani Tanganyika na Zanzibar. Katika Mabalozi hao 28 labda kutoka upande wa pili hawazidi wawili au watatu, hapo hapana uwiano.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaomba au tunaiomba Wizara inayohusika angalau na sisi upande wa pili tusogezewe kidogo, kutusaidia kuwachagua Mabalozi kutokana na sifa zilivyo, Zanzibar kuna wasomi wengi tu, angalau tuwapate wafike nane, angalau tuwapate nane katika hao 28. Hilo ni suala langu la kwanza ambalo naliomba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, katika kitabu hicho hicho kumezugumzwa mambo ya Muafaka. Wenzetu walioanza kwanza na mambo ya Muafaka lakini wakashindwa, waliahidi kwamba wataisaidia Zanzibar na mpaka leo hawajaisaidia kitu.

Tunaomba wazungumze na wanaohusika kwa haraka ili waweze kuisaidia Zanzibar ina matatizo hata ya kulipa umeme, kwa hiyo, tusaidiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka kulizungumzia kuhusu Muafaka ni kwamba, Muafaka umeleta amani sana kule Zanzibar, tunashukuru sana. Lakini amani hiyo imesababisha makubaliano ya pande mbili inapofika katika mambo ya kupata haki au uchaguzi inakuwa ngumu mfano mmeona Pemba, Muafaka uliwekwa upande na hali halisi ilikuwa ngumu. Tulikubali kwa kuwa wenzetu vile viti vilikuwa vyao toka mwanzo hatukuwa na sababu lakini itakapokuwa sasa tunang'ang'ania hatutakubali, hilo sio siri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo napenda kulizungumzia ni kuhusu biashara za nchi za nje kwa sababu ni mambo ya Muungano, lakini Zanzibar inaathirika sana kwa kubanwa na wenzetu wa *TRA* mpaka tunakuwa hatuna pumzi. Kwa hiyo, tunawaomba wenzetu wa *TRA* watuachie kidogo hali yetu kule ngumu tuweze kulipa umeme, itusaidie. *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka kulizungumzia ni kuhusu misamaha ya misaada ambayo Tanzania inapata, misaada hiyo kule Zanzibar hatufaidiki na sisi jamani ni nchi moja inakuwaje misaada hiyo inasamehewa huku tu upande mmoja kule wanapata shida? Tunaomba na sisi ni nchi maskini vile vile tusaidiwe katika mambo ya misaada isiwe inafaidika Bara tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfano mzuri tunaomba wenzetu Bara kwa kuwa wao wanapata misamaha kutoka nchi za nje na sisi watusamehe deni la umeme kama walivyosamehewa wao kwa sababu Zanzibar hatuwezi kulipa deni la umeme la shilingi bilioni 32. Zanzibar ilikuwa imezuiwa misaada siku nyingi tu kwa muda wa miaka nane na mnajua nani alizuia sio siri leo wanasimama hapa wanalaumu kule Zanzibar hatupati misaada wao ndio wamesababisha tukafikia hapa, leo wamesahau? Naomba utusaidie sana katika hilo kwa kutupa msamaha katika umeme kama mnavyopewa ninyi. *(Kicheko/Makofi)*

Lingine ni kuhusu *NEPAD*, iko Bara tu kule Zanzibar haipo na ilikusudiwa kwa Tanzania na sisi kule ni Watanzania jamani mbona mnatusahau, faida hii inayopatikana hapa mtupe, mtusaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni letu lakini wenzetu hapa walilalamika sana, Mkuu wa Upinzani alisema kwamba, watu wawili wateuliwe, Mheshimiwa Rais Zanzibar ameshasema kwamba, hateteua, ameshajibu. Hili wala halina mushkili hatateua wasipate taabu bure. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni nchi ya Muungano, inapoona hivi sasa Tanzania kuna jambo kutoka nchi za nje litakuja ni vizuri na wao wakakaa na wenzao upande wa pili, wakaelewana ili pasitokee mivutano. Mfano hawa Wazungu wa umeme wanaitwa nani vile majina yao? *(Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** *Net Group.*

**MHE. MOHAMED ABDULLY ALLY:** Eeh, *Net Group. Net Group* wametoka Afrika Kusini wamekuja Tanzania katika nchi ya Muungano. Ilikuwa wenzetu hawa wa Tanzania Bara wakae na Zanzibar wawaambie hivi sasa sisi tumeshindwa kuendesha Shirika hili la *TANESCO* tunawaita Wazungu waje kuendesha. Kwa hiyo, lazima mjirekebishe sasa kibiashara mkae hivi, mkae hivi, sio wanakuja Wazungu hapa bila wenzao kujua wanafanya wanavyotaka wala hawajui kwamba suala hili ni la Muungano na la kisiasa. Haya ndiyo makosa waliyofanya wenzetu, matokeo yake wanatunyanyasa kule ingawa umeme ule ule uliotoka Zanzibar unapelekwa na Bagamoyo kwa Ndugu yangu Kikwete. Nyaya zile zinatoka Zanzibar halafu zimeunganishwa na kupelekwa Mkoa wa Pwani, hakuna maneno ni nchi moja lakini tena kwa nini tunavuana nguo? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, CCM haing'ang'anii kabisa uongozi, tunakwenda kwa utaratibu inapofika wakati mtu yule anaondoka tu kwa taratibu, kwa ngoma hasa, mfano, viongozi wetu wengi tu wameshaondoka Marais wote waliofikisha miaka kumi wameondoka. Lakini sio kila siku mtu yule yule, Rais yule yule, Katibu Mkuu yule yule, Mwenyekiti yule yule, mwenye uamuzi yule yule, sasa nani anang'ang'ania uongozi hapo? Hii ndiyo hali yetu ilivyo na haya yote nayasema kwa sababu nimeyasikia humu ndani ilipokuwa inachangiwa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, safari hii Mheshimiwa Kikwete, angalau kabadilika kidogo, sio siri kaweza kusaidia mambo mengi tu kule Zanzibar katika Ofisi yetu ya Mambo ya Nchi za Nje. Kaweza kujenga Ofisi yetu ambayo ilikuwa mbovu sana, inavuja, inapendeza sasa ukipita tu utajua hii ni Ofisi ya Mambo ya Nchi za Nje. Kapeleka gari, wafanyakazi, hivi ndivyo inavyotakiwa na upite upitie ukazungumze nao usaidie sio kama kila siku tunakuja hapa tunakupigia kelele, hilo tumefurahi na tunakuunga mkono, tuko pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesema sina mengi lakini muhimu naomba mzingatie sana hayo niliyoyasema. Sasa hivi hali yetu ya Muungano kuhusu mambo ya nchi za nje ni nzuri, tunaomba izidishwe kabisa ilivyo, watoto wetu wa Zanzibar wapate elimu waende huko nje wakasome ili waje kutawala. Sisi kule Zanzibar, CCM tutatawala maisha bwana hakuna mchezo kule. *(Makofi/Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Hatukubali

**MHE. MOHAMED ABDULLY ALLY:** Tutawala maisha hatuna mchezo kama mtakuja kutulaumu mtatulaumu wakati huo. Yule mtingisha kibiriti yule aliyetingisha kibiriti anasema kimelegea hakikulegea bwana kiko vile vile. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nilisema sina mengi isipokuwa hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MUTTAMWEGA B. MGAYWA:** Mheshimiwa Spika, naomba kukupongeza kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wenzetu, ambao tumeungana nao pamoja kuendeleza jukumu la kuwasaidia wananchi.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kutoa pole kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu, ambao wamepatwa na misiba au majanga mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda kutoa shukrani kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba, mtindo tulionao wa kujaliana kwenye matatizo ni mtindo mzuri, nawapongeza sana kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zaidi nitaongelea kuhusu Balozi zetu za nje. Kwanza, nawashukuru kwa kazi nzuri wanayoifanya lakini pamoja na hayo kuna matatizo mbalimbali ambayo yanazikumba Balozi zetu na wamejitahidi kusahihisha matatizo hayo huko huko kwa kutumia Bajeti Ndogo, kwa hilo, nawapongeza.

Mheshimiwa Spika, lakini kubwa zaidi ambalo linanipa shida ni kuhusiana na Balozi zetu ambazo tulitegemea kwamba, zingefanya majukumu makubwa ikiwa ni pamoja na kutafuta masoko, teknolojia kwa maana ya kuhamisha teknolojia kutoka nje, kwa hiyo, tumejikuta Balozi zetu hazifanyi kazi hii. Tunafuta masoko ambayo yanatarajiwa yapatikane kutokana na Balozi zetu ambazo ziko nje.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo moja limewakumba wanafunzi wetu kwa mfano, Uingereza kulikuwa na malalamiko mengi ambapo wengine wametutumia hata barua kuomba Bunge liwasaidie kwamba hakuna ushirikiano mzuri kati ya Balozi na wanafunzi wanaosoma nje. Wanapokwenda kwenye Balozi hizo aidha wanakimbiwa, hawapewi misaada ya kina au kueleweshwa mambo mbalimbali wanachukuliwa kama ombaomba wa Ubalozi.

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa najaribu kuelewesha Balozi zetu kwamba, kwa mfano nchi ya India inaingiza pesa nyingi sana kutoka nje kwa kupitia wanafunzi na Wahindi ambao wako nje ya nchi hiyo kwa maana ya kufanya kazi. Wameunda Jumuiya ambayo inawaunganisha Wahindi wote kuhakikisha kwamba, angalau 20% ya pesa yao yote ya nje inarudi nchini. Chukulia mfano Tanzania tuna zaidi ya vijana 3,000 ambao wako Uingereza, ikiwa vijana hawa kila mmoja angeleta Pound 300 zikatumwa huku wafungue Akaunti zao ni kiasi gani tungekusanya kutoka kwa vijana hao? Nadhani kuna haja Balozi hizi kukaa nao kwa karibu, wawaeleweshe wajue umuhimu wa kuikumbuka nchi yao ili wa-*invest* kwao badala ya kutumia fedha hizo nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine naomba niipongeze Kamati ambayo ilisema hapa kwamba, Waheshimiwa Wabunge tumepitishiwa Bendera na tutatumia bendera za Bunge. Kwa kweli ni jambo lililokuwa linatukera sana Waheshimiwa Wabunge, ukichukulia kwamba, unapokuwa Jimboni umechaguliwa na wananchi wa Vyama mbalimbali mfano CCM, *TLP,* CHADEMA, sasa inapokuwa kwenye gari lako umeweka bendera ya Chama sio rahisi mwanachama wa Chama kingine kukufuata kuleta hoja matokeo yake anasita kukuona. Hoja hiyo niliwahi pia kuliandikia Bunge kipindi cha nyuma wakanijibu kwamba wangeijibu. Nashukuru leo imejibiwa. Hiyo ni kumpa Mbunge uhuru wa kuongea na wananchi bila kujali Chama gani anatoka.

Mheshimiwa Spika, lakini katika mapendekezo niliyokuwa nimetoa, nilipendekeza kwamba, mbali na bendera kwa vile bendera tumejifunza nje kwamba wenzetu kule nje Wabunge wana bendera zao ili kumpa uhuru zaidi Mbunge pia kwa ajili ya mahusiano na wananchi au kuwakilisha Jimbo, ni wakati muafaka sasa hata anapohama Chama hicho ahame na Ubunge wake, kama wanavyofanya wenzetu kule nje kwa sababu tunajifunza kutoka nje na ni lazima tujue kwamba hatuwezi kwenda peke yetu, tunaenda na wenzetu nje na ndio maana ya Wizara hii kwamba, tunashirikiana na ni kazi ya Wizara kuona wenzetu wanaendaje na wanacheza mchezo gani. Sasa basi kama tumeamua kuwa na bendera ili kumfanya mwananchi awe huru kumwona Mbunge wake, basi na Mbunge awe huru anapohama Chama kama wenzetu. Hiyo ni hoja nadhani mtaifikiria. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Rudi. *(Kicheko)*

**MHE. MUTTAMWEGA B. MGAYWA:** Sio kurudi huko, kwa sababu sikuanzia huko. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naomba nisisitize suala la kuhamisha teknolojia, suala hili ni muhimu na ni kazi ya Balozi zetu. Balozi wetu aliyepo *South Africa,* atupe siri hawa wenzetu wa *South Africa* wana-*manage* vipi Idara, mashirika mpaka leo hii Tanzania tunafikia ku-*import* watu kutoka nje? Tunao wasomi ambao wana *Ph.D., Masters,* wamesoma nje. Sasa tunataka huyu Balozi wa Afrika Kusini, atuambie hawa watu wa Afrika Kusini wanakuja na teknolojia ipi kwa sababu mashirika yote tumeweka watu kutoka nje na zaidi ni Afrika Kusini. Hizo ndio kazi za Balozi kama zilivyo Balozi nyingine, unakuta wanashutumiana mfano Marekani, Urusi kwamba, huyu ameiba teknolojia, huyu ameiba ujuzi huu, sasa ni kazi ya Balozi zetu pia kutufanyia kazi hiyo ili tuondokane na ku-*import* wasomi.

Mheshimiwa Spika, niongelee kidogo kuhusu amani, mimi sio mshabiki wa vita, ninapoongelea suala la Marekani na Mataifa madogo ninaona kama kuna ubabe fulani na unakuja pale mtu anakuambia kwamba anatengeneza amani. *Okay,* Iraq wananchi wake walikuwa hawana amani, wamepambana wameweka amani sasa na sisi Tanzania kwa vile ni dunia ya tatu, tumwombe pia ashughulikie amani ya Burundi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuwaambie wazi kabisa kwamba, ulisaidia kule sasa saidia amani ya Burundi na wao wakae sawa na nchi nyingine jirani ili tuondokane na kero ya wakimbizi na kuhatarisha maisha ya wananchi wetu wa mipakani na vita pia hufunzwa, kwa maana hiyo siku moja na sisi tunaweza kujifunza vita hiyo. Kwa hiyo, naomba tuwaambie wazi ijapokuwa ni vigumu kwa sababu tunawategemea lakini kwa sababu mimi siwategemei, naishi kwa pamba ya kijiji, nina uwezo wa kusema hayo kwamba, hatuwategemei tutawaambia wazi.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni kuhusu misaada. Tumepokea misaada mingi sana kutoka nje na misaada iko katika Wizara hii na misaada yote hiyo imetokana na mahusiano ya Tanzania na nchi hizo. Nikihesabu misaada yote ambayo tumepokea kwa muda wote wa Bajeti iliyopita na Bajeti hii ni mingi mno, je, Ubalozi wetu ulioko labda Uingereza hauwezi kutupa siri hiyo wanayofanya inakuwaje tumepokea misaada mingi sana lakini tunaona hatuendi? Wao wanasema tumetoa *billions of money* lakini ukiangalia Mtanzania wa kawaida hana hela. Sasa atupelelezee kule tuone inakuwaje au hizi hela zinarudi na zinarudi kwa njia ipi? Kwa sababu misaada mingi sana tumepokea lakini fedha hiyo hatuioni kwenye mifuko ya wananchi, zinakwenda wapi?

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi hii, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefikia mwisho wa kipindi cha asubuhi. Watakaochangia mchana mpaka saa kumi na mbili ni wa nne nao ni Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Gwassa Sebabili, Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, halafu watoa hoja wataingia.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja jioni.

*(Saa 06.54 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti*

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza kabisa, nakushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii ya kwanza jioni hii ili niweze kuchangia kwenye hoja ya Wizara hii ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama kuunga mkono hoja ya Wizara hii na kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Mabalozi wetu, pamoja na watumishi wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayofanya ya kuiwasilisha nchi hii katika nchi mbalimbali, mikutano mbalimbali na kujenga jina zuri la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni kioo cha nchi, ndiyo kioo chetu katika masuala na mahusiano na nchi za nje na najua ni kazi ngumu sana kwa mema na mabaya na najua hasa Waziri huyu sijui ana *passport* ngapi kwa sababu kila wakati yupo njiani. Mara yupo huku, mara yuko huku na ana familia yake, nadhani haifaidi hata kuwa na mzazi wao mmoja kwa sababu ya kazi tuliyomkabidhi. Katika hili anafanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ningependa kusema kwamba, nadhani nimeelewa hotuba ya Wizara hii pamoja hii *new foreign policy.* Nimesoma hotuba ya Wizara vizuri na nimeelewa. Hotuba

inazungumzia masuala ya ugaidi, migogoro ya Bara la Afrika, vita vya kindani vya Mataifa yetu, habari za vita katika Maziwa Makuu, Umoja wa Afrika, madeni, umaskini na nafasi ya Tanzania katika masuala haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nashukuru wenzetu wamejitahidi kudumisha jina zuri la Tanzania na jukumu la Tanzania la kihistoria katika kutetea uhuru wa Mwafrika. Kabla ya uhuru wa Bara la Afrika, Tanzania ilikuwa ni kimbilio la wapigania uhuru na hata baada ya Afrika kupata uhuru bado tumejaza wakimbizi zaidi ya laki sita, wapo hapa. Wakimbizi hawa wanasababisha matatizo mengi kwa Watanzania kama ilivyokuwa wakati ule, tunapigwa mabomu na nchi za jirani kwa sababu ya kuwa na wakimbizi katika nchi hii lakini hakuna tulilofaidi. Vijana wetu wamekufa nje ya nchi hii kama vile Afrika Kusini, Zimbabwe, Msumbiji na Uganda, kuna makaburi na tulikuwa tunachangia wakati ule kwa kutoa chakula, damu, nguo, fedha ili wenzetu wapate uhuru. Lakini kama kawaida ya mambo haya ya wema, tenda wema nenda zako usingoje shukrani, binadamu hawana wema kwa kila utakalowatendea. Huenda tumebaki hapa tulipo na umaskini huu kwa sababu tulielekeza nguvu zetu kwenye ukombozi wa wenzetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili ningependa nipongeze tena ukurasa wa 24 wa hotuba ya Waziri. Nimpongeze yeye, Rais wetu na Mabalozi wetu, kwa kazi nzuri wanayofanya ya kudumisha jina hili. Ni kazi ngumu na hivi sasa tunaanza kuheshimika. Kuna wakati niliwahi kutoa hadithi hapa, nilikwenda New York na wenzetu wa Kenya na Uganda. Sasa Mwamerika Mweusi mmoja alikuja pale akatuuliza sisi watatu wewe unatoka wapi, wa Kenya akasema Tanzania, akaja kwa yule wa Uganda, akasema Tanzania, akaja kwangu, nami nikasema Tanzania. Akasema Tanzania *everybody Tanzania why?* Nikasema angalia *passport* mimi natoka Tanzania. Baadaye akauliza kwa nini wenzako wanataja Tanzania. Wakati ule kule Uganda kulikuwa na Idd Amin na pale pengine mambo hayakuwa mazuri, nikasema mimi sielewi. Lakini ni kwa sababu Tanzania ilikuwa na jina zuri. Kwa hiyo, kila mtu alitaka kujihusisha na jina zuri. Kazi hii ya wenzetu ya kudumisha jina zuri la Tanzania kama walivyofafanua katika ule ukurasa wa 25, tunaomba waendelee nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kazi kubwa ni namna ya kudumisha sifa hizi na jina hili. Tukienda huko nje wakati mwingine wanauliza unatoka wapi, ukisema Tanzania, wanauliza nchi ya Nyerere? Sasa nasema kazi hii ya kudumisha jina zuri ni pamoja na Watanzania wote kuwa waangalifu kuchagua viongozi wanaofanana na jukumu hili kwenye ngazi za juu, jukumu la kutunza jina la nchi hii. Hii ni kazi ngumu sana na mambo mazuri hayaji tu. Sasa katika hili kama walivyoeleza katika ule ukurasa wa 24, ni kweli Bara letu lina matatizo. Wengine wanaita bado ni Bara la giza, wengine wanaita Bara la balaa, Bara la wakimbizi, Bara la UKIMWI, Bara la matatizo ya ukame, njaa na Bara la umaskini wa kupindukia. Hivi sasa katika mabara yote ya dunia nadhani kwa upande wa umaskini hili ndilo linaloongoza. Katika zile nchi nyingi maskini zinatoka hapa, wastani wa watu wengi wanatumia dola moja kwa siku na hili ni tatizo. Unawezaje kudumisha majivuno yetu kama tunaishi kama ombaomba? Hili ni tatizo kubwa.

Lakini Mheshimiwa Naibu Spika, aibu zaidi pale unapoangalia kwenye Televisheni, Waafrika wamekazana kujifunza kuua wenzao, wanawinda wenzao kama sungura na wanafurahia kuua wenzao. *Is a continent of misery*. Hivi sasa wanamalizana tu, *as if* UKIMWI hautoshi, yaani kumalizana kwa bunduki. Tunataka Wazungu ndiyo waje kutukomboa tena, ni aibu tena aibu sana na kwa kweli ni aibu ya hali ya juu sana. Nafurahi kwamba, Tanzania ni moja ya nchi zinazosaidia kutatua matatizo haya ya Maziwa Makuu. Wanakuja hapa kila wakati kama ilivyokuwa wakati wa Hayati Mwalimu Nyerere na tunaendelea kudumisha sifa hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili naomba kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Jakaya Kikwete, Mabalozi wetu, Rais wetu na watumishi wote wa Wizara yake, kwa kazi hii ngumu wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu ya pili ni kwamba, Watanzania tuendeleze na kudumisha jukumu hili la kihistoria. Kabla na baada ya uhuru wa Tanganyika mwaka 1961 Watanganyika na Watanzania baadaye tulifanya mambo yafuatayo:-

(a) Tuliwasha mwenge na kuuweka juu ya Mlima Kilimanjaro. *(Makofi)*

(b) Tulishiriki kuunda Umoja wa Afrika *(OAU)* wa wakati ule. *(Makofi)*

(c) Tulikubali Tanganyika iwe Makao Makuu ya Ukombozi katika Bara la Afrika mwaka 1964. Hayati Mwalimu Nyerere, alikubali nchi yake iwe ndiyo Makao Makuu na alitenga sehemu ya nchi yake huko Kongwa itumiwe na wapigania uhuru. Wapigania uhuru kutoka Afrika Kusini, Namibia, Zimbabwe na Angola. Waliishi pale Kongwa kwa uamuzi wa *OAU* wa mwaka 1964. Wengine wote walikuwa wanaogopa maana unapotunza watu wanaopigana unaweza kuangamiza watu wako na ndivyo ilivyotokea katika Mikoa yetu ya Lindi na Mtwara.

(d) Si hivyo tu katika kutetea uhuru tulipeleka askari wetu kwenda kushiriki katika kukomboa nchi za Afrika na ndiyo maana kuna makaburi ya watu wetu huko Zimbabwe, Msumbiji na Afrika ya Kusini. Askari wetu wamefia kule Watanganyika na Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, malipo ya uhuru wetu ni nini? Mimi nilishiriki vile vile Msumbiji na Ndugu Museveni, Balozi Kileo kule Addis, tulipigana kule wakati tukiwa *Youth League.* Sasa tunapozungumzia hatma ya Afrika ni vizuri tukakumbuka kwamba, watu kama Nelson Mandela, Robert Mugabe, Hayati Joshua Nkomo, Oliver Turnbo na Mtumbuka aliyeko *World Bank* na *Second Commander* wa Jeshi la *South Africa* ni *product* ya Tanganyika - Tanzania. Walikuwa Mgagao na Dakawa na ndiyo maana mara kwa mara wanakuja hapa kukumbuka makaburi ya wenzao waliofia hapa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo langu ni kwamba, Wizara hii ipeleke *agenda* hii kwenye Umoja wa Afrika kwamba, pale mlipoamua mwaka 1964 kuwa pawe panatunza wapigania uhuru tuweke alama. Tuweke alama ya kumbukumbu ya historia ya nchi hii na Watanzania tuchangamke katika hili tume-*sacrifice* juzi amekuja Makamu wa Rais wa Namibia, akaomba akaone alipokuwa anakaa wakati anatafuta uhuru. Sasa kama tusingejali pale angekwenda kukuta tumejenga vitu vya ovyo ovyo au labda tumelima mashamba hakuna kitu. Lakini alitoa machozi alipoona makaburi ya watu wa Namibia, *South Africa,* Msumbiji na kwingineko yapo pale, lakini hakuna alama. Katika nchi nyingine mahali kama pale panakuwa kama mahali pa hija na ndiyo maana *South Africa* kila mwaka, mwezi fulani wanakuja pale Mazimbu kufanya kama hija ya kukumbuka wenzao. Sasa Watanzania tuchangamke.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna makambi yafuatayo: Mgagao, Nachingwea, Tunduru, Bagamoyo, Kongwa, mote humu na Dar es Salaam pale Kurasini. Hizi zote ni Kambi za Wakimbizi lakini mahali pengine kama Ujerumani na wapi vijana wanakwenda kufanya *homage* pale, kukumbuka wazazi wao walipatia wapi uhuru na inakuwa ni maeneo ya utalii. Katika *vision* ya *foreign policy* pale na kwa njia hiyo inaweza hata ikawa ni maeneo ya utalii na mkatengeneza hata fedha watu wakifika pale. Kwa hiyo, nilikuwa napendekeza tufanye hilo.

Vituo vyote hivyo mahali pengine pamegeuzwa Makambi ya wafungwa, wakija wale wanaona wenzao tena wamefungwa na wao hawakuwa wamefungwa, siyo vizuri. Maeneo yote niliyoyataja hayo tushirikiane, tuandikishe nani walikuwa pale na kwa bahati nzuri wao wana *interest* ya kutaka washirikishwe tuweke alama gani za kumbukumbu katika maeneo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika napendekeza Wizara i-*champion agenda* hii ipeleke *AU* kusudi wakaweke *agenda* kwamba, waweke alama za kumbukumbu katika maeneo haya na sisi tuonekane tulifanya kitu gani katika suala hili la ukombozi. Tulimwaga damu na tumepoteza watu wetu. Naomba hilo Mheshimiwa Waziri, alichukue liwe ni *agenda*.

Akina Oliver Turnbo, Cisulu, Mtumbuka na Mandela, bahati nzuri wengi hawajafa na wengine bado wapo kwenye nchi zao na wana kumbukumbu hizi. Juzi nilipokwenda Zimbabwe kwa sababu ya mgogoro wa ardhi, baadhi ya wapigania uhuru waliokuwa wanakaa Nachingwea walisema bwana ile *farm 17* bado ipo kule, kama hawa wanaendelea kuleta fujo tutarudi tena kusudi tuanze tena kazi ya kukomboa ardhi yetu. Kwa hiyo, Watanzania tusitegemee mengine, sisi tuchangamke tubadilishe mambo haya ili historia isifutwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, tujenge *monument* ya Hayati Mwalimu Nyerere. Inasikitisha kwamba, tumezika kule mbali basi inakuwa hivi hivi tu. Ni rahisi kusahau historia. Tuweke alama za kumbukumbu watu wakija waone ni pale. Mimi nilikwenda kule Beijing wakati nikiwa Waziri wa Ulinzi, wakanipeleka kwenda ku-*pay respect* pale kwenye kaburi la Mao. Sasa sisi hapa katika haya mambo pamoja na kwamba tulimzika Mwalimu kule lakini tuangalie, tutazame njia *how best we can do it* kusudi pawe ni mahali pa kumbukumbu ambapo watu wataendelea kukumbuka historia. Ni rahisi kusahau historia. Watu wengine hawataelewa. Leo tukisema tuliwahi kutawaliwa vijana hawaelewi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, nilikuwa napendekeza kwamba, hii Kongwa ikiwezekana tufanye kama labda *Institution* fulani ambapo watu wote kutoka Afrika watakuwa wanakuja pale kusoma kusudi wajue historia. Kwenye *vision* yake katika Kitabu chake Mheshimiwa Waziri, ameeleza jambo zuri sana. Kwa sababu muda hauruhusu tazama ule ukurasa wa 17 katika ile *point* ya mwisho ya kwamba, tutumie jiografia yetu Watanzania ku-*maintain bonds* na wenzetu wanaotuzunguka. Jiografia ya Tanzania ni raslimali, ni mgodi mzuri ambao tungekuwa na akili timamu za kimapinduzi tungeendelea kuchota hawa watu wote wazidi kuja hapa. Wenzetu kule Kusini wanataka kujenga kituo pale Mpulungu uwanyang'anye biashara yote na kuua bandari ya Kigoma, Reli ya Kati na Bandari ya Dar es Salaam. Katika suala la uchumi huu ndio utekelezaji wa *vision* na *mission.....*

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kumalizika)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. GWASSA A. SEBABILI:** Mheshimiwa Naibu Spika, niruhusu nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia hoja hii iliyoko mbele yetu. Awali ya yote naomba kutamka kwamba, naiunga mkono hoja hii moja kwa moja. *(Makofi)*

Naomba nimshukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara husika na pia Mabalozi wetu popote walipo katika ulimwengu huu, kwa kazi nzuri ambayo wameifanya na hasa hasa ambayo imeandika historia mpya kabisa katika kipindi hiki cha miaka karibu mitatu tangu Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kusema kweli kazi ambayo imefanywa na Wizara hii katika kipindi hiki ni kubwa mno na inastahili pongezi na inaonekana katika nyanja mbalimbali hasa tunapofikiria jinsi ambavyo tumeweza kufutiwa madeni mengi kwa sababu ya propaganda zilizofanywa na Wizara hii na Mabalozi wetu nchi za nje. Pia jinsi uwekezaji ulivyoweza kushamiri zaidi kwa sababu wenzetu waliweza kufanya bidii zaidi kutangaza siasa yetu nzuri na sera zetu za uwekezaji ambazo ni za kuvutia. Vile vile jinsi tulivyoweza kupata misaada mingi ya kibinadamu, mikopo nafuu na hata mikopo ambayo tutaweza kupewa riba kubwa lakini kwa sababu njema ya maendeleo ya nchi yetu, imetupa nafasi kuwa na uwanja mzuri kwa Mikutano mingi ya Kimataifa, ambayo ni sehemu ya kujenga uchumi wetu kwa sababu watu hawa wanapokuja wanatuachia kitu katika nchi yetu. Katika hali hiyo tumewapa hata nafasi watu wetu kupata kazi katika mashirika mengi ya Kimataifa na ninafikiri kuliko ilivyowahi kutokea katika historia ya Tanzania tangu kupata uhuru. Kwa misingi hii na mingine, kwa kweli Wizara hii inastahili pongezi kwa kazi nzuri ambayo imefanya na tunawaomba waendelee kuongeza bidii ili heshima ya Tanzania iendelee kujengeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi iliyopo sasa kwa wakati huu ni Bunge kuishauri Serikali la kufanya. Haiwezekani kwa wale watu tunaotoka Magharibi ya nchi hii, tukazungumza lolote tusigusie suala la wakimbizi. Ilikuwa hivyo miaka ya nyuma kwa watu wanaotoka katika Mikoa ya Kusini na Mikoa ya Kusini Milimani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nafikiri kwamba, umefika wakati, sijui, ninasema kwamba, sijui, kama kwa kweli kuna sheria maalum kuhusu wakimbizi inayokuwa inatungwa na nchi moja moja katika ulimwengu wa sasa mbali na zile sheria za Jumuiya ya Kimataifa. Tunajua zipo *charters* nyingi, lakini kwa hali ya Tanzania ambayo imekuwa ikipokea Wakimbizi kwa zaidi ya miaka sitini leo kwa kumbukumbu zangu, nakumbuka kwamba, wakimbizi wa kwanza walioingia Wilayani Ngara kutoka Burundi ilikuwa ni mwaka wa 1946. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri kwamba, umefika wakati Serikali

ishauriwe au pengine kwa kushirikiana na Jumuiya ya Kimataifa, nchi ziweze kuwa na sheria ya kujilinda yenyewe, kuwalinda wakimbizi wanaoingia katika nchi yao na kulinda raia na mali zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kusema kweli vurugu ambayo imekuwa katika nchi yetu kwa miaka hii kumi tangu tatizo la Burundi la mwaka 1993, tatizo la Rwanda la mwaka 1994, imekuwa ni kubwa mno na vurugu hiyo imetupa matatizo makubwa sana, ni kero. Nafikiri kuna haja ya kuwa na sheria kwa sababu najua kama nchi kama Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo isingekuwa na sheria wakati wa vita yao na kambi kubwa za wakimbizi Goma, wakati wa vita ya Yugoslavia hasa Cosovo, Vietnam na kwingineko, ambako kama wasingekuwa na sheria watu wao wangekwisha na sisi watu wetu wanakwisha kwa sababu pengine hakuna sheria ya kutulinda. Nafikiri ni vizuri tukafanya kitu kama hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mporogomyi, amesema sana lakini nikumbushe kwamba, mwaka 2001 mwezi wa Nne, mimi sikuja hapa Bungeni kwa sababu tu nilikuwa katika kushiriki mazishi ya Watanzania wengi waliokuwa wakiuawa na Wakimbizi wa Burundi asubuhi na jioni. Tumeharibiwa mambo mengi, nchi imeletewa njaa, magonjwa ya binadamu na mifugo, imekuwa jangwa, wanyamapori wetu wamekwisha, nchi sasa imejaa silaha, ujambazi sasa umetoka mipakani huko tulipo umefika Dar es Salaam, hakuna mahali ambapo usalama upo kwa sababu ya wakimbizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili linatokana na masuala mengi tu. Kwanza, hawa watu walipokuja kwa ubinadamu na Katiba ya nchi yetu na Katiba ya Chama chetu cha Mapinduzi, tulifikiri wanakotokea mambo yangekuwa shwari na wakarudi haraka. Kwa bahati mbaya wakaingia mipakani wakajenga. Hawakuwekwa mahali pamoja wakatulia, walikuwa wamezagaa kila mahali katika nchi, waliruhusiwa kufanya biashara za ajabu ajabu, wengine sasa hivi ni matajiri kuliko hata Watanzania wenyewe kutokana na maliasili zetu ambazo wanapora na wanachafua. Kwa maana hiyo, mimi nilikuwa nafikiri niishauri Serikali kama kuna uwezekano na hakukuwa kuna sheria kuhusu wakimbizi kwa jumla yao, basi sasa wakati umefika wakimbizi watungiwe sheria au nchi itunge sheria za kulinda raia wake, mali zao na usalama wa mipaka yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo suala la kufikiria sana. Wilaya ya Ngara imepoteza watu wanaokadiriwa kama 40 hivi tangu wakimbizi wa Rwanda na Burundi waingie katika Wilaya ile. Hatuwezi kuzungumza habari za wizi wa mifugo, uharibifu wa mazingira, miundombinu, watu wakatishika wakashindwa kufanya kazi zao na jinsi ambavyo hata misaada inayotoka Serikalini tuliyokuwa tunaizungumza ya *TASAF* na nini tunavyoshindwa kuifanyia kazi kwa sababu watu hawana amani wala utulivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa hili kwa hasara ambazo zinahesabika, nategemea kwamba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anajibu hoja za Wabunge atatuambia hivi Serikali ya Tanzania haina haki ya kudai fidia kutoka kwa Jumuiya ya Kimataifa? Hasara zote zilizopatikana Mikoa minne imeguswa sana nayo ni Mkoa wa Kagera, Mkoa wa Kigoma, Mkoa wa Rukwa na sehemu ya Mkoa wa Tabora. Kwa Mikoa mingine kama Tabora, Kigoma na Kagera ni zaidi ya miaka 30 ya kupokea wakimbizi, tangu uhuru mpaka sasa hatujapata amani hata kidogo kwa sababu ya watu hawa. Nina hakika Serikali inajua haya na nina hakika Serikali inazijua hasara hizo na nina hakika Serikali inatunza kumbukumbu zake, hivi itakuwa hivi mpaka lini?

Kwa nini Serikali moja hii ipewe mzigo mkubwa, leo tuna wakimbizi zaidi ya laki saba katika Tanzania na ndiyo nchi pekee iliyo na wakimbizi wengi katika Bara la Afrika na ulimwengu mzima. Jumuiya ya Kimataifa inatufikiria nini? Naomba Mheshimiwa Waziri, atakapokuwa anajibu hoja basi atuambie sisi ndiyo Jumuiya ya Kimataifa, hatugawani hasara za namna hii, sisi tu ndiyo tunajua haki za binadamu na sisi tu ndiyo tuna huruma kwa watu ambao wanateswa na wanakimbia kutoka kila mahali? Naomba suala hili litazamwe katika hali yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kitu kinaitwa kinga ya Kibalozi. Shirika hili la Wakimbizi mahali pengi bila kujua kama walifanya hivyo kwa nia mbaya au vinginevyo, lakini kuna watu wameteseka au wamepoteza haki zao na watu hao wameshindwa kutimiza wajibu kwa raia wa nchi hii kwa sababu ya kusema wao wana kinga ya Kibalozi. Pale Ngara kuna watu waliokuwa wanafanya kazi katika *UNHCR* zaidi ya 32 ambao walifukuzwa kazi mwaka 1996 kwa muda wa saa sita tu na wanadai kati ya shilingi

milioni 40 na 50. Lakini Wizara imehangaika kiasi kikubwa sana, nawashukuru kwa kazi nzuri wanayoifanya lakini watu hawataki kulipwa. Kuna watu wameuawa katika kazi za Shirika hili kwa sababu ya wakimbizi, kuna watu wameuawa na wakimbizi. Matatizo yote kama haya tumeyaleta katika Serikali lakini Serikali haiyaoni? Inayaona na inayafanyia kazi lakini kizingiti ni kwamba, mashirika haya yana kinga ya Kibalozi. Kinga ya Kibalozi hata kwa kuua? Kinga ya Kibalozi hata kwa mtu kutoka jasho halafu asilipwe haki yake? Mimi naomba kabisa suala hili lifikiriwe na litazamwe katika hali yake ili wananchi wajue kwamba, Serikali yao inawalinda na wajue kwamba sheria za Kimataifa pia zinawalinda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la uvamizi wa ardhi sasa ambalo ameligusia Mheshimiwa Choya, Mbunge wa Biharamulo. Sisi tulioko mpakani tuna tatizo ambalo si dogo. Sasa hivi wakimbizi kutoka Rwanda na Burundi siyo kwamba sasa wanakimbia, wengine wanakuja kutafuta ardhi. Sasa limeingia suala la *East African Community*, maombi yao ni kwa sababu wao wamekuwa ni wengi wanataka mahali pa kupeleka watu wao. Nilikuwa nafikiri kwamba, Wizara hii inahusika ilitazame vilivyo, ilipeleleze inavyowezekana, iishauri Serikali namna ya kufanya ili kuondoa adha itakayoingia kama ile ya Palestina na Israel kama ile ya Australia na Aboligans sasa hivi wanavyonyukana ili tuweze kuokoa maisha ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sikuzoea kupigiwa kengele, naomba niseme tena kwamba naiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu kuzungumza. Kwanza kabisa, nitamke kwamba, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni kwamba, wazungumzaji wengi wameizungumzia hotuba kwa kuchambua maeneo mbalimbali kadri yalivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake amemsifu Rais wa Jamhuri kwa kazi nzuri anayoifanya ndani ya nchi na nje ya nchi. Mimi vile vile nakubaliana naye na nakubali kwamba, hata yeye anastahili pongezi kwa sababu na yeye ni mwakilishi kule. Maana katika nchi zingine hata ingekuwa Marekani au zingine, wanapomtaja Rais vile vile wanamtaja na Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na tunawasikia sana. Kwa hiyo, tunadhani na yeye anastahili pongezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kutokana na hotuba yake mimi nitachangia katika masuala mawili ambayo nitakuomba radhi na wale wengine kwa sababu mnaweza kudhani kwamba nayawasilisha si katika Wizara hii bali ni Wizara zingine, lakini hajayataja, kwa hiyo, nadhani nitalindwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, anasema alifanya ziara nchini Urusi na Mawaziri wengine walikwenda na akasema alipozungumza nao walikubaliana kwamba, watatuongezea nafasi za masomo na vijana wetu wakaenda kule. Wakaomba tuwauzie matunda, samaki, kamba, kahawa, chai, korosho na mengine.

Nadhani huu ni utaratibu mzuri ambapo sasa kama ni kwenda kwenye nchi hiyo na atakwenda kwenye nchi zingine, kama mfanyabiashara anazungumza na ana kitu cha kuwapa watu siyo kama ombaomba. Maana kuna watu wanaosafiri kama ombaomba tu. Sasa pale mimi nadhani amekwenda kama mtu ambaye anawakilisha Taifa lenye matatizo kwamba, kuna machungwa kule Tanga, kuna korosho kule Kusini na kuna chai havina soko. Sasa wakazungumza naye, kwa hiyo, mimi mwenyewe najisikia kama fisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku moja fisi alivamia kwenye nyumba ya jamaa kulikuwa na mtoto analia, sasa mama wa mtoto akamwambia mtoto anyamaze vinginevyo atafungua mlango na kumtupa nje halafu fisi akamtafune. Sasa mara ya kwanza aliposema hivyo, fisi mate yakamdondoka akakaribia mlangoni. Mara ya pili akamwambia mtoto anyamaze vinginevyo atamtupa nje halafu fisi akamtafune. Fisi akaganda pale kabisa. Mara ya tatu aliposema hivyo fisi alilala pale kwenye mlango mpaka asubuhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii alivyotuambia kwamba, amekutana na watu wanahitaji bidhaa zetu, ni suala la Wizara ya Ushirika la Masoko na Waheshimiwa Wabunge wanaotoka kwenye Mikoa inayolima

kahawa, chai na korosho na wafanyabiashara katika suala la samaki na wengine kumkaribia Mheshimiwa Waziri na kumwuliza hebu tuambie vizuri ili awafafanulie na wakubaliane kwa pamoja wapange programu. Sasa pale atawaambia hizo *opportunities* zilizokuwepo kule, ndiyo maana ya mpango huu. Kwa hiyo, ninapoyasema haya ni kwamba, mimi binafsi nimefurahia na nadhani watu wa Wizara ya Ushirika na Masoko na watu wa Wizara ya Kilimo na Chakula watamwuliza Mheshimiwa Waziri ili awape *details* waweze kufanya mkakati wa pamoja ili hii nia nzuri ya waliyomwita na wakazungumza juu ya mambo hayo inaweza ikatimia vipi. Kwa hiyo, kazi iliyo mbele yetu na wale wengine ni kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri amezungumza katika ukurasa wa 28 kifungu cha 51 na nitaomba ninukuu: "Kwa ajili hiyo Mheshimiwa Spika, nchi zetu haziwezi kuuza mazao ya kilimo wala ya mifugo katika nchi tajiri kwa sababu bei za wenzetu ziko chini kuliko zetu kwa sababu ya ruzuku. Kwa mfano, wafugaji wa nchi za Ulaya, Marekani, Japan wanapata ruzuku ya *USD* 3 mpaka 7 kwa ng'ombe kwa siku, wakati watu bilioni 1.5 duniani wanaishi kwa chini ya *USD* 1 kwa siku au watu bilioni 2.5 wanaishi kwa chini ya *USD* 2 kwa siku. Kwa jumla Mataifa tajiri ya Ulaya na Marekani yanatoa ruzuku ya *USD* bilioni moja kwa siku kwa wakulima wao."

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunajua kwamba, Viongozi wa Kimataifa wakishirikiana na viongozi wa nchi za Afrika bado iko sababu ya kujenga hoja za msingi kwenye majukwaa. Maana tunaweza tukapumbazika na kujenga hoja za kuwaita wawekezaji katika madini, wawekezaji katika Sekta za Viwanda, lakini tukasahau kwamba, nchi za Ulaya hizi ambazo zinatoa ruzuku kwa ng'ombe na kwa wakulima wao. Kwanza, wakulima wa Marekani ni wachache, wakulima wa Uingereza ni wachache lakini wanalisha Mataifa yale. Nilikuwa nasoma wakati nikiwa *form four*, kuhusu *Tennis Valley Authority* kwamba, wale wanalima pamba na wanatengeneza nguo, mabua yale yanakatwa katwa wanalishw a mifugo na vitu vingine. Kwa hiyo, kama ilivyo asilimia ndogo ya watu wa Marekani wanalisha nchi ile.

Sasa nasikia Mawaziri wa Biashara wa nchi za Afrika wanapokwenda kule kwenye *World Trade Organization* wananung'unika kwamba, ninyi mnawapa watu wenu ruzuku, sasa mnataka wawape nini funza. Kwamba, mnawapa ruzuku, mnataka wawape nini. Watu hao ni wachache na wanalisha Mataifa yale. Nyie kila siku mnapohesabu ni kwamba mmepunguza mfumuko wa bei, mnahesabu eti bei za vyakula kwa miaka mitano zilibaki pale pale, sasa bei za vyakula si mazao ya wakulima. Sasa zilibaki pale pale mnacheka wakati wafanyakazi mliwaongezea mishahara . *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nashangaa nasikia watu wanapiga kelele mmewapa ruzuku, sasa mnataka wawape nini na wakati ni wachache. Lakini sisi ambapo wakulima ni asilimia 80 na tunasema tunataka kuondoa umaskini wape ruzuku tunasema hatuna fedha. Kwa sababu hawawezi kuandamana na kwa sababu tunajua hata wasipozalisha tukiwapuuza kwanza hawataandamana na ni wajinga hawatatuondoa madarakani. Lakini la pili hata wasipolima tutakwenda kuombaomba mchele Ulaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hali kama hii, Mfaransa alikuwa anasema *cest le temps de chercher la verite qui conduire a la vie eternelle.* Ni wakati muhimu wa kutafuta ukweli uongozao katika maisha ya milele. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hii hotuba inavyosema najua kabisa anachokifanya Mheshimiwa Waziri, anapokwenda ni kiungo muhimu. Hata Uganda anakwenda Marekani, anakwenda Uchina anafanya *deal* jamani mimi nina ndizi au nina kahawa naomba mtanipa kiasi hiki sitaki kutaja siri zao hao watawaletea ndizi halafu tutahesabiana huku. Sasa sisi ukienda kule unakwenda kuomba mchele tu wakati Shinyanga wanaweza kulima, halafu mnautelekeza mnawapa shilingi 10 si vizuri. Kwa hiyo, ndicho tunachosema kwamba, wakati umefika wa kutafuta ukweli na tuutafute wote kama Taifa ili tuweze kuwasaidia hao watu asilimia 80 ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa katika hili wanatoa ruzuku na ameeleza hapa kwamba, nchi tajiri zinafanya hivyo na najua *agenda* ya Mataifa ya Afrika kwenda kuwanung'unikia kwamba, ninyi watu wenu mnawapa ruzuku, sisi haiwezekani. Lakini jana kulikuwa na maelezo hapa wametupa kuhusu *Coffee STABEX*, unatumia mgongo wa mtu unapata fedha halafu zile fedha zikifika unasema tukimpa hizi fedha ataelewa. Hivi mlevi anaweza kulima kahawa halafu ukauza wakakupa ruzuku! Tukimpa hizi fedha

atalewa. Sasa mlevi amelima kahawa yake tani 50,000 umeuza nje wamekupa bilioni 40, hebu mpe na yeye shilingi 10 unasema atalewa. Hivi mlevi analima tani 50, 000 za kahawa! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumetoa hapa takwimu kwamba, mwaka 1994 alipata shilingi 1,200/= na uchumi wetu tulikuwa tunakusanya sijui bilioni 25, mwaka huu unampa shilingi 50 na tunakusanya trilioni moja na nusu na mishahara imepanda kwa sababu tangu Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, aingie madarakani sijawahi kusikia kama kuna mwaka umepita bila kuwaongezea wafanyakazi mishahara japo mishahara hiyo haitoshi. Huwezi kumpa Hakimu wa Wilaya shilingi 80,000 /= halafu unacheka hazitoshi. Lakini wamekuwa wakiongezewa mishahara angalau. Sasa huyu mkulima fedha kwa kilo zinapungua, halafu unacheka, unasema tukimpa hizi fedha atalewa, analewa nini? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninachotaka kusisitiza hapa ni kwamba, wakati umefika tufanye maamuzi sahihi na tutumie Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na tutumie Mabalozi wetu, ametaja hapa Mabalozi wanaokaa nje, kila Balozi aulizwe wewe umefanya nini? Mwingine atasema tumeleta taarifa za usalama, sasa taarifa za usalama Marekani wanataka kuvamia. Ulitafuta soko wapi, umeandika maelezo yapi, unaunganisha nini na nini kwa sababu *we have to produce and we have to sale*, sasa huna cha kuzalisha na huna cha kuuza. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tutakuwa tunapata shida. Kwa hiyo, ninachotaka kusema ni kwamba, katika hoja wanazozipeleka kwenye Mkutano wa *World Trade Organization* na kwenye Mikutano ya Kimataifa hauwezi kuwafyonza wenzako na yapo mambo ya msingi. Nanukuu kitabu kimoja cha Baba wa Taifa kimeandikwa Tanzania Tanzania anasema mle ndani: 'Yako mambo ya msingi hata ungeliyapinga ufe, kuyapinga ni lazima kitabu cha mashairi na akasema wengi wape." Sasa wengi wape kama wanataka kumuua mama yako, wewe ununua kamba unawapa kwamba mnyonge hupingi. Sasa tunachosema hapa ni kwamba, hawa watu haiwezekani kikombe cha chai pale London ilivyokuwa mwaka 1994 sasa hivi imepanda kikombe cha kahawa hakijapungua. Marekani hivyo hivyo, Canada hivyo hivyo, kikombe cha chai au cha kahawa. Halafu leo hii unakuja wewe hapa kwenye soko unampa shilingi 10 sasa huu ni wizi na ni dhuluma.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa yapo Mashirika kule Marekani, Uingereza yame-*argue, OXFAM* Uingereza wame-*argue* kwamba, sisi hapa hatuwezi kuwanyonya watu, tunakunywa kahawa hapa asubuhi tunawanyonya tuwapeni hawa watu *STABEX*. Halafu anajua akizipitisha hizo fedha huku kwenye utafiti atapata mrahaba na atapata gari nzuri. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unawapa watu fedha wafanye utafiti wakati kahawa inakosa soko. Wakati tuna UKIMWI hapa Serikali haijawahi kutoa hata shilingi bilioni 2 kukipa Chuo cha Muhimbili au *University* yoyote ifanye utafiti wa dawa ya kutibu UKIMWI, shilingi bilioni 2 hakuna. Halafu leo unasema tunawapa fedha watafiti kuhusu kahawa bora tumewapa shilingi bilioni 12, *are you serious!*

Mheshimiwa Naibu Spika, *if we have to be serious* sasa, wao ambacho hawataki kwa mfano, kama watu walizalisha kilo milioni 60 au tuseme wamezalisha kilo milioni moja na nusu na fedha unazomlipa ni shilingi milioni moja na nusu. Lakini gharama za kuzalisha ni shilingi milioni mbili na laki mbili. Hata ukimpa mbegu bora atazalisha kilo milioni tatu, lakini gharama ikiwa ni shilingi milioni nne na nusu na ukampa bado shilingi milioni tatu atakuwa na upungufu lakini Serikali ndiyo itakayopata. Kwa sababu Serikali itaendelea kutoza kodi yake ambayo ni *fixed* na wakati mwingine inaongezeka ya shilingi 50/=. Kwa hiyo, mahesabu haya hayahitaji uwe umemaliza darasa la saba ili kuyajua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, baada ya kusema hayo, nisije nikapigiwa kelele. Namshukuru Mheshimiwa Waziri, kwa jitihada alizozifanya kwenda kule na aendelee na wale wengine ambao tumesikia hivyo tumwulize ili tuone programu hiyo, ili tutakapokuja kwenye Bajeti nyingine tuseme kile ulichotudokeza kwamba, ulikwenda wakakunong'oneza watu wa Urusi hilo soko limepatikana, kwa sababu ile ni nchi kubwa na ina watu wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri, na naunga mkono hoja hii kwa mara ya pili. *(Makofi)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika na mimi niungane na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote, kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kipindi chote hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunamfahamu Mheshimiwa Jakaya Kikwete, kwa uwezo wake mkubwa wa kuchapa kazi. Kule Zanzibar aliwahi kuwa Naibu Katibu Mkuu, miaka ya 80 alifanya kazi nzuri sana kwa wakati huo. Kwa hiyo, tunamfahamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba vilevile nimpongeze Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, kwa kuweza kulirudisha jina la Tanzania vizuri. Nalisema hili kwa kutoa mfano, mwaka 1988 nilimwalika mfanyabiashara mmoja mkubwa sana kutoka Qatar alikuwa na nia ya kuwekeza katika Bandari ya Dar es Salaam kufanya *free port.* Alipofika akaleta wataalamu kama saba kufanya utafiti wa haraka haraka. Alipomaliza tukampeleka kwa Mheshimiwa Rais, akamwambia Mheshimiwa Rais, una nchi nzuri sana, lakini haijulikani badilisha sera zako tutawekeza ahsante sana. Akaondoka.

Alikuwa akitaka kuwekeza karibu bilioni 3 wakati huo, alikuwa ni mfanyabiashara mkubwa sana alikuwa anaitwa *Mameko Operation Panel Qatar.* Kwa hiyo, nchi ilikuwa haijulikani, sasa nchi inajulikana ni hatua nzuri sana inahitaji kuendelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ningependa Mheshimiwa Waziri, azungumzie kuhusu suala na *NEPAD*. Bado suala hili la *NEPAD* linaonekana ni suala zaidi la Nigeria na Afrika Kusini kuliko Mataifa mengine ya Afrika. Tuliwahi kwenda kwenye Mkutano kama *SADC* na *Pan African Parliaments,* Waheshimiwa Wabunge wengi wa nchi nyingi za Afrika wanalalamika kwamba, *NEPAD* haijulikani vizuri. Mimi nafikiri Wizara ingechukua hatua za kuwaelimisha Watanzania juu ya mpango mzima wa *NEPAD*, bado uelewa ni mdogo sana.

Tatu, Mheshimiwa Spika, nina rafiki yangu mmoja mcheza mpira wa zamani kule Chake Chake, alisema CCM itaendelea kutawala maisha, mimi sina tatizo na hilo. Tatizo langu moja tu, mwaka 1964 Marehemu Karume, Mwanamapinduzi, rafiki sana wa baba yangu, alisema Zanzibar hakutokuwa na uchaguzi mpaka baada ya miaka 60. Lakini tukawa na uchaguzi baada ya miaka 14. Sasa mambo haya ya Mungu tuyaache kama yalivyo tu sisi hatuna uwezo nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la msingi nafikiri na la muhimu sana na namshukuru sana Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, ni kuweka taratibu ambazo zitatuhakikishia Watanzania watakuwa na uwezo wa kuchagua Kiongozi wanayemtaka chini ya Tume Huru, chini ya Katiba iliyo nzuri, chini ya wafanyakazi walio waadilifu na uchaguzi ambao utakuwa huru na wa haki. Nani ataendelea kutawala, wananchi wa Tanzania wataamua. *(Makofi)*

Nne, Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake ukurasa wa 46 amesema kwamba, anajitahidi sana kumsukuma Katibu Mkuu wa *Commonwealth* ili aweze kutoa mchango wake kutokana na ahadi aliyoiweka ya kutekeleza Muafaka. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri, kwa hatua hiyo. Lakini Mheshimiwa Waziri, nina hakika Katibu Mkuu wa *Commonwealth* atakuuliza je, haya mambo yaliyokuwa hayahitaji fedha Mheshimiwa Jakaya Kikwete, kwa nini hamyatekelezi? Utakuwa huna jibu. Kwa nini huteui watu wawili, kwa nini Mheshimiwa Rais kaanzisha mwenyewe *Commission* yake yeye mwenyewe na ikapitisha sheria akaahidi kila mwezi atakutana nao mara moja. Huu ni mwezi wa tisa hajakutana nayo hii *Commission* hata hili linahitaji fedha za *Commonwealth! (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nasema kuna mambo yetu sisi wenyewe ya ndani tunahitaji kuyafanya na Muafaka namshukuru sana Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, aliusimamia kidete kwa nguvu zote. Kulikuwa na watu walikuwa wakiupinga kwa nguvu zote, lakini Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, akausimamia kwa nguvu zote, namshukuru sana na ninamwomba aendelee kabisa na juhudi hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu Bunge lako sasa lazima tufike mahali tuwe above politics. Kuna mambo ya kinchi tulipata dosari katika matukio ya tarehe 26 na 27 Januari, 2001 nchi

ikapata doa, tukakaa kitako kusema jamani tuondoe doa tulilolipata katika nchi yetu. Leo Mheshimiwa Rais wetu Benjamin Mkapa, anakwenda kila mahali anapata heshima, Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa akienda anakwenda kifua mbele, wenzake wakizungumza kuhusu migogoro, anawaambia sisi tumeitatua wenyewe, tunamsikia Mheshimiwa Jakaya Kikwete akisema hivyo. Haya mambo tunaweza kuyamaliza wenyewe na hiyo imetujengea heshima. Sasa haiwezekani Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wawaahidi Watanzania wote, wawaahidi walimwengu wote kwamba, sisi tutasimamia Muafaka huu kwa ukamilifu, halafu warudi na kauli zao, hatutoeleweka. Heshima ya nchi haitokuwepo, tusizungumze mambo ya kisiasa kisiasa hayatusaidii na heshima ya nchi itakuwa haipo. Kwa hiyo, naomba sana wakati wa kuutekeleza Muafaka kikamilifu umefika na utekelezwe ili nchi yetu ijenge heshima yake.

Tano, ni suala la *International Criminal Courts.* Bahati mbaya katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, haikuelezea kabisa kuhusu suala hili. Mimi ningependa niliseme kwamba, moja katika matatizo ambayo dunia sasa hivi inayakabili ni suala la ugaidi na masuala mengineyo. Lakini vilevile lipo tatizo la kuanzishwa kwa hii Mahakama ya Kimataifa ambapo baadhi ya nchi ambazo zimeridhia hapo mapema sasa zinafanya kampeni ili watu wake wasiweze kushtakiwa katika Mahakama ya Kimataifa. Tungependa kupata *position* ya nchi yetu juu ya suala hili. Je, tupo miongoni mwa nchi zile zinazoghiribiwa ili hao ambao hawataki raia wake washtakiwe kwenye Mahakama hiyo tuwaunge mkono. Nini msimamo wetu juu ya jambo hili? Ningeomba Mheshimiwa Waziri, utupe msimamo wa nchi yetu. *(Makofi)*

Sita, Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Freeman Mbowe, alizungumzia suala la urari wa biashara baina ya *South Africa,* Tanzania na nchi nyinginezo na akaomba uwezo uongezwe katika Balozi zetu ili ziweze kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, *AU* tunaagiza bidhaa kutoka kwao zenye thamani ya shilingi milioni 95 kwa mujibu wa ripoti ya Benki Kuu, sisi hatujasafirisha kitu isipokuwa mwaka 2001 kidogo tulipeleka kama shilingi milioni saba. Nasema bado Tanzania hatujaweza kufungua masoko ya ziada ukiyaacha yale ya *Europe* na hii ni kasoro kubwa sana tunayoifanya. Wengine tulikuwa tunahisia tu za Uarabu na kadhalika. Lakini ukitazama Mataifa ya Magharibi yameweza ku-*tape* uchumi wa nchi za *Gulf* kwa asilimia kubwa sana. Tokea kwa kuwauzia silaha, kuchukua mafuta yao na kuwapelekea bidhaa zao. Sisi tumekuwa waoga tu bila sababu yoyote ile ya kutumia masoko haya. Kwa hiyo, ningemwomba Mheshimiwa Waziri katika mambo ya ushirikiano suala hili lazima tulitazame kwa undani zaidi.

Lakini la pili, ni aina ya bidhaa tunazoletewa. Sasa hivi wenzetu wa *South Africa* kwenye Makampuni haya ambayo wanayo hata ile *toilet paper* ambayo inapatikana hapa Tanzania pia inatoka kwao, imefikia mahali hata watumishi wa kawaida pia wanatoka kwao. Tulipokuwa *South Africa* tuliwauliza baadhi ya Waheshimiwa Wabunge juu ya sera zao. Wakasema ukitaka kuwekeza *South Africa* lazima uwe ni mzaliwa mweusi na upate asilimia 30 ya hicho unachotaka kuwekeza na wewe mwekezaji lazima ukamsaidie yeye kupata. Mbali na kwamba wanazo benki zao wao wenyewe za Serikali zinazosaidia. Katika *employments* asilimia 50 lazima Kampuni yoyote iajiri Mwafrika. Sasa kweli tupo katika utandawazi, nakubali kabisa tuko kwenye utandawazi. Lakini utandawazi una *stage* mbili, kuna *stage* ya kuogelea na *stage* ya kuoga. Wakati wa kuogelea kuna baadhi ya nguo unabakisha, wakati unaoga unavua nguo zote. Nafikiri lazima twende ile *stage* ya kwanza ya kuogelea. *(Makofi Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu wa *South Africa* wakienda Kenya hawahitaji *Visa*, lakini sisi tunahangaika sana na mambo ya *Visa,* pengine wakati umefika sasa wa kuangalia mazingira ya watu wengi wanaoweza kufanya biashara na ku-*move freely* ili kuweza kufanya kazi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine kwa sababu ya muda ni suala la *Pan African Parliaments* na *SADC Parliaments*. Mheshimiwa Waziri ni vizuri akatueleza juu ya gharama za kuendesha vyombo hivi pamoja na *East African Parliaments.* Kwa sababu itafika mahali nchi itakuwa haina uwezo wa kuchangia katika vyombo hivi na vinakuwa *real effective.* Kwa hiyo, ni vizuri vilevile tukapata *position* ya Serikali juu ya kuanzishwa kwa *SADC Parliament* na *Pan African Parliaments* na sasa hivi tunayo *East African Parliament,* gharama zake na uwezo wetu katika kufanyia kazi na kuviendesha vyombo hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala la watumishi wa Wizara, inaelekea *seniority* haitazamwi tena sasa hivi kwenye Wizara na ndiyo maana kuna watu wanakaa muda mrefu katika nafasi moja na wangetegemea pengine wangeweza angalau kupelekwa katika Ubalozi. Lakini bado tunaendelea na utaratibu ule ule wa kuchukua Mabalozi wa kisiasa. *(Makofi)*

Tuko kwenye utandawazi, hivi sasa pita kwenye Makampuni mengi ya kigeni yameajiri watu wasio Watanzania ni kwa sababu ya uwezo. Lakini ni kwa sababu vilevile tumesomesha watu wachache sana ukilinganisha na wenzetu. Sasa ni vizuri watu wetu tulionao vilevile nao tuwape moyo wa kufanya kazi. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri katika suala la kuongeza uwezo wa wafanyakazi wetu, ni kuwapa nafasi wale vijana ambao wako Wizarani na wamekaa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni matatizo ya Zanzibar na Muungano. Haya matatizo yamezungumzwa toka wakati tuko Chama kimoja na tumekuwa tunaendelea nayo kama hadithi kila siku. Sasa mimi nafikiri tunayo mihimili mitatu ya Serikali, tuna *Executive, Judiciary* na tuna *Parliament* na kila chombo kimoja kina wajibu wake katika kufanya kazi. Mimi nafikiri wakati umefika wa Bunge kuzi-*address properly* hizi *issues, otherwise* tutakuwa tuna-*postpone* kila siku na kila siku tunakuja kwenye Bunge, kwa sababu hatutaki kuli-*address properly*. Nashauri Kamati yetu ya Kudumu ya Mambo ya Nje, i-*short list* haya matatizo, yale ambayo yako ndani ya uwezo wa Bunge kuweza kuyatatua tuyatatue, hatuwezi kuja hapa kila siku tunaingia kwenye *globalization,* sisi wenyewe ndani tuna mgogoro tutaingiaje kwenye utandawazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi naomba hili suala tusifanye mchezo nalo. Muungano umebaki kwa muda wa miaka 40 sasa, hatupaswi kuwa na matatizo haya madogo madogo tena. Tumeshatoka huko hebu tutoke sasa tutumie na *Institution* ya Bunge kulimaliza hili tatizo. Tutamsaidia sana Mheshimiwa Rais Benjamini William Mkapa, aliyeahidi kwamba, atamaliza matatizo haya katika kipindi cha miezi sita. Tulielewa ni magumu sana hayawezekani kwa miezi sita kumalizika. Kwa hiyo, nafikiri njia moja ya kumsaidia ni kulishirikisha Bunge kikamilifu, tukatazama yale ya muda mrefu na yale ya muda mfupi tukayatatua ili tuingie kwenye *East African Community* tukiwa na kauli hii moja, tuingie kwenye *SADC* tukiwa na kauli moja, tuingie kwenye *Pan African Parliament*, tukiwa na kauli moja, tuingie kwenye *UN* tuwe na kauli moja. Hatuwezi kuendelea na matatizo tukayafuga kila siku ni aibu sana. Tanzania tuna uwezo wa kutatua matatizo yetu, hatuna sababu ya kuja hapa Bungeni kubishana kwa mambo ambayo si ya Kitaifa, hakuna sababu hata kidogo, tunao uwezo huo. Mimi nafikiri tutumie busara tulizonazo tulimalize hili tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, namwomba Mheshimiwa Waziri, kwa kutumia upande huu wa *East Africa, Community,* tuifanye Zanzibar iwe *free zone* au *free port* yote ili tuondokane na matatizo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. OMAR MJAKA ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hotuba hii kwa asilimia kwa mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ndio kioo cha Taifa letu nje ya nchi yetu hii ya Tanzania. Kwa dhana hiyo basi, nachukua fursa hii kumpongeza sana sana Mheshimiwa Waziri pamoja na wahusika wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio mazuri tuliyonayo kisiasa, kiuchumi na kimaendeleo ndani na nje ya nchi yetu yamefanikiwa kwa kiasi kikubwa na juhudi, uwezo na usimamizi imara wa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Taifa letu linaheshimika vizuri sana sana nje na ninampongeza Mheshimiwa Waziri na pia ninamtakia aendelee na kazi vizuri na kuimarisha umoja, mashirikiano na upendo kwa wafanyakazi wote ndani ya Wizara yake hiyo ambayo pia kwa uchumi wa dunia ya leo ndiyo muhimu sana kwa nchi yetu ambayo inahitaji uhusiano mzuri nje ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa kumi na tisa wa hotuba ya Waziri, limmelezewa suala la ugaidi. Nachukua fursa hii kumpongeza sana kwa kujenga mazingira ya kutokuwepo na shutuma ya nchi yetu nje kuhusiana na suala la ugaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nachukua fursa hii kuwapongeza sana sana kwa upendo na utukufu wao kwa Serikali yao na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninalisema hili kwani wakati tulipokuwa tunapitisha Muswada wa kupambana na ugaidi, palizungumzwa mengi, jambo ambalo lilijenga hofu kwa wananchi wetu wa madhehebu mbalimbali ya dini hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali laizma iwashukuru Watanzania kwa uvumilivu wao na kwa kweli wameona kuwa Serikali yao haikuwa na nia ya kugandamiza dini yoyote hapa nchini na wala haikuwa na dhana yoyote kuwa ugaidi unahusiana na waumini wa dini fulani hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa ishirini na moja unaelezea kuhusu maendeleo duniani. Ninanukuu Mheshimiwa Waziri amesema kuwa: "Hali ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii duniani ni suala kubwa na *agenda* muhimu katika mikutano mbalimbali ya Kimataifa. Maendeleo ni suala la msingi kwa Taifa letu na kwa watu wetu wote nchini. Kwa hiyo, nazidi kuishauri Serikai kwa suala hili lisilifanyiwe mzaha hata kidogo. Watanzania tunahitaji maendeleo ya kweli ndani ya karne hii ya 21, ambayo uchumi wake ni wa sayansi na teknolojia. Suala la elimu lazima lisimamiwe vilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo mnalo Wizara hii inisaidie ni juu ya suala la mafuta ya Zanzibar. Ninanukuu Gazeti la Uhuru 16 Julai, 2003 lililoandika habari kutoka Baraza la Wawakilishi. Kuna sehemu imeandikwa "Serikali bado haijaridhia suala la uchimbaji mafuta Visiwani. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema bado haijaridhia suala la uchimbaji na utafutaji wa mafuta katika Kisiwa cha Unguja na Pemba na kusisitiza hakuna kampuni ya kigeni inayoendesha kazi hiyo kwa sasa. Bado tunafikiria uwezekano wa kuliondoa suala la mafuta katika orodha ya Muungano. Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na wataalam mbalimbali katika Kisiwa cha Pemba, yapo mafuta mengi Vitongoji wakati kwa upande wa Unguja ni rasi ya Chwaka".

Mafuta hayo yanaweza kabisa kutosheleza mahitaji ya matumizi ya ndani na kusafirisha mengine nje ya nchi na kuingiza fedha za kigeni. Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje ninamwamini sana sana, kwa ukweli na juhudi zake, ninamwomba hasa kwa vile aliwahi kuwa Waziri wa Nishati na pia kwa vile bado yupo Serikalini na pia kwa kuwa tulipokuwa katika Semina moja Dar es Salaam, niliwahi kuulizia uundwaji wa Tume ya Pamoja ya fedha ya Muungano ambapo alinijibu vizuri na Tume hiyo hivi sasa imeshaundwa. Ninaomba ukweli wa suala hili la mafuta. Mimi Vitongoji ni kwetu kwa kuzaliwa na pia hivi sasa ni Mbunge. Naomba maelezo ya hili kwa usahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono kwa asilimia 100.

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Nampongeza Waziri na Naibu Waziri, pamoja na wataalam wote wa Wizara. Naipongeza Wizara kwa uwajibikaji mzuri katika Sekta ya Itifaki, kwa upande wangu naridhika sana kwani nahisi bado tunakwenda sambamba na ulimwengu, lakini bado nashauri mafunzo zaidi yatiliwe mkazo kwa kizazi kipya, kwani mtazamo wangu halisi walio wengi ni wazoefu wa siku nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Wizara hii pamoja na shughuli zake nyingi za kidiplomasia, isaidie nchi yetu kuitangaza nje kiuchumi katika nyanja tofauti. Aidha, naomba sana Wizara hii kukiangalia sana kwa kukiboresha Kituo cha *AICC* kwa kukirekebisha kulingana na mahitaji ya kidunia kwani kituo hiki ni muhimu kwa Watanzania na kinatuletea sifa kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii lazima isimame kidete kutetea maslahi ya nchi katika propaganda za kigaidi kwani imebainika yapo mashinikizo ya makusudi kuharibu sifa za nchi kupitia propaganda za ugaidi, hivyo Wizara iwe nyepesi kujibu hoja, lakini pia huku ikiangalia usalama wa wageni na mali zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naishauri Wizara hii iwashughulikie raia wetu ambao pasina kutokujua na tamaa zao, wamejipeleka *DRC* kijeshi na hivi sasa wanasumbuka, naomba warejeshwe nyumbani na kupatiwa elimu ya uraia. Ahsante.

**MHE. AZIZA SLEYUM ALLY:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia. Nachukua nafasi hii kuwapongeza Waziri na Naibu Waziri, kwa kazi nzuri za juhudi wanazofanya kwani ni kazi nyingi ngumu ambazo wanafanya kwa niaba ya wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na juhudi zao, yapo mafanikio mengi sana ambayo tunayafahamu na yanaonekana kwa umma, tunashukuru sana. Naomba kuchangia maeneo machache tu kutokana na hotuba ya Waziri ilivyojitosheleza yenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na utaratibu wa kisiasa, wawakilishi wetu wa nje ya nchi, yaani Mabalozi, tunamshukuru Rais kumteua Balozi mmoja wa kike mpaka sasa, kwani inaonyesha mwanzo mzuri umefikiriwa hadi sasa. Uwepo uteuzi wa nyongeza kwa Mabalozi (Wanawake) kwani baada ya moja, mbili na tano. Nina imani hayo yako mbioni na yatazingatia uwezo na pia hata umri. Kwani vijana wa kike pia wa kiume wapo wanao uwezo wa kuwa wawakilishi, tuna imani nao kwani kutokana na nchi yetu yenye maadili na Uongozi wa Chama Cha Mapinduzi unavyolea vijana kwa utaratibu mzuri na imani wapo na wanatosha,

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iweze kuwasiliana na Balozi ambazo zinatoa *Visa* kwa usumbufu mfano, Amerika/UK kwani kuna usumbufu mkubwa sana kwa wanaotaka *Visa* hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wema usizidi uwezo. Nafikiri sasa imetosha kwa hawa wakimbizi kurudi makwao na kuwa na utulivu ndani ya nchi zao kwani watakaporudi ndio mwanzo wa kujifunza kuanza amani (usemi usemao mzigo mzito apewe Mnyamwezi), sasa Wanyamwezi tumechoka kubeba wakimbizi hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutumia Wizara hii kama itafanya utaratibu mzima wa kutangaza utalii, nina imani tutapata watalii wengi zaidi na kuwaleta ndani ya nchi yetu ili kukuza pato la nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, natamka rasmi naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. JUMA A. KAPUYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naunga mkono hoja kwa asilimia 100. Pili, nimempa Balozi wa Urusi mpango wa kuendeleza soka Tanzania, hususan timu za wanaume za wakubwa na watoto. Naomba Wizara yako itusaidie kuzungumza na Balozi huyu umuhimu wa msaada huo kwa Watanzania. Tatu, naomba masuala ya kusaidiana na Wizara ya Kazi na pia *NGOs* za ndani ya nchi yetu katika kuwatafutia vijana wetu kazi nje ya nchi yapewe kipaumbele. Wenzetu wa Kenya, Uganda, Msumbiji, wanafaidika sana na nguvu hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nampongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake, kwa hotuba yao nzuri.

**MHE. LEONARD N. DEREFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naunga hoja mkono hoja kwa asilimia 100. Nawatakia utekelezaji mwema wa malengo mliojiwekea kwa Bajeti ya 2003/2004. Naomba kutoa ushauri ufuatao:-

- Mara nyingi Wizara yako ikiandikiwa barua huwa haijibu. Mimi nimewahi kuandika barua kwa Wizara yako kuhusu kijana aliyenyanyaswa na *WFP* - Isaka sikuwahi kupata jibu. Huu si utaratibu mzuri, watendaji wako wa ofisi siyo makini. Utaratibu mzuri wa ofisi ni kujibu barua zinazoandikwa na wananchi kwa Wizara. Ni vyema Wizara ikarekebisha.

- Yapo mashirika ya hadhi ya Kibalozi yanapofanya makosa inahitajika kibali kitolewe na Wizara yako lakini malalamiko ya wananchi hayashughulikiwi ipasavyo.

- Katika Balozi zetu nchi za nje, mara nyingi Wizara hulipa mishahara tu pasipo kutoa fedha za kuwafanya watende kazi zao kwa ufanisi. *Embassy* yetu kule India na China haipewi fedha za kutosha kuwawezesha kutenda kazi zao kutokana na umuhimu wa *Embassy* hizo kutokana na idadi kubwa ya watu na umuhimu wao kiuchumi duniani.

- Pale New Delhi, Serikali ya India ilitupatia kiwanja cha kujenga ofisi lakini hadi sasa kiwanja hicho hakijajengwa. Sehemu iliyoko Ofisi ya Ubalozi haina hadhi ya Kibalozi ingawa makazi ya Balozi ni safi sana. Ni vyema Serikali ikaona namna gani itaweza kupata fedha za kujenga jengo lake huko India.

- Kutokana na umuhimu wa India kibiashara ni busara kwa Wizara kupeleka mtendaji aliyebobea kibiashara kuwa Afisa Biashara katika Balozi hii.

- Nchi kama Ivory Coast (Cote'devoir) Sierraleone na Liberia, ambazo zilikuwa nchi zenye amani kwa muda mrefu na ni kitu gani kiliwafikisha walipo sasa na kuwa na vurugu kubwa. Ni vyema Tanzania ikafanya utafiti na kujifunza makosa waliyofanya na kuwafikisha katika vurugu hizo! Mtu mwerevu hujifunza kwa makosa ya wengine na siyo kujifunza kwa makosa yako!

- Kwa nchi nyingi zilizo na vurugu zilianza kwa kuwa na viongozi wao. Ona nchi za Liberia, Sierraleone, *DRC*, Rwanda, Burundi, Ethiopia, Uganda na kadhalika. Hata waliofukuza viongozi wao kama Somalia, Ghana na kadhalika. Hata Zanzibar wakati mwingine damu ya marehemu Karume huwa inawapata kama vurugu za *CUF*, Lazima tujifunze kuwahamasisha viongozi wetu. Kuwa viongozi mjue mmejiletea matatizo makubwa. Tanzania tuna bahati hatujamwaga damu, huwa tunamwaga machozi viongozi wanapofariki kwa amri ya Mwenyezi Mungu. Tuendeleze utaratibu wa kuwaenzi viongozi wetu wakubwa kwa amani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. HAJI MWITA HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Viongozi wenzao wa Wizara hii kwa juhudi zao za dhati za kufanikisha shughuli za Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Nina amini sana juhudi zao ndio msingi wa mafanikio ya kuiweka nchi yetu ya Tanzania kuwa ya heshima kubwa chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, kama heshima hii ilipoanzishwa na Baba wa Taifa Mwalimu Julius K. Nyerere.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania imekuwa ikifurahia amani na utulivu wake kwa muda wote kutokana na siasa zake na hulka ya watu wake tokea asili na jadi na ukarimu wake na jirani zake au nchi zote duniani. Hali hii imetupatia sifa, heshima na uaminifu mkubwa kwa ulimwengu huu na hasa katika nchi za Maziwa Makuu na majirani zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeridhika sana na maelezo ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri, hotuba ambayo kadri ya uwezo wake imetueleza mafanikio na maendeleo yanayotokana na Wizara hii pamoja na maendeleo ya amani na utulivu wa nchi yetu hii. Ninaiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. Hata hivyo, ninayo mambo machache ya kuchangia na kutaka maelezo wakati Mheshimiwa Waziri, atakapokuja kufanya majumuisho yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni baada ya kusikia kuugua vibaya kwa Nduli Iddi Amini Dada huko uhamishoni Saudi Arabia na kuwa ikiwa atarudi nchini Uganda akiwa hai, hata ikiwa kwa kungojea ahadi yake ya kufa, atakabiliwa na mashtaka ya uhalifu wa nchi hiyo aliofanya wakati wa utawala wake, hali ambayo ilituweka Tanzania katika hali mbaya sana ya usalama na uchumi wa nchi yetu Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hali hii tukasikia zaidi kuwa mtoto wa Nduli Iddi Amini Dada, ambaye yuko nje ya nchi ya Uganda anajitayarisha na uvamizi wa nchi ya Uganda ambayo ni jirani zetu wema na vile vile ni nchi mwenza katika Shirika letu la Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikiwa hali hii ni kweli au ikiwa lisemwalo liko au kama haliko linakuja, je, suala hili ikiwa bado ni mapema analiambiaje Bunge lako Tukufu na wananchi wa Tanzania juu ya taarifa hizi hasa tukizingatia kuwa Tanzania yetu kuwa nyota inayong'ara isije ikatiwa giza na vitendo vya wasiopenda maendeleo ya dunia yetu hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya tahadhari hii na kutaka kupata maelezo japo kidogo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, kwa imani yangu yote ninaiunga mkono hotuba hii kwa asilia mia kwa mia. Ahsante.

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Aidha, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote walioshiriki katika kuandaa hotuba hii kwa makini na umahiri mkubwa sana. Hongera sana.

Nampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa jitihada zake za kulitafutia jawabu la kudumu matatizo ya mpaka kati yetu na Malawi. Tatizo hilo sasa litakwisha baada ya kufungua Ubalozi na Malawi. Nashauri sasa mikakati iwekwe kuhakikisha kwamba, wananchi wa Malawi wajione kuwa wao ni sehemu ya Tanzania, kijamii, kiuchumi na kimazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuendelea kuwepo kwa Ziwa Nyasa kunategemea kwa kiasi kikubwa mipango endelevu ya matumizi ya ardhi upande wa Tanzania kwa sababu ya ukweli kwamba, zaidi ya asilimia 50 ya maji yanayoingia katika Ziwa Nyasa yanatoka Tanzania. Tayari hali imeanza kuonyesha kuwa Wilaya za Makete na Mbinga zina matumizi ambayo yameanza kuathiri biolojia ya Ziwa hilo. Ufumbuzi wa tatizo hilo ni kukubali matumizi ya pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara kwa kuimarisha mahusiano yetu na nchi jirani. Kuwepo kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki ni mfano mzuri. Hata hivyo, Mtanzania anayeishi Kusini mwa Tanzania haelewi kwa nini hakuna mahusiano rasmi kati ya wananchi wa Kaskazini mwa Msumbiji na Malawi. Je, Serikali inazo taarifa kwamba, mahusiano yasiyo rasmi kati ya nchi hizo yanazikosesha mapato nchi hizo na hasa Tanzania. Ushirikiano wa watu kwa watu ni endelevu zaidi kuliko ule ushirikiano wa Serikali na Serikali, hasa ngazi za juu peke yake. Athari za ushirikiano kwa viongozi ni kwamba pale wanapotofautiana, basi mfumo mzima wa ushirikiano unayumba au kuvunjika.

Tanzania inazungukwa na nchi nane, Wizara haina wawakilishi wataalam nje ya Makao Makuu yasiyo rasmi, Dar es Salaam badala ya Dodoma. Nashauri Wizara hii iangalie uwezekano wa kuwa na Ofisi za Ushirikiano wa Kimataifa katika Mikoa ya pembezoni ili kuondoa urasimu ambao unafanya watu wa mipakani wasiwe na mahusiano rasmi hadi wapate kibali au idhini Makao Makuu Dar es Salaam.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, pongezi zinatolewa kwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, *DAP* na Wakuu wa Idara wa Wizara. Hongera kwa kazi nzuri za kuitangaza Tanzania.

Pili, Wizara ina mpango gani katika suala zima la kujenga nyumba zetu kwa Mabalozi wetu nchi za nje.

Tatu, hivi katika hali ya teknolojia ya Mawasiliano, kuna haja ya msingi ya kuwa na wachumi katika uwakilishi wa Balozi? Mimi nafikiri, chini ya mfumo wa *Internet,* uchumi wa kila mtu uko ndani ya uwezo wa vidole vyake. *Website, Internet, FAX, Mobile phones,* zina mfumo tosha katika biashara.

Je, fungu la *hospitality* linatusaidiaje katika kufanya *lobbying* za ndani na nje ya nchi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna vigezo gani vinavyovutia nchi kuweka ubalozi nchini Tanzania? Kuna vigezo gani kwa nchi yetu kuteua nchi ya kuweka Balozi zetu? Kuna nchi ngapi duniani ambazo zimevunja au tumevunja uhusiano na zipi katika hizo tumerudisha uhusiano wetu.

Afrika ilitawaliwa, ilichukuliwa baadhi ya raslimali, maliasili, watu na kadhalika, kudhoofisha nguvu za Bara hili la Afrika na kudumaza uchumi wa nchi zetu. Utumwa, Ukoloni, Ukoloni Mamboleo na kadhalika. Hii hali iliichakaza Afrika kuonekana kijeba kiuchumi ingawa ni kubwa kiumri. Afrika na Tanzania tunaungana na kauli yako nzito uliyoitoa *South Africa* kudai Afrika ifidiwe. Naomba maelezo.

**MHE. KILONTSI M. M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe maelezo ya nyongeza kama nilivyokwisha unga mkono hoja.

Balozi zetu nyeti kama ile ya Brussels, Geneva, London na Washington zipewe kipaumbele katika huduma mbalimbali. Kwa mfano, Ubalozi wetu wa Brussels, hawakuweza kuhudhuria Mkutano wa *ACP/EU* uliofanyika kule Brazzaville na mingine ya *SADC.* Natumaini utawawezesha wahudhurie kikao cha mwezi ujao huko Arusha. Serikali yetu lazima ifanye jitihada za makusudi ku-*develop sufficient capacity for analysis, planning, formulation and implementation of projects and management of aid.* Nchi za Magharibi hasa zile za *EU* zinasema hatuna uwezo wa kutumia fedha hizo. Ndiyo maana mpaka hivi sasa fedha za *EDFs - 6$^{th,}$ 7$^{th}$ and 8$^{th}$* bado hazijatumika na karibu tunaingia kwenye *9$^{th}$ EDF.* Tunaomba tupewe taarifa ya mazungumzo yanayoendelea katika *negotiations* zetu ndani ya *Economic Groupings* tuna mikataba nazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kuunga mkono hoja.

**MHE. BERNARD K. MEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza uniruhusu nitoe pongezi kubwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, kwa hotuba nzuri sana aliyoitoa leo mbele ya Bunge lako Tukufu. Nawapongeza pia Naibu Waziri na Maafisa wote wa Wizara, kwa kazi nzuri na nitanguliza mapema kuunga mkono hotuba hii.

Kazi kubwa iliyo mbele ya Wizara yetu ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na itakayoifanya nchi yetu ipate heshima ya kushirikishwa katika mambo mbalimbali katika Bara letu na hasa eneo la Ukanda wa Maziwa Makubwa, ni kazi ya kutafuta amani ya kudumu kwa kuzuia na kutatua migogoro. Kwangu mimi, suala hili si la mikakati, ni la *Principle.* Kutafuta ufumbuzi wa migogoro ya nchi zinazotuzunguka iwe ni moja ya *pillars* au *principles* za siasa au Sera Mpya ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Ni vyema kukawa na Idara maalum Wizarani inayoongozwa na Balozi aliyebobea katika mambo haya na kuwe na timu ya wataalam wa *conflicts* watakaofanya kazi kwa uchambuzi na ufanisi wa hali ya juu. Kwa mazingira ya Tanzania, *Foreign Policy Principle* ya kutafuta ufumbuzi wa migogoro kwa njia ya amani, itaijengea heshima nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. ABDULLATIF H. ESMAIL:** Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kusema kwamba, ninaunga mkono hoja hii mia kwa mia. Vile vile napenda kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Dr. Abdullkader A. M. Shareef, Naibu Waziri, na Ndugu Phillemon Luhango, Katibu Mkuu, pamoja na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninazipongeza Balozi zetu kwa bidii wanazofanya kuitangaza nchi yetu, kiuchumi, kibiashara, utalii na kadhalika. Ninaipongeza Wizaa kununua jengo la Ofisi Rome (Italia), pamoja na nyumba ya kuishi, Pretoria *South Africa*, pamoja na magari kwa ajili ya Balozi mbalimbali ulimwenguni. Kwani, *appearances matters a lot.* Japo Waziri amesema kwamba, amani na utulivu vimeendelea kuwa bidhaa adimu duniani (ukurasa 7) lakini tushukuru Uongozi wetu wa Rais Benjamin William Mkapa (Bara), Rais Amani Abeid Karume (Zanzibar), umetuwezesha kuwa na amani na utulivu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhamira ya kufungua Ubalozi Oman na Malaysia ifuatwe, kwani nchi hizi kuna umuhimu mkubwa wa uwakilishi wetu, biashara na Watanzania wengi wanaishi nchi hizo.

Ziara ya Marais wetu ziongezwe ili waweze kutembelea nchi mbalimbali, wakaone wenzao na mipango yao ya maendeleo. *To travel is to learn as well as relax.* Ziara za Wizara hizi kwa mara zote zina uso wa Kimuungano, ninapongeza kwa jambo hili. Ninaipongeza Wizara kwa kufanya bidii Kiswahili kuingizwa na kuwa lugha rasmi Umoja wa Afrika.

Kuhusu wakimbizi, ningelishauri wawekwe kwenye kambi ndani ya nchi zao mipakani na sio katika ardhi ya Tanzania. Ninaishauri Wizara kuajiri watumishi wapya ili iwe na ufanisi zaidi, pamoja na kuwa na watumishi wenye ujuzi wa uchumi na biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja mia kwa mia. Ahsante sana.

**MHE: ALI SAID SALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Zanzibar ni nchi kama nchi nyingine duniani, ni vyema basi nafasi yake ikawekwa wazi katika Jumuiya hii. Ni vyema basi Zanzibar ikashirikishwa na kuwa na haki sawa kama zilivyo nchi nyingine za Afrika Mashariki. Pili, *OIC* ni moja katika Jumuiya zinazotoa misaada ya maendeleo, na kwa kuwa nchi yetu ni miongoni mwa nchi masikini duniani. Je, ni lini Serikali itaamua kujiunga na Jumuiya hii ili kujikwamua na umasikini wa kutupwa katika nchi yetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwa suala la ugaidi limekuwa ni tatizo la Kimataifa, lakini ni vyema kwa Serikali yetu ya Tanzania ilitizame suala hili kwa uangalifu mkubwa. Vinginevyo suala hili linaweza kuzusha balaa kubwa kwani tayari baadhi ya watu wanahisi kwamba Sheria ya Ugaidi imetungwa kwa ajili ya kuwakomoa watu wa dini fulani.

Nashukuru Wizara hii kwa kufanya mipango ya makusudi ili kupunguza tatizo la ajira katika nchi yetu kwa kuwatafutia ajira nje ya nchi Watanzania. Kwa kuwa diplomasia ya uchumi ni jambo gani katika nchi yetu, ni vyema Wizara ikaandaa utaratibu wa kutoa elimu kwa umma ili waweze kutumia na kuleta tija kwa Taifa.

**MHE. AGGREY D.J. MWANRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wote wa Jimbo langu la Siha napenda kumpongeza Mheshimiwa Jakaya M. Kikwete, Mbunge na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa hotuba nzuri na yenye uchambujzi wa kina ambayo imetolewa asubuhi hii ya leo. Naunga mkono hoja.

**MHE. FRANK M. MUSSATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Vile vile ninawapongeza Mheshimiwa Jakaya Kikwete, Waziri, Naibu wake, Mheshimiwa Dr. Shareef, Bwana Luhanjo, Katibu Mkuu, Mabalozi wote na wafanyakazi wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri waliyoifanya katika mwaka 2002/2003. Nawatakia kila la kheri kwa mwaka 2003/2004.

Ninaomba Wizara iangalie yafuatayo:-

(i) Nchi za *DRC* na Burundi ziko kwenye vita za wenyewe kwa wenyewe na nchi hizi ni Kiwanda cha kuzalisha wakimbizi ambao wanaendelea kufurika katika Mkoa wa Kigoma na kuleta athari nyingi kwa wakazi wa Mkoa huu. Serikali ikishirikiana na Jumuiya ya Kimataifa ifanye kila liwezekanalo kuleta amani katika nchi hizo ili wakimbizi warudi makwao mapema iwezakanavyo na wakazi wa Mkoa wa Kigoma waishi kwa amani na kuendelea na shughuli za maendeleo bila bughudha ya wakimbizi.

(ii) Nawapongeza wote waliohusika katika kufanikisha kuingiza lugha yetu Tukufu ya Kiswahili katika matumizi ya Kimataifa hususan katika AU. Serikali isimamie na kuhakikisha kwamba lugha yetu hii inaenziwa na kutumiwa katika Mikutano mingine hata nje ya AU.

(iii) Ninaomba Wizara hii ilitake Shirika la *UNHCR* linaloshughulikia wakimbizi kuwafuta machozi wakazi wa Mkoa wa Kigoma kwa kuimarisha miundombinu na kurejesha hali nzuri ya mazingira ambavyo vimeharibiwa na wakimbizi toka nchi jirani za *DRC* na Burundi. Aidha, wakazi wa Mkoa huu wameathirika kiulinzi na kiusalama kutokana na ujio wa wakimbizi. *UNHCR* ishirikiane na Mashirika

mengine kama *WFP* kujenga barabara za lami Mkoani Kigoma kama shukurani kwa Mkoa huu kupokea wakimbizi kwa zaidi ya miaka 30 hivi sasa. Ahsante.

**MHE. JEREMIAH J. MULYAMBATTE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia nafasi hii kukupongeza sana kwa hotuba yako nzuri yenye mwelekeo na upo wa hali ya juu. Nasema hongera sana. Pia nampongeza Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalamu wote wa Wizara hii.

Mchango wangu, naishauri Serikali kuhusu suala la kuimarisha na kuboresha Ofisi zetu za Ubalozi huko nje kwani aibu zinazotokana na Balozi zetu ni mbaya. Ofisi zetu hazikarabatiwi kwa muda mrefu. Wanafunzi wasomao nje ya nchi hupata shida kupata matumizi kwa wakati na hulazimika kukopa.

Mheshimiwa Naibu Spika, *VISA* kuna urasimu sana kitu ambacho huleta kero kwa wale wanaotaka kusafiri. Wizara ifanye marekebisho ya kuwa na utendaji wa moyo wa kujituma.

Mheshimiwa Naibu Spika, karadha na masurufu hayarejeshwi kwa wakati na kuonyesha kutokuwa na uaminifu upande wa matumizi ya fedha za Wizara. Naunga mkono hoja.

**MHE. MOHAMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu na wataalamu wao wote kwa pamoja kwa kuweza kukaa na kuandaa Bajeti yao hii ambayo inaonesha ufanisi wa hali ya juu kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lako hili Tukufu lilipitisha sheria kuhusu diplomatic passport kwa mke au mume wa Mheshimiwa Mbunge, lakini jambo la kushangaza jambo hili liliishia humu humu ndani ya Bunge lako Tukufu kwani hadi hii leo unapokwenda kwenye Ofisi za Uhamiaji imekuwa unaanzisha jambo jipya ambalo pale halijulikani kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikiwa sisi ndio tunaotunga sheria za nchi hii kwa kupitia Bunge lako hili Tukufu. Leo unafika kwenye Ofisi za Uhamiaji na kujiona kama hujui kazi yako!

Mheshimiwa Naibu Spika, Balozi zetu za nje ziimarishwe na kupewa nguvu za kiuwezo ili waweze kukabiliana na matatizo mbalimbali yanayowakabili pale wanapopata kesi za Watanzania walioko nje ya nchi kwa urahisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uteuzi wa Mabalozi ambao wanatuwakilisha nchi za nje, kwa upande wangu ningeliomba iongezwe idadi ya Mabalozi hasa kutoka upande wa pili wa Muungano Zanzibar ambako mpaka hivi sasa ni idadi ndogo sana tuliyopata katika kuiwakilisha nchi yetu hii hasa tukithamini kuwa yale yanayokwenda kufanywa yanahusu Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kuchukua uamuzi kwa makusudi ya kuwarejesha wakimbizi makwao kwani mzigo mkubwa tulioubeba kwa kuwahifadhi wakimbizi umetuletea matatizo mengi na kushamiri kwa ongezeko la silaha ambazo zimezagaa kila upande na kusababisha wizi na unyang'anyi kuongezeka kwa kasi kubwa hata kufikia hali ya kutisha kwani Askari akiwa na uniform tu anaweza kumiminiwa risasi bila ya yeye mwenyewe kujua kosa lake ni zile *uniform.*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo machache, napenda kuunga mkono hoja hii asilimia mia moja. Ahsante.

**MHE. MOHAMED A. ABDULAZIZ:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, sio siri kwamba ipo tofauti kubwa ya kiuchumi kati ya Mkoa na Mkoa. Zipo sababu nyingi, lakini moja ni kiwango cha misaada ambacho baadhi ya Mikoa inapata kutoka kwa Wafadhili mbalimbali wa nje ya nchi. Zipo taarifa kwamba Wahisani wa nje wanayo tabia ya kuchangia ni wapi waelekeze misaada yao. Nashauri Serikali na hasa Wizara ya Mambo ya Nje ijitahidi kuwaelimisha Wahisani wa nje kusambaza misaada yao katika nchi nzima ili kuepuka ujenzi wa matabaka ya kiuchumi hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la wakimbizi napenda kupongeza Wizara kwa juhudi za kidiplomasia inayozifanya ili kujenga misingi ya amani na utulivu katika nchi za jirani zenye migogoro ili kuwafanya waishi kwa amani na kupunguza wimbi la wakimbizi.

**MHE. ESHA H. STIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri Jakaya M. Kikwete kwa kazi zake nzuri za Kimataifa anazozifanya siku hadi siku na mafanikio yameonekana. Halikadhalika Naibu Waziri wake Mheshimiwa Dr. Abdulkader A. Shareef nawapongeza kwa kazi zao za kuliletea heshima Taifa letu. Kwa hiyo naunga mkono Bajeti yao 2003/2004 mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka ya huko nyuma niliwahi kuchangia hoja ya manyanyaso ya vijana wetu waendapo nchi za nje (kupigwa na kunyang'anywa mali zao) na Mheshimiwa Waziri aliahidi kufuatilia masuala hayo na nina hakika alifanya hivyo. Leo nachukua fursa hii tena kumjulisha Mheshmiwa Waziri kwamba bado mipaka ya nchi jirani vijana wetu wanafanyiwa vitendo vya ukatili.

Hivi karibuni June, 2003 kijana mmoja anaitwa Salumu alikuwa anakwenda Botswana kupitia Zambia na Zimbabwe. Kwa heshima kubwa Zambia walimpokea na kumgongea *VISA* yake na akaendelea na safari yake hadi Zimbabwe. Hapo Zimbabwe alipokelewa kwa mateso, hakuruhusiwa kupita kwenda Botswana bila sababu ya msingi, zaidi ya kashfa na kupigwa na kunyang'anywa fedha zake. Kijana huyo Salumu alirudi Tanzania, kwa msaada wa Ubalozi wa Tanzania akiwa na maumivu makali. Aliniomba nimsaidie aje kwako kukuona akueleze mwenyewe mateso aliyoyapata. Bahati mbaya sikuweza kumsaidia kwa sababu kipindi hicho ulikuwa na shughuli nyingi za Kitaifa. Kupitia mchango wangu huu, nawasilisha ombi la kijana huyo Salumu mkazi wa Nzasa Mbagala kama utahitaji kumwona kama anavyotaka. Basi nijulishe nitampelekea taarifa akuone akiwa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli sina mchango zaidi kwani hotuba ni nzuri, sina cha kukosoa.

Mwisho, naunga mkono hoja hii tena mia kwa mia.

**MHE. BEATUS R. MAGAYANE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri Kikwete kwa hotuba nzuri na mafanikio makubwa katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la wakimbizi ni vyema lipewe msukumo wa kipekee. *UNHCR* kwa dhati waangalie uwezekano wa kuhudumia wakimbizi ndani ya nchi zao katika maeneo salama badala ya kuvuka mipaka na kuleta matatizo katika nchi jirani.

Jumuiya ya Kimataifa itimize wajibu wake kwa kutoa michango yao ya kuhudumia wakimbizi badala ya kutamka michango kama *public relations gimmick* tu. Wakimbizi wanapokosa huduma muhimu ni mwanzo wa kuleta wizi, vurugu na ujambazi katika Vijiji jirani. Pamoja na mwanga na matumizi yanayoonekana nchini Burundi, juhudi za makusudi kushawishi *FNL* kuweka silaha chini, bila hilo kufanyika Burundi haitatawalika. Pia mshikamano kwa Wahutu ni muhimu badala ya kupigana vijembe na kuendeleza uhasama.

Mheshimiwa Naibu Spika, matamshi ya nchi za Uingereza na Marekani kuwa wananchi wao wasitembelee Tanzania na hasa Zanzibar kwa sababu ya tishio la ugaidi, kumeathiri sana mapato ya nchi yetu. Ni vyema wawekwe to task kwa hasara tuliyoipata na hivi watakiwe kuziba pengo litakalotokea. Wasiwe wanasema hovyo bila kushirikisha nchi husika mapema.

Mataifa makubwa hudharau maamuzi ya Umoja wa Mataifa na kujiamulia wenyewe mambo jinsi wanavyotaka. Ni hatari. Kitendo cha Marekani na Uingerza kuvamia *Iraq* bila idhini ya Umoja wa Mataifa kimedhihirisha ubabe tu wa wakubwa, hata hizo silaha zilizosemekana zimelundikana hasijapatikana. Nini hasa ilikuwa kisa cha kuivamia *Iraq?* Mataifa haya yatakiwe kutamka kuwa walikosea na watakiwe kuijenga upya *Iraq* chini ya usimamizi wa Umoja wa Mataifa kwa gharama zao.

Nampongeza Rais Benjamin Mkapa kwa juhudi zake za kuleta amani eneo la Maziwa Makuu. Ni vyema na Wakuu wa nchi nyingine wakatambua juhudi hizo na wakaacha chokochoko za kuleta vurugu eneo hili. Naunga mkono hoja.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa pongezi kwa kazi nzuri ya Wizara kwa kudumisha sifa nzuri za nchi yetu. Pia pongezi zimwendee Rais wetu na Mabalozi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania kwa kushirikiana na nchi husika ijenge alama za kumbukumbu za kudumu katika maeneo yote yaliyokuwa ya wakimbizi katika Tanzania. Sehemu hizo ni:- ya Kongwa - Mkoa wa Dodoma, Mugagao - Mkoa wa Iringa, Nachingwea - Mkoa wa Lindi, Tunduru - Mkoa wa Ruvuma, Bagamoyo - Mkoa wa Pwani, Kurasini - Mkoa wa Dar es Salaam, Mazimbu - Mkoa wa Morogoro na Dakawa - Mkoa wa Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuwe na siku ya kuwakumbuka mashujaa hawa na Askari wetu waliofia nje. Tuige mnara kama ule wa Washington *DC* kuhusu Waamerika waliofia Vietnam, ujengwe ili kuwakumbuka Askari wetu waliofia nje na majina yao yote yaandikwe kwenye mnara huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, agenda hii ipelekwe AU ili ifanyiwe kazi. Pia tuwe na Chuo Kongwa na pawe na mahali pa hija. Makambi yote yatunzwe na yajengwe vizuri ili yawe mahali pa utalii wa aina yake. *Vision and mission ya foreign policy* ukurasa wa 17 *English Vision, Geiographical position* ya nchi yetu itumike vizuri kwa kujenga barabara za kuunganisha Bahari ya Hindi na Maziwa ya Tanganyika na Nyasa na kutoka Kusini hadi Kaskazini ili ifaidike na transit trade.

Kuna hatari ya Makampuni ya Afrika ya Kusini kuua Bandari ya Kigoma, Reli ya Kati na Bandari zetu kwa kujenga Bandari ya Mpulungu na barabara nzuri na reli kutoka Mpulungu kuelekea Kusini Via Kusama. Hii ni hatari kwetu. Msumbiji wanajenga Pemba na Beira ili kuzuia daraja la Muungano. Wakati wa kutekeleza *vision and mission* ya sera yetu ni huu. Inshallah.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuchukua fursa hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Jakaya M. Kikwete, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Naibu Waziri Mheshimiwa Dr. Abdulkader A. Shareef, Katibu Mkuu Ndg. Phillemon L. Luhanjo, Katibu Mkuu, viongozi na watumishi wa Wizara, Balozi zetu na Taasisi zote zilizo chini ya Wizara hii kwa hotuba nzuri. Nafarijika sana.

Wizara hii imeendelea kufanya kazi nzuri sana ya kuboresha uhusiano wa Kimataifa na kuitangaza Tanzania duniani katika jitihada za kukuza uwekezaji, biashara, utalii na masuala mengine muhimu yenye maslahi kwa Tanzania duniani kwa jumla na katika uhusiano na majirani zetu katika *EAC, SADC* na nchi za Maziwa Makuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile ni jambo linaloleta matumaini makubwa kwamba Wizara imekamilisha sera mpya ya Mambo ya Nje inayoweka mkazo mkubwa zaidi katika diplomasia ya kiuchumi *(Economic Diplomacy).* Hii ni hatua kubwa katika kujikomboa kiuchumi na kuitoa Tanzania miongoni mwa nchi masikini zaidi duniani *(LLDCs)* hasa katika zama hizi za utandawazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo hapana budi kwa Wizara hii na Serikali kwa jumla kuchukua hatua thabiti za kutekeleza kwa vitendo na kwa mafanikio ya hii sera mpya. Zaidi ya kutamka, hapana budi kuboresha utendaji wa Balozi zetu nje ili ziweze kumudu kwa ufanisi mkubwa zaidi wajibu wao wa kutekeleza sera hii mpya. Nashauri kwamba ama mafunzo maalum ya uendelezaji uwekezaji na biashara yatolewe kwa Mabalozi wetu pamoja na Maafisa wa Balozi zetu wanaohusika na masuala ya uchumi au wengi wa Mabalozi wapya na watumishi wapya wa Balozi zetu wawe waliobobea katika fani za uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya hivyo, nashauri kwamba mkazo mkubwa uwekwe katika kuhakikisha kwamba waambata wa biashara/uchumi wanakuwepo kila inapowezekana katika kutekeleza jukumu hili, ni muhimu kwa Mabalozi wetu hasa katika *bilateral missions* na waambata wa biashara

wawekewe malengo maalumu na mafanikio yao katika kuyafikia/ kupita malengo hayo pamoja na ufanisi wao katika kuleta taarifa za masoko *(Market Intelligence)* kuhusu uwekezaji, utalii, biashara na maeneo mengine yatakayowezesha kukuza/kuboresha maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili sera hii mpya na Balozi zetu ziweze kupata mafanikio yanayotarajiwa, hapana budi kuboresha utendaji wa wadau mbalimbali hapa nyumbani pamoja na kuboresha uhusiano wa kiutendaji kati ya Balozi zetu na wadau mbalimbali kama vile Wizara ya Viwanda na Biashara, Kilimo na Chakula, Ushirika na Masoko, Nishati na Madini na Maji na Mifugo pamoja na Taasisi zao husika. Aidha, utendaji uhusiano bora na Taasisi zisizo za kiserikali kama vile *TCCIA, TCI* na kadhalika. Ni muhimu katika ufanikisha jitihada zinazohitajika chini ya hii sera mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha biashara cha Tanzania kilichopo London kimefanya kazi kubwa na nzuri katika kukuza uwekezaji, utalii, biashara na masuala mengine ya kiuchumi. Nashauri Wizara/Serikali itazame uwezekano wa kufungua Vituo vipya vya aina hii katika maeneo na nchi nyingine. Aidha, Wizara itazame uwezekano wa kuongeza idadi ya wawakilishi wa heshima *(Honorary Counsels),* pale ambapo hatujafungua Balozi zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza kabisa nianze kwa kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii adimu, na mimi vilevile nichangie kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Napenda kusema bayana kwamba naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kadhalika napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote waliochangia kwa kauli na kwa maandishi ambao bila shaka Mheshimiwa Waziri atawatambua kwa majina kwa michango yao mizuri iliyojaa busara na uzalendo na yenye lengo la kuimarisha utendaji kazi wa Wizara yetu kwa manufaa ya wananchi wetu na Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, naomba Mheshimiwa Waziri aniruhusu kwa njia ya pekee nimshukuru kwa dhati kabisa Mheshimiwa Dr. William Shija na Wanakamati wake kwa michango yao muhimu sana. Ushauri wao kwetu na vilevile ushirikiano wao na sisi katika kutekeleza majukumu yetu. Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, kwetu sisi kwa kweli kabisa na kwa dhati nakiri kusema kwamba wamekuwa chachu kubwa sana kwetu sisi.

Siyo tu katika kutekeleza na kufanikisha majukumu yetu mbali pia katika kututetea na kutusemea kwa Mheshimiwa Waziri Basil Mramba ili Mheshimiwa Basil Mramba azidishe huruma na uungwana wake kwetu sisi. Licha ya ukweli kwamba mafanikio ya uwindaji wake ni sana sana kuua sungura moja tu au wawili na si kuua kongoni, sikwambia nyati au kiboko.

Kwa hiyo, nawashukuru sana Wanakamati wa Mambo ya Nje. Kama ninavyomshukuru vilevile mwindaji wetu mkuu Mheshimiwa Basil Mramba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, namwomba Mheshimiwa Waziri aniruhusu nimshukuru binafsi vile vile rafiki yangu na ndugu Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Msemaji wa Kambi ya Upinzani wa Mambo ya Nje, kwa michango yake na ushirikiano wake nasi katika kutekeleza majukumu yake.

Nampongeza pia kwa kupewa nafasi hiyo ambayo naamini kwamba sio tu hataitendea haki lakini pia naamini ataishikilia kwa muda mrefu sana kivulini. *(Makofi)*

Nampa pole ndugu yangu Mheshimiwa Khalifa kwa hilo la mwisho, kukaa kivulini kwa muda mrefu. Lakini napenda kumhakikishia kwamba sisi Wizarani, mimi na Waziri na maafisa wetu wote tutampa msaada wote na ushirikiano wote anaoutaka katika kutekeleza kazi zake kwa manufaa ya nchi yetu na manufaa ya wananchi wetu. Asisite kuomba msaada huo pale anapohitaji. Ofisi yangu na Ofisi ya

Waziri milango yetu iko wazi kabisa. Mheshimiwa Khalifa nampongeza, namkaribisha na namshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nitoe mchango wangu kwa kutoa ufafanuzi na majibu kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa baadhi tu ya maswali na mapendekezo mepesi mepesi waliyotoa kama anavyosema ndugu yangu pale Mheshimiwa Semindu Pawa na kumwachia Mheshimiwa Waziri maswali na mapendekezo mazito mazito. Maana Waswahili wanasema kama simba mwenyewe yupo uwanjani hakuna sababu ya mimi kujaribu kuunguruma. Ila napenda niseme wazi tu kwamba hata ninapojaribu kuunguruma basi nakuhakikishieni naunguruma kwa msaada wake mkubwa na ushirikiano wa hali ya juu anaonipa mimi binafsi na anaowapa wenzangu Wizarani wengine, tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, michango ilikuwa mingi sana kiasi kwamba hadi tunakaa ilikuwa ikiteremka kama mvua hapa. Kwa hivyo tutajaribu kujibu yale ambayo yanatuhusu sisi lakini watu pia kwa kutupenda na kwa kuona kwamba tunajaribu na tunajitahidi kutekeleza majukumu yetu hapa wametupa maswali mengi mengine siyo yetu. Lakini tunachotaka kusema ni kwamba yale yetu tutayashughulikia na kuyajibu hapa kadri tuwezavyo. Yale ambayo hatutapata nafasi hapa kuyajibu kwa kina au hata kuyajibu kwa ufupi basi tunawaahidi Waheshimiwa Wabunge hatukudharau wala hatukupuuza tutayashughulikia kwa maandishi na kwa kina moja baada ya moja. Natumaini yale ambayo sio yetu wanayowahusu wameyasikia. Lakini sisi tunataka kuwahakikishieni pia tutachukua jukumu la kuyafikisha kwa waliyoyahusu. Kwa hivyo kama hatukuyataja hapa sio kama tunadharau. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na mchango mkubwa na mzuri uliotolewa na Wanakamati, Kamati ya Mambo ya Nje. Imependekeza kwamba zitolewe fedha za robo mwaka ili kulipia madeni yaliyolimbikika hasa kuhusu pango za nyumba na mishahara ya *local staff.* Ninachotaka kusema ni kwamba Wizara yangu kwa kweli ilizitaka Balozi zetu zote zilizoko nje zitume maelezo na ufafanuzi kamili wa madeni waliyodaiwa hadi mwisho wa mwaka wa fedha, mwaka jana. Walifanya hivyo, walituletea maelezo yao kamili, madeni yote wanayodaiwa na sisi kwa bahati nzuri kuanzia mwaka wa fedha wa 2003/2004 Serikali iliamua kwa kweli kutoa fedha ya matumizi ya mengineyo katika mtindo huo wa robo mwaka. Kwa hiyo, uamuzi ulikuwa tayari umetolewa, lakini ninachopenda kusema ni kwamba Wizara ilitupa fedha za madeni yote yale yaliyoorodheshwa na Balozi zetu na sisi tukazituma fedha hizo kwa Balozi zetu sote. Kwa hivyo tunaamini na tunaraji kwamba hatutakuwa na deni wala hatuna deni hadi kufikia mwisho wa mwaka wa fedha. Sasa jana au juzi kuanzia mwezi huu kama yametokea hayo hatuna uhakika nao, lakini tunachukua juhudi ya kuhakikisha kwamba hakutakuwa na madeni, hizo ni juhudi tunazozichukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Kamati imependekeza kwamba zipatikane fedha za maendeleo ili ziweze kusaidia kujenga majumba. Hili nitamwachia Mheshimiwa Waziri. Lakini lingine ambalo limezungumziwa hapa ni kwamba sera yetu ya diplomasia ya kiuchumi, tunakubaliana na maoni ya Kamati kwamba ipo haja ya kuangalia kupanua wigo wa washiriki katika suala zima la diplomasia ya kiuchumi, hilo tunakubaliana naye kabisa. Kwa kweli tumeanza kushirikisha vikundi vya wafanyabiashara mbalimbali katika suala hili la kupanua wigo wa wadau wa kusaidia sera yetu ya Mambo ya Nje ambayo inalenga zaidi katika mambo ya uchumi. Hivi karibuni Wizara itaanza kuleta taarifa mbalimbali vile vile katika website ya Taifa kuhusu maswali ya Tanzania.

Aidha, napenda kusema kwamba Balozi zetu zilizopo nje hasa za Tokyo na London na nyingi tu nyingine zinazo website zao tayari. Kwa hivyo na wao wanachangia katika kutoa taarifa zinazohitajika na kushiriki katika kuendeleza na kusambaza sera yetu ya kuvutia mambo ya uchumi. Kazi nyingine ambayo imeshaanza kufanyika na imefika mbali tuko katika hatua za mwisho mwisho ni kuwa na website yetu wenyewe Wizarani. Muundo wa *website* ile umekamilika sehemu nyingi ambazo zinahitaji taarifa zimeshatiwa lakini yale maswali mazito mazito na ufafanuzi wa kina bado haujaingizwa kwa sababu lazima tupate michango ya Wizara mbalimbali zinazohusika. Kwa hivyo tumo katika kutafuta michango ije ili na sisi tuweze kuikamilisha na kukamilisha suala hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu barua imetolewa pendekezo kwamba kuwepo barua ambazo zinakuja ama kwetu Wizarani au katika Wizara nyingine wakati mwingine inachukua muda mrefu

hazijibiwi. Ni kweli tunakubali kwamba tatizo hilo lipo. Lakini ukweli wenyewe ni kwamba sio barua zote zinazokuja Serikalini huwa zinatakiwa sisi tutoe majibu. Kwa zile ambazo tunatakiwa tutoe majibu tunakuwa tunatoa inaweza ikatokea upungufu hapa na pale, lakini tutajitahidi, lakini pia barua nyingine inabidi tuzipeleke katika Idara, Ofisi na Taasisi mbalimbali zinazohusika. Kwa hivyo pia inatokea wakati mwingine barua ikachelewa kwa sababu mbalimbali, sidhani kwamba kuna upuuzi wa makusudi au dharau wakati mwingine watu wanatingwa na kazi, lakini tunaahidi kuchukua hatua ambazo zitasaidia kufuatilia swali hili.

Pia imependekezwa kwamba Wizara ifungue Balozi wetu kule Uholanzi, Arabuni, Asia na Amerika ya Kusini hasa hasa Brazil. Kama Mheshimiwa Waziri alivyoeleza katika hotuba yake kwamba ipo nia ya kufungua Balozi katika nchi hizi ambazo amezitaja na vile vile alifafanua kwa nini kwa hivi sasa pamoja na kwamba tumefungua Ubalozi wetu kule Uholanzi tulilazimika kwa kipindi hiki kifupi tu kwamba tusiende kufungua kwa hivi sasa, lakini baadaye tukijaliwa mwakani lengo hilo lipo la kuendelea kufungua. Kwa hivyo napenda kwamba muamini na nasema kwamba dhamira ya Serikali ni kuwa na Ubalozi katika maeneo yote muhimu ambayo kuna maslahi muhimu ya Tanzania hasa ya maswali ya kiuchumi na hilo ndilo linalotusukuma.

Kwa hiyo, ipo nia ya kufungua Ubalozi Oman ambao wapo Waheshimiwa Wabunge waliozungumzia suala hili kwa sababu ya ukaribu wetu na wao, historia, lakini vile vile kwa sababu ya biashara. Tuna wananchi wa Tanzania pale wasiopungua nusu milioni ambao kwa njia moja au ya pili wana mahusiano ya Tanzania, hata kama wao wameshachukua uraia wa kule, lakini bado wana mahusiano ya Tanzania. Watoto wao, familia zao na ndugu zao. Kwa hivyo hiyo ni sababu peke yake inayotufanya tufungue Ubalozi. Lakini kwa hivi sasa bado matazamio yetu katika kipindi cha miaka 10 ijayo tutakuwa tumeshafungua Balozi katika nchi hizi hasa Oman, Malaysia na ikiyumkinika Amerika ya Kusini kama Brazil.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Kamati ilipendekeza kwamba Chuo cha Kidiplomasia kile ile milki ya kumiliki jengo lile ipewe Tanzania, ili Tanzania iweze kusimamia suala hili. Suala hili kwa kweli linashughulikiwa kati ya Wizara yangu na Serikali ya Msumbiji. Napenda kusema kwamba Majadiliano kuhusu suala hili yako katika ngazi za juu kabisa Serikalini na tumefikia mbali na tunaamini kwamba haitachukua muda kabla ya kupata jibu ambalo tunalipenda na ambalo nyinyi wenyewe mmelipendekeza hapa.

Kuhusu kupandishwa hadhi Chuo chetu cha Diplomasia napenda kusema kwamba Wizara hivi sasa kwa kushirikiana na Chuo inaendelea na mipango mizuri kabisa ya kukipandisha hadhi chuo hicho. Tumeanza na ukarabati wa majengo kama alivyoelezea Mheshimiwa Waziri vile vile uajiri wa watumishi na sasa mitaala ya chuo hicho vile vile imerekebishwa ili chuo hicho kiwe na mitaala ya kuhusika na mambo yanayotupa shida sana siyo kwetu sisi lakini katika eneo letu zima nalo ni *conflict resolution* na *strategic studies.* Tumeiagiza Bodi ya Magavana ambayo imezunduliwa hivi karibuni kusimamia swali hilo lakini tuna hakika kwamba itachukua muda mrefu kabla ya kuikamilisha dhamira hiyo.

Pia kumetolewa pendekezo kwamba Mikutano ya Kimataifa mingi kabisa ifanyike nchini. Napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba tutajitahidi na kwa kweli tunajitahidi kuvuta Mikutano mbalimbali ya Kimataifa kuja nchini kwetu. Mkutano huu utakaofanyika kuhusu *Great Lakes Region* wa viongozi ni sehemu hiyo ya mbio zetu tunazokwenda kwamba Mikutano kama hii ije katika nchi yetu. *(Makofi)*

Lakini pia napenda kukumbusha katika hotuba ya Mheshimiwa amedokeza pale kwamba Mikutano mingi ya Kimataifa imefanyika katika kituo chetu cha Mikutano pale Arusha karibu Mikutano 120 na zaidi ya watu 14,000 wamekuja, bado tunasema kwamba ni ndogo na bado tunataka kuzidisha juhudi kwamba Mikutano ya Kimataifa izidi kuwa mingi nchini Tanzania. Nadhani sasa hivi hali ya upatikanaji wa mahoteli katika Tanzania umeimarika sana, hali za usafiri, ndege zinakuja nyingi kwa hivyo ipo hoja ya sisi kuijenga kwa wenzetu kwamba kwa nini tatizo lenu ni nini ikiwa mahoteli yapo, ikiwa hali ya hewa nzuri ipo, ikiwa mnataka ukarimu upo, mkitaka watu wapole wapo, mkitaka usalama wenu upo, vyote ambavyo mnavitaka kwetu vipo. Kwa hiyo, wanaanza kusikiliza na tunaamini tutazidi kufanikiwa.

Vile vile Kamati imependekeza kusaidia Watanzania wengi kupata kazi katika Taasisi na Mashirika mbalimbali ya Kimataifa. Kwa kweli hiyo ni kazi yetu tumekuwa tukiifanya na tunaendelea kuifanya. Lakini tutazidi kushirikiana na wenzetu ambao wana *database* nayo ni Utumishi, kwa sababu jukumu la kuwa na *database* ya wataalamu wa Kitanzania, wenye ujuzi mbalimbali ndani ya nchi na hata kwa nje ya nchi kimsingi ni jukumu la Utumishi. Sisi tutashirikiana nao kuwasaidia kupata na kuandaa *database* ya Watanzania wanaoishi nchi za nje kwa kutumia Balozi zetu, kutumia *website* ili Watanzania wajiandikishe na wameshaanza kufanya hivyo. Ubalozi wetu wa London, Bonn wana *page* maalum ya kuwataka Watanzania wenye utaalamu mbalimbali wanaoishi, wanaofanya kazi hata wale ambao wamebadilisha uraia wao lakini bado asili zao ni Watanzania pia waingie katika *database* ile. Kwa sababu hatimaye watu kama hawa watatusaidia tu katika kujenga nchi yetu, imani yao, mapenzi yao bado yako nchini. Kwa hiyo, tutashirikiana na utumishi katika kutayarisha *database* kama hiyo.

Vile vile Kamati imesema kwamba tuongoze na tuongeze juhudi katika kueneza lugha ya Kiswahili itumike katika Bara la Afrika. Tumelivalia njuga, Mheshimiwa Semindu Pawa huwa ana usemi huu anasema kwamba Kampeni mmempa mjuzi, nzi watashika adabu zao. Pia amezungumzia Kamati kuhusu sera ya Kidiplomasia ya kiuchumi, Wizara inakubaliana na maoni ya Kamati, Wizara itashirikiana kwa karibu sana na Wizara nyingine husika kama vile Maliasili, Viwanda, Biashara, Kilimo na kadhalika ili kutekeleza sera yetu hii mpya ya mambo ya kiuchumi. Kwa hiyo, tumekuwa tukifanya hivyo. Lakini tutazidisha tu juhudi na hasa kwa vile sasa hivi jukumu la kutetea na kupigania sera yetu hii si la Wizara yetu peke yetu kama alivyosema Mheshimiwa Waziri mwanzoni mwa hotuba yake. Kwamba inahusu wote wadau, inahusu Wabunge vile vile, kwa hivyo tutashirikiana na ninyi nyote katika kufanikisha swali hili. Maswali mengine namwachia Mheshimiwa Waziri mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Khalifa amesema maneno haya napenda kunukuu: “Hakuna rafiki wa kudumu bali maslahi ya kudumu, kilicho cha kudumu na maslahi ya Taifa husika tu”. Wanasema Waingereza, *we could’nt agree with you more.* Huo ndio msingi unaotuongoza na ndio utakaoendelea kutuongoza. Kwa kweli swali hilo la maslahi ndilo linaloongoza Mataifa mengi duniani hivi sasa, sisi kamwe hatutakuwa na uhusiano na mtu wala uhusiano na nchi kwa ajili ya maslahi yake yeye. Siku zote maslahi yetu ndiyo yatakuwa mbele. Sasa kama maslahi yetu yatawiana na yake au hayatogongana na yake na yeye akawa tayari kushirikiana na sisi tutamnyooshea mkono. Lakini kama akifikiri kwamba atataka tuanzishe uhusiano kwa maslahi yake mwenyewe la! la! la! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Khalifa na kulihakikishia Bunge lako kwamba sisi hatushiki kuti kavu, kabisa. Sisi tunashika matawi madhubuti mabichi yaliyojaa matunda. Kuhusu Jumuiya ya Afrika Mashariki nitamwachia Mheshimiwa Waziri alielezee kwa uzuri. Lakini kuna swali moja ambalo Mheshimiwa ameligusia na baadhi ya Wabunge pia wameligusia, donda ndugu, *OIC.*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili ni kweli kwamba baada ya Zanzibar kujiunga na *OIC* na kukazuka utata kuhusu kujiunga kwake uhalali upo au haupo je matatizo gani yatatokea, je, Katiba iliangaliwa, haikuangaliwa na kadhalika, kiasi kwamba likazuka sokomoko ndani ya nchi lakini pia vile vile wale wanaopenda kufitini nje ya nchi na wao wakaingia katika ngoma, wakaanza na wao kuzusha maneno likawa limeleta sokomoko kubwa sana kiasi kwamba lingetuvuruga.

Kwa hiyo, tukaona busara na kuzungumza sisi kama watu waliokomaa, kama wananchi wenye kupenda amani, usalama, utulivu na umoja wa nchi yao tukakubaliana sote kwamba kwa hivi sasa Zanzibar itoke. Serikali ya Muungano ifanye uchunguzi wa kina na iangalie kwa taratibu na umakini uwezekano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kujiunga au kutojiunga lakini bila ya kutuongoza mwongozo mkuu, sababu kuu, lengo kuu liwe maslahi ya nchi yetu. Bila ya kuathiri umoja wetu, bila ya kuvuruga amani yetu na nchi yetu ibakie moja. Kama maslahi yatapatikana kwamba yapo na misingi muhimu tuliyojiwekea haitavurugika wala haitaharibika hakuna sababu kwa nini tusijiunge. Uchunguzi huo umekuwa unaendelea vizuri, umekuwa unafanyika vizuri, umefikia karibu hatua za mwisho mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeshaulizwa hapa kama mara mbili au tatu na ninaamini hata nasikia lipo swali kama hilo bado linakuja. Lakini napenda kusema tena hapa kwamba Serikali ya Muungano ilipotoa ahadi yake kamwe haikutoa kwanza peke yake imetoa kama Serikali ya Muungano ambayo

imetujumuisha sote. Pili, haikutoa kwa hadaa wala udanganyifu wala shagalabagala la! imetoa kwa uthabiti kabisa na kwa imani kabisa kwamba litashughulikiwa ipasavyo lakini tulinde misingi yetu mikuu ambayo tumekuwa tukiipigania na kuitetea miaka nenda, miaka rudi kiasi kwamba kila mtu ndani ya Bara la Afrika, nje ya Bara la Afrika sio tu wanastaajabu kwamba Tanzania pamoja na makabila yote tuliyokuwa nayo, dini tulizokuwa nazo, rangi tulizokuwa nazo na umaskini tuliokuwa nao.

Tmeshikamana kitu kimoja kuna amani, utulivu wanatuonea gele wengine, wengine wanashangaa kwa sababu zote ambazo zimepelekea nchi nyingi ndani ya Afrika na nje ya Afrika kusambaratika na kuingia katika migogoro zipo Tanzania. Ikiwa kama makabila tunayo, kama dini tunazo, ikiwa kwa rangi tunazo, unachokisema hapa ambacho kinawavuruga wengine huko nje sisi tunazo, lakini na papo bado tumesalia watu wamoja, kitu kimoja nchi ya amani na utulivu nawasihini ndugu zangu Watanzania ndani ya Bunge hili na nje ya Bunge hili tuaminiane hivyo. Hakuna nia mbaya, nia thabiti kabisa. Swali hili nimeanza kufikiria mwisho na hatua muafaka itachukuliwa ambayo ni ya maslahi ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Mheshimiwa Khalifa amezungumzia suala la Zimbabwe anasema hivi Tanzania inaunga mkono Zimbabwe inamwunga mkono Mugabe na kupinga Wapinzani hivyo anashauri tusiendelee na kumkumbatia Mugabe na tuachane kukumbatia watu wanaotaka usultani na kukaa madarakani milele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania haiungi mkono mtu. Si Rais Mugabe tu lakini mtu yoyote kwa sababu suala la kuchaguliwa kiongozi katika nchi yoyote ni swali la wananchi wenyewe, sio letu. Lakini ikiwa itatokea nchi ikataka kulazimisha nchi mojawapo kama hizi za Afrika kwamba lazima nchi ile imchague fulani au imuache fulani hapo tutapiga kelele. Tukipiga kelele hatupigi kelele kwa sababu sisi tunampenda mtu yule Principle, basi.

Lakini tunasema kwamba sisi tunachounga mkono kule Zimbabwe ni wananchi wa Zimbabwe na Zimbabwe yenyewe kwa haki yao ya ardhi yao. Tunaunga mkono wananchi wale wamiliki ardhi yao waliojaliwa na Mwenyezi Mungu kama tunavyomiliki sisi na katika hilo tusione haya wala tusione vibaya. Kwa sababu siku moja itatujia sisi itawajia wengine la kwa hili tunaunga mkono nchi, tunaunga mkono wananchi, tunaunga mkono haki zao, sio mtu. Lakini tukasema pia Tanzania haipuuzi umuhimu wa Utawala Bora na inashikilia suala hilo inasema jamani Utawala Bora ndio ufunguo, hatupuuzi hilo.

Kuhusu viongozi kung'ang'ania madaraka kwa muda mrefu napenda kusema kwamba huo ni uamuzi wa nchi husika kwa mujibu wa taratibu zao. Sisi tuna utaratibu wetu hapa nchini kwa vipindi viwili vya miaka mitano mitano kwa Marekani vipindi viwili miaka minne minne hata sisi katika CCM hapa tuna utaratibu wetu tuliojiwekea wa kubadilishana viongozi. Tumetoka kwa Mwalimu Marehemu Mungu amlaze mahali pema, tumekwenda kwa mzee wetu Mzee Mwinyi, tumetoka kwa Mzee Mwinyi tumekuja kwa Rais Mkapa na utaratibu huo ndio tunaokwenda nao wa kubadilishana viongozi katika chama chetu. *(Makofi)*

Kuhusu kuburuzwa na mataifa makubwa yumkini Mheshimiwa Khalifa anazungumzia nchi nyingine sio Tanzania. Tanzania hii haiburuzwi na wala haitaburuzwa. Nadhani kwamba hata Mheshimiwa mwenyewe anatuunga mkono juu ya msimamo wetu wa Iraq. Tumechukua msimamo mmoja kwa sababu hata hatuburuzwi na hata wakubwa wanaojaribu kutaka kutuburuza wanalielewa vizuri hilo. Kwa hivyo wanapokuja kwetu wanakuja kwa heshima yao, wanakuja kwa adabu zao wanajua mipaka yao iko wapi. Sisi hatuchelei kusema sio mzee na hayo tukiendelea kuyafanya. *(Makofi)*

Kuhusu sera ya kupambana na ugaidi na maana ya ugaidi sisi sera yetu iliyoletwa hapa haikutoka Marekani hatukuburuzwa na mtu yeyote ni sera imeanzia Umoja wa Mataifa sisi tulikuwa part ya *negotiation.* Misaada iliyopitia katika AU sisi tulikuwa wakunga wa kuizalisha na zaidi ya hapo sisi tuliathirika wenyewe hatukuburuzwa na mtu yoyote na wala hatutaburuzwa.

Sasa kama itatokea iwiane na wengine hiyo si kama wao wametaka, bali kwamba sisi tunafuata mkondo ulio sahihi. Sera ya Mambo ya Nje anazungumzia hivi kwamba Ubalozi si mahali pa kupumzika na kuzeeka taratibu.

Sisi tunasema naam!! Kweli kabisa na hakuna mtu anayeteuliwa kwa ajili ya kwenda Ubalozini kustaafu au kuzeeka taratibu. Uteuzi wa Mabalozi unategemea pamoja na mambo mengine nini *mission* nini jukumu la mahali na wakati anaopelekwa Balozi yule.

Hili halihusiani na umri linahusiana kama mshenga ukitaka kumtuma mtu pahali unamtazama nani nikimtuma ana uwezo, ana ujuzi na anaweza akafanikisha malengo yako. Hayo ndiyo tunayoyapata.

Kuhusu mgogoro wa Burundi anasema kama karoti haifai si vibaya kujaribu shubiri. Ni kweli hiyo ni njia mojawapo kama inawezekana kutumika. Lakini kama hapana budi Mzee Mwinyi alikuwa anasema "kama unaweza kumwua mtu kwa asali kwa nini umuue kwa sumu".

Kwa sasa bado hatuamini kwamba tumefikia kutumia shubiri au kutumia bakora. Katika suala hili vile vile kuna Mbunge aliyependekeza kwamba tatizo la Burundi bora ni kumwita Rais Bush aende kule akaifanye kazi nzuri aliyoifanya Iraq.

Sidhani kwamba hata Rais Bush mwenyewe baada ya aliyoyaona Iraq kama atapenda kwenda pahali pengine, lakini hilo nitamwachia mwenyewe apeleke kama sisi hatutaweza kupeleka. *(Makofi)*

Kuhusu hali ya muafaka wa CCM na *CUF* nasema kwamba sisi tunaisemea nchi yetu tunapokuwa nje. Sisi kama Wizara ya Mambo ya Nje tunasemea maswali yote ya nchi yetu tunapokuwa nje. Tunapokuwa ndani ya nchi masuala yasiyotuhusu tunaachilia wanaohusika. Kwa hiyo, naamini pia naye anaelewa utaratibu wa suala zima hili la CCM na *CUF* kuhusu muafaka, anajua taratibu zilizokuwepo, anajua wapi pa kusemea na anajua nani anashughulika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo napenda kuunga mkono hoja asilimia kwa mia. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NCHI ZA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote ambao wamechangia humu ndani ya Bunge na wale ambao walichangia kwa maandishi.

Wabunge wenzetu wapatao 14 wamechangia Bungeni na tumepata michango ya maandishi 21 kwa hiyo tumechangiwa sana. Lakini nianze tu kwa kusema kwamba tunawashukuru kwa yote mliotuchangia, mmetuimarisha nasi tutakwenda kuyafanyia kazi. *(Makofi)*

Naomba niwatambue waliochangia humu Bungeni. Kwanza ni Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje Mheshimiwa Dr. William Shija, Msemaji wa Kambi ya Upinzani, swahiba wangu Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Waziri Kivuli, Mheshimiwa Mwadini Abass Jecha, Mheshimiwa Freeman Mbowe na Mheshimiwa Lazaro Samuel Nyalandu.

Waheshimiwa Wabunge wengine ni Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, Mheshimiwa Anatory Choya, Mheshimiwa Mohamed Abdully Ally, Mheshimiwa Muttamwega Mgaywa, Mheshimiwa Gwassa Sebabili, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed na mwisho kabisa ni Mheshimiwa Naibu Waziri Dr. Abdulkader Shareef. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Mohamed A. Abdulaziz, Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mheshimiwa Prof. Juma A. Kapuya, Mheshimiwa Dr. Milton M. Mahanga, Mheshimiwa Aziza S. Ali, Mheshimiwa Leonard N. Derefa, Mheshimiwa Beatus R. Magayane, Mheshimiwa Mbaruk K. Mwandoro, Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mheshimiwa Frank M. Mussati, Mheshimiwa Semindu K. Pawa, Mheshimiwa Ireneus N. Ngwatura, Mheshimiwa Esha H. Stima, Mheshimiwa Aggrey D. J. Mwanri, Mheshimiwa Kilontsi M. M. Mporogomyi, Mheshimiwa Ali Said Salim, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mheshimiwa Jeremiah J. Mulyambatte, Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud, Mheshimiwa Jackson M. Makwetta na Mheshimiwa Abdullatif Hussein Esmail. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Naibu Waziri kwa kufafanua mambo mengi, kwa hiyo sitachukua muda mrefu kwenye hayo. Lakini naomba nianze kwa kuzungumzia hili suala la Jumuiya ya Afrika Mashariki, kumekuwepo na maswali au ushauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kumekuwepo na ushauri kwamba tuongeze wingi wa bidhaa, lakini pia tuongeze ubora. Pia, tuwe na mkakati maalum wa kujipenyeza katika masoko ya Kenya na Uganda. Haya aliyasema Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa. Tumefurahia sana ushauri wake, sisi Serikalini tunasema tumesikia, natumaini wenzetu wa Sekta binafsi nao wamesikia. Lakini wakati wote ndio jitihada yetu kwamba tungependa kuwa washiriki wa ukamilifu na siyo tupo tupo tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo na suala la nafasi ya Zanzibar katika Jumuiya. Suala hili limezungumzwa na Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mheshimiwa Mohamed Abdully Ally na wapo wengine wamelileta kwa maandishi. Labda nieleze tu kwamba, Jumuiya tuliyonayo katika muundo wake ina tofauti kidogo na Jumuiya tuliyokuwa nayo. Jumuiya yetu ya sasa kazi yake kubwa ni uwezeshaji *(facilitation),* kutengeneza mazingira. Hakuna kitu unachoweza ukaenda kwenye Jumuiya pale ukakipata, kipo tu hivi unakwenda kukichukua na kwa hiyo ukasema: "Sisi Tanzania vipi, sisi Kenya kuna nini, sisi Zanzibar kuna nini, sisi Bara kuna nini!"

Mheshimiwa Naibu Spika, Jumuiya yetu inatengeneza mazingira ya kuwezesha kuongezeka kwa uzalishaji mali Afrika Mashariki kama *one investment area.* Unatengeneza mazingira ya kuwezesha soko la Afrika Mashariki kupanuka, lakini pia unafanya kazi ya kuwezesha bidhaa na huduma kufika kwenye soko kwa urahisi. *Consensually,* hiyo ndio kazi inayofanywa na Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Kwa hiyo, hakuna kitu pale utakachokwenda ukasema sisi chetu kipo wapi? Hakuna cha kupata pale! Jumuiya inashughulika zaidi katika masuala ya kuweka sera zitakazowesha uzalishaji kuongezeka, huduma kuongezeka, soko kupanuka na bidhaa kuweza kutoka upande mmoja kwenda upande mwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la kuwa na bidhaa za kuuza katika soko, kuwa na huduma ya kuuza katika soko ni la nchi moja moja, ni la raia wa nchi hizo na ni la wafanyabiashara wa nchi hizo. Inategemea sasa nchi yenyewe ilivyojizatiti kuongeza uzalishaji na ilivyojizatiti kuwa na kitu cha kuuza katika hilo soko. Wakati mwingine zile sera za Jumuiya ya Afrika Mashariki zinawezesha pia kusaidia uwezeshaji ukue ndani ya nchi na huduma zikue.

Mheshimiwa Naibu Spika, nini kwa mfano ninapozungumzia kuwezesha bidhaa au soko kupanuka au bidhaa kufika kwenye soko? Kwa upande wa sera nitatoa baadhi tu ya mifano. Kumefanyika uamuzi wa Benki kuu kwa nchi zetu za Afrika Mashariki kuhusu *convertibility of the currency.* Zamani kabla ya hapo ukitaka kwenda kufanya biashara Kenya, inabidi uende Benki ya hapa Tanzania uchukue hela za Tanzania, ubadilishe upate Dola, halafu unakwenda Kenya, kule unakwenda kwenye Benki ya huko unabadili unapata hela ya Kenya unakwenda dukani kununua bidhaa. Kwa uamuzi wa uwezeshaji kisera, tumekubaliana kwamba huna haja ya kufanya hivyo. Chukua hela zako za Tanzania, unakwenda kwenye Benki yoyote Kenya, unabadilisha unapata noti za Kenya, unakwenda kununua bidhaa unarudi zako Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huo ni uamuzi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa hiyo, kama kuna kitu utakachokitafuta, cha kupata kwenye Jumuiya ile, watakwambia tumeshakuwezesha kufanya biashara kwa uamuzi wetu huu wa sera.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kurahisisha usafiri, iko *passport* ya Afrika Mashariki, kuna *interstate pass,* tumekubaliana kwamba utakapofika kwenye *airport* utakuta kuna *counter* maalum ya raia wa Afrika Mashariki ambapo mnapita kwa haraka zaidi (kwa upendeleo). Kwa hiyo, hayo ndio maamuzi ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, kuna kurahisisha bidhaa kuvuka mipaka. Kwa mfano, umefanyika uamuzi wa harmonization of standards, Mashirika yetu ya viwango ya Afrika Mashariki yanakaa kwa pamoja. Yamezungumza na kukubaliana kwamba tutawianisha viwango vyetu vya ubora na

wakishakubaliana viwango vile vinatangazwa katika nchi zote tatu kwamba, viwango vya tairi za *General Tyre* ni hivi. Kwa hiyo, bidhaa ikionekana ina muhuri wa *TBS,* ukiipeleka Kenya huwezi kwenda kuulizwa tena. Wakenya hawawezi kupeleka kwenye Shirika lao la viwango waanze tena kutafuta ubora wa ile bidhaa. Viwango vya Tanzania ndio viwango vile vile ambavyo Kenya inavitambua na Uganda inavitambua. Huu ni uamuzi ambao umefanyika katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, unawezesha biashara kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano hivi sasa ninazungumzia *East African Customs Union,* miongoni mwa vikwazo vya kufanya biashara ni kodi na wakati mwingine kuna vikwazo vingine visivyokuwa kodi. Kwa mfano tulikuwa na matatizo hapa katikati, ya mbolea yetu ya Minjingu. Kuna wakulima Kenya walikuwa wananunua mbolea ile, lakini kulikuwa na watu wanaagiza mbolea kutoka nje, katika kutengeza fitina ya mbolea yetu ya Minjingu, wakasema ile *Minjingu phosphate* si mbolea! Kwa hiyo, ikawa inazuiliwa pale mpakani kwa sababu si mbolea! Hivyo ndio vikwazo ambavyo vinaitwa *non tariff barriers,* unatoa *definition* tu hivi, maana vingine wanaviwekea kodi na vingine wanaweka tu tafsiri ambazo zinakuwekea ugumu. Nasema *customs union* itatusaidia kwa kuondoa migogoro ile inayohusu viwango ambavyo ni vya kodi, lakini pia vitatuwezesha hata kufika mahali kuondoa hizi *non tariff barriers.*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uwezeshaji miundombinu ni kitu muhimu sana. Kwa hiyo, Jumuiya ya Afrika Mashariki inachokifanya ni kuhakikisha kwamba ili bidhaa ziweze kutoka Uganda zikafika Tanzania, zikatoka Tanzania zikaweza kufika Kenya, suala la miundombinu limeangaliwa kwamba ni moja ya kitu kitakachowezesha. Sasa, pale katika Jumuiya ya Afrika Mashariki hapapatikani fungu lolote linalohusu barabara, hazipo pesa pale!

Hakuna fedha za kutengeneza bandari, hakuna fedha za kutengeneza viwanja vya ndege, ila tunakaa kama Jumuiya ya Afrika Mashariki, tunasema tunataka tuunganishe nchi zetu kwa barabara. Kwa pamoja tunachukua wataalam wa nchi zetu tatu wanakaa. Watanzania wanazungumza miradi ya barabara kwa upande wa Tanzania, Waganda wanazungumzia miradi ya barabara kwa upande wa Uganda na Wakenya wanazungumzia miradi ya barabara kwa upande wa Kenya. Kwa pamoja inaunganishwa inaitwa *East African Road Network.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kikubwa hapa ni kuipa ile Sura ya Ukanda *(Regional Character)* ili unapokwenda kuombea barabara ya kutoka Dodoma mpaka Namanga, unasema barabara hii inakwenda Nairobi na yule wa Nairobi anapokwenda kuomba barabara kutoka *Athi River* mpaka Namanga anaambiwa barabara hii inakwenda mpaka Dodoma, lakini inakwenda mpaka Tanzania. Kwa hiyo, kwa maarifa haya na kwa sababu katika Jumuiya zenye fedha, wanazo fedha zinazoitwa za kusaidia *Regional Integration.* Sasa, fedha za *Regional Integration* huzipati kama hupeleki mradi wa *Regional Integration. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu akianza kusema: “Mbona nimeona barabara, lakini Zanzibar haimo, kwa hiyo hainufaiki kwenye Jumuiya.” Katika dhana hii haipo, lakini kilichoingizwa kwenye mradi wa barabara ni ferry ya kutoka Zanzibar kuja Bara. Mfano, kama Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed anaweza kutoka Unguja pale anapakia gari lake kwenye *ferry* anateremka nalo Dar es Salaam, anakuja zake Dodoma. Akimaliza hapa wakati wa kurudi anapakia gari lake kwenye *ferry* anaenda zake. Lakini sasa hivi hana uwezo huo kwa sababu gari ni lazima libaki Zanzibar, hana namna ya kulivusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mradi wa Barabara za Afrika Mashariki hiyo ndio *project* ambayo imeingizwa kwenye Jumuiya. Lakini katika *infrastructure* kwa maana ya miundombinu tunaangalia barabara, tumeangalia miradi ya mawasiliano ya simu, tunaangalia miradi ya nishati, miradi ya usafiri wa anga, bandari na reli. Kwa hiyo, kila kimoja kina wakati wake. Kama sasa hivi tunashughulikia mradi wa barabara, nina hakika wakati Mheshimiwa Profesa Mwandosya na wenzake watakapokuwa wanashughulikia Bandar, basi na bandari zetu zilizopo Tanzania bila ya kubagua zitakuwepo katika ujenzi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini point ninayoisema hapa jamani, hakuna kitu cha kwenda kutafuta pale Afrika Mashariki ukasema: “Sisi tunapata nini hapa?” Tunatengeneza mazingira, mazingira ambayo uhodari wake ni sisi wenyewe ndani ya nchi zetu kuchemka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tujenge viwanda ili tupate bidhaa za kuuza, tuongeze kilimo ili tupate chakula, maana midomo ya kula ipo tu, au tuongeze kilimo ili twende tukauze. Kule Kaskazini mwa Kenya, Lokchogio ni jangwa tu, ukilima mahindi kuna soko la kwenda kuuza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndio maana ninaliafiki sana wazo la Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed kwamba: "Kwa nini Zanzibar wasiifikirie kuifanya ni kituo kikubwa cha uzalishaji huria na soko lipo?" Lipo soko la Afrika Mashariki, lipo soko la *SADC,* lipo soko la Marekani chini ya *AGOA* na lipo soko la Ulaya chini ya *Everything But Arms (EBA).*

Kwa hiyo, nataka kusema kuwa, jamani nimelieleza kwa namna hii, nadhani tumeelewana kwamba Afrika Mashariki pale hakuna kitu tutakachokwenda kuuliza: "Mimi hapa ninapewa nini?" Jumuiya inakutengenezea mazingira ya kukuwezesha wewe kuongeza uzalishaji mali, kukuhakikishia kwamba ukizalisha soko lipo, ukiongeza huduma soko lipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani hili nimelifafanua vizuri...

**WABUNGE FULANI:** Muda!

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Bado, nitamaliza tu, hili ndio lilikuwa kubwa zaidi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu masuala ya Zimbabwe Mheshimiwa Naibu Waziri ameeleza vizuri. Suala la kuburuzwa tumelieleza vizuri. Pia, suala la uteuzi wa Mabalozi amelieleza vizuri. Kwa kweli Rais anapofanya uteuzi wa Mabalozi, nani anataka kumtupa wapi kwenda kufanya kazi gani ndio kinachoongoza. Kwa hiyo, wakati mwingine mtu fulani kama ana uwezo wa kuwafungulieni milango mahali fulani, hata akiwa yuko mahali fulani mnamwambia: "Bwana tusaidie hapa." Atusaidie kufanya hiyo kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, Mabalozi katika utaratibu wao wa kufanya kazi si kwamba wanaishi milele, wale ambao ni watumishi wa Serikali wanatawaliwa na Kanuni za Utumishi wa Serikali na umri wa kustaafu wa watumishi wa Serikali, lakini kuna wakati ambapo kama anahitajika anaweza kupewa mkataba wa kuendelea nao. Wale ambao si watumishi wa Serikali wanapewa mikataba maalum na mikataba hiyo inaweza kuongezwa inapokuwa hapana budi. Mabalozi kuwa watumishi wa Serikali na wasiokuwa watumishi wa Serikali ni utaratibu wa popote pale duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano sisi hapa Tanzania tumepata Mmabalozi kutoka Marekani mara ya tatu mfululizo ambao si watumishi wa Serikali. Tulikuwa na yule Kasisi, Blood Anderson, halafu alikuja Charles Stith, Kasisi tena, sasa hivi tuna Balozi mfanyabiashara na mwenyewe anasema: *"I am a businessman."* Kwa hiyo, nasema ni utaratibu tu, ni nani anaweza kukufanyia nini. Pengine walipomteua wenyewe waliangalia sasa hivi *we are looking at business interest,* peleka mtu atakayeweza kuifanya kazi hiyo. Kwa hiyo, tunapofanya uteuzi huo muelewe misingi inayotumika. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *NEPAD* kuna haja ya kulifafanua zaidi kwani linaonekana kama ni la Nigeria na Afrika ya Kusini. Ni kweli kwa kiasi fulani inaonekana hivyo. *NEPAD* imeanza vizuri kwa uamuzi uliofikiwa Lome Togo, wakawaambia wenzao wale wanne wafanye kazi ya kutengeneza program na wakaja kuripoti Lusaka, Zambia. Walikuwa ni Rais Obasanjo, Rais Mbeki, Rais Butefrika wa Algeria na Rais Mubarak wa Egypt.

Mheshimiwa Naibu Spika, waliporipoti suala hilo Lusaka na Mzee Wade naye akaja na mpango wake mwenyewe, hakuna mtu aliyemwagiza, anauita *Omega plan,* Viongozi wakasema: "Kwa nini tugombee fito wakati tunajenga nyumba moja?" *Omega plan* na *map* iunganisheni iwe mpango mmoja, tukawa na *New African Initiative (NAI).* *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kule Afrika Kusini jina *NAI* halitamkiki, lina maana mbaya kidogo, ndipo likabadilishwa jina tukaja kwenye *New Economic Partnership For Africa's Development (NEPAD).* Ni mpango wetu wa Viongozi na Viongozi wetu pale Lusaka ndio wakasema: "Ninyi wenzetu

watano muunde *Steering Committee* tutaongeza wenzenu wengine 15. Kwa hiyo, ni mpango wetu sote. Sasa kinachotokea na ambacho kinaleta matatizo ni upashanaji wa habari, wakienda inakuwa tabu sana kupata habari! Kwa sababu hiyo, ndio maana kuna hisia hizo, lakini jamani ni suala letu sisi wote na kilichofanyika ni kuhakikisha tu kwamba sekretarieti iliyokuwa Afrika Kusini ihamishwe na kupelekwa Makao Makuu, Addis Ababa na kwa hiyo, tutakuwa tumeondoa hali hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo suala la ruzuku, wamesema ruzuku sawa na sisi tutoe tu, mtu anatoe nyie mnapiga kelele ya nini! Labda nijaribu kulieleza. Mataifa makubwa haya ndio yanayohubiri biashara huria, kwamba tufungue masoko, tuondoe vikwazo vya kodi na tuondoe vikwazo visivyokuwa vya kodi. Lakini wanapotuhubiria sisi, mnapokuja kwenye soko la mazao ya kilimo wao wenyewe wanaweka vikwazo visivyokuwa vya kodi kwa njia ya ruzuku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mataifa yale kama wasingeweka ruzuku, sisi ndio tungekuwa tunawalisha. Kama wanataka sisi tufungue masoko yetu kwa kuondoa vikwazo, kwa nini wao wanazuia masoko yao kwa njia ya ruzuku? Ndio maana tunasema tunayo haki ya kudai hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika biashara za Kimataifa kwenye nchi zetu sisi, jambo ambalo tuna uwezo nalo kwa maana ya kiuchumi *(at a comparative advantage)* ni kwenye Sekta ya Kilimo. Ukitutoa kwenye kilimo pengine hatuwezi! Mfano, ng'ombe mmoja anapata ruzuku ya Dola 7 kwa siku kule Japan, wewe maziwa unaweza ukaenda ukauza?

**WABUNGE FULANI:** Hapana!

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Eeh, huwezi kuuza!

Mheshimiwa Naibu Spika, ndio maana maziwa yao wanaweza kuuza mpaka Dar es Salaam! Chukua gharama ya kusafirisha maziwa, bado yakija hapa yanauzwa kwa bei ndogo, nasema kinachoifanya yawe na bei ndogo ni kwa sababu ya ile ruzuku. Tunasema ni kitu haramu, siyo halali kama ambavyo mnataka tufungue masoko yetu na wao wafungue na wakitufungulia soko la kilimo ndipo sisi tutakapopata nafuu kubwa na uwezo mkubwa kwa sababu hapa tuna uwezo napo, kwenye viwanda hatuna! Kwa hiyo, ndiyo maana jambo hilo, siyo kwamba kwa sababu na sisi tuweke, hapana. Tunadhani kuna suala la msingi ambalo ni lazima nao watoe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la *Commonwealth,* tumefanya jitihada kubwa ya kuzungumza nao na wanakuja, nadhani Winston Cocks, Naibu Katibu Mkuu, anakuja tarehe 4 na tarehe 5 atakuwepo, tutazungumza kwamba ule ni wajibu wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Magayane amezungumzia ugaidi, matamshi ambayo yametolewa na wakubwa je, hatuwezi kuomba fidia kwa hasara waliyotutia?

Sisi tunachowataka waache tu, wakiacha wala hatuna haja ya kuomba fidia. Tunachowataka ni kwamba, wanapofikiria kufanya hivyo watupe taarifa mapema. Nasema hivyo kwa sababu kama litatokea tukio la ugaidi watakaokufa zaidi ni Watanzania kuliko hao wageni na hiyo ndio experience. Hata mwaka 1998, uzoefu wetu ni kwamba waliokufa pale ni Watanzania, hakuna hata Mmarekani mmoja aliyekufa! Mombasa walikufa Wakenya na Myahudi mmoja. Kwa hiyo, nasema kwamba na sisi tuna interest kubwa sana ya hili na tunao uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Iraq kwamba tuwaambie wakubwa hawa waombe radhi, binafsi nasema hakuna haja, vita vimeisha tuangalie ya mbele tu sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimniwa Naibu Spika, Mheshimiwa Frank Mussati, amezungumzia kuhusu Mkoa wa Kigoma kufidiwa kutokana na wingi wa wakimbizi. Mabadiliko ya ile Sheria tunayoitaka ni kwamba, yaweze kutambua dhamana na mzigo tunaoubeba. Hivi sasa tunaonekana kama vile tunayofanya tunastahili na hatustahili kuomba chochote kile cha kusaidiwa! Unaweza kufika mahali ukakuta wakimbizi kwenye

makambi wanaishi vizuri zaidi kuliko majirani zao! Haya ndio ambayo tunayasema na Sheria ile ikibadilishwa itatoa jukumu la wajibu rasmi kwa Jumuiya ya Kimataifa kusaidia nchi zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya, ameshauri Serikali yetu izungumze na Urusi kuhusu utekelezaji mpango wa kuendeleza soka Tanzania. Anataka kuendeleza soka siyo Simba! Tunao Mkataba wa ushirikiano wa kiutamaduni, kwa hiyo, tukiutumia vizuri haya yote yanawezekana.

Mheshimiwa Aziza S. Ali, amezungumzia usumbufu wa kupata visa katiba Balozi za Marekani na Uingereza. Hilo ni tatizo la kweli. Tunaendelea kuzungumzia nao, lakini Mataifa ambayo yanadiriki kumkamata Rais wa nchi na kumpeleka kwao kwenda kumshtaki wakati mwingine kuzungumza nao ni wagumu sana! Tunaendelea kusema tu, lakini ni wagumu sana kutusikiliza. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mohammed A. Abdulaziz, amezungumzia namna ya kuhakikisha kwamba katika kugawa misaada ya maendeleo, Mikoa inafikiriwa sawa sawa. Binafsi nimesikia na wenzetu wa Mipango na Hazina wapo nao pia wamesikia watalizingatia.
Mheshimiwa Leonard N. Derefa, ameulizia ni kitu gani kinasababisha Ivory Coast na Sierra Leone kuwa na matatizo? Ni ubinafsi wa watu tu, ama wanataka madaraka ama wanataka utajiri. Hayo ndiyo yanayosababisha nchi zetu zinakuwa matatizoni, lakini pia kuna Mataifa makubwa wakati mwingine yanaingilia kati!

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, ameulizia kuhusu mipango ya mtoto wa Idd Amin kutaka kuvamia Uganda kutokea kwa *DRC.* Sisi pia tumesoma kwenye magazetu tu, hatujui kama ni kweli ama si kweli! Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa ameuliza, raia wetu waliojipeleka kwa tamaa zao wenyewe huko *DRC* ili watumikie Jeshi tunawafanyaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, wako wenzetu wamekwenda kule *DRC* kutafuta riziki, lakini tulichosema sisi ni kwamba, utaratibu ule sio sawa sawa. Tunafanya mazungumzo na Serikali ya Kongo. Mheshimiwa Rais alinituma kwenda kuzungumza na Rais Kabila na tukaelewana kwamba, kwa kweli kinachoendelea siyo sawa na kwa hiyo tukawaomba wenzetu wale warudi na Serikali ya Kongo ikafanya uamuzi huo. Tunasikia kwamba wengine wamechukua uraia wa Kongo, sasa unafanyaje tena! Kama ameamua kuikana Tanzania hakuna la kufanya! Lakini tunadhani kwamba haikuwa sawa kwa watu kwenda kufundisha Majeshi katika nchi nyingine bila maelewano ya Kiserikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Semindu K. Pawa amesema, Afrika ilitawaliwa raslimali zake na hivyo kudumazwa, anaomba maelezo zaidi kama tunaweza kupata fidia. Tunaendelea kuyazungumza haya, lakini fidia yenyewe wakati mwingine ni kuiomba kwa kutufungulia masoko tuingize bidhaa zetu bila ushuru, pengine ndio fidia zenyewe. Tumejaribu pale Durban ikawa tabu sana! Mheshimiwa Esha H. Stima amezungumzia kwamba, Watanzania kadhaa wametekwa na kunyang'anywa mali zao wanaposafiri nchi za nje hasa Afrika na mfano ni wa mtu wa Kijiji changu kule Msata. Tunapopata taarifa tunashughulikia, lakini tusipopata taarifa hatuna namna ya kushughulikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Freeman A. Mbowe ameulizia nini kinachotokea Nigeria? Suala letu kubwa huko ni namna gani tutaendeleza biashara. Nafasi ipo, ni vizuri wafanyabiashara wetu tu wachangamke, wakichangamka watapata soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbaruk K. Mwandoro amezungumzia kwamba Maafisa wa Ubalozi wapewe mafungu maalum yenye mwelekeo wa kiuchumi. Hiyo ndio jitihada tunayoifanya, nina hakika tukifanikiwa hayo tutakuwa tumeimarisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

## MATUMIZI YA KAWAIDA

### Fungu 34 - Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kabla ya hatujaanza hatua hii Kanuni ya 81 (2) (a) kinataka katika hatua hii tuhoji kifungu kwa kifungu. Sasa kama mlivyoona wote inabidi tuhoji vifungu vya Balozi zote za dunia nzima. Sasa tunaweza tukachelewa. Bahati nzuri Mheshimiwa Spika, alituwekea utaratibu tulikuwa na hali hii wakati wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kulikuwa na vifungu vingi. Kwa hiyo, aliweka utaratibu ambao ni vema leo tukaufuata wa kuhoji vifungu kwa jumla na yeyote ambaye atakuwa na hoja yoyote, basi anaweza kusimama kama hakuna tumalize badala ya kuhoji Balozi kwa Balozi dunia nzima. *(Makofi)*

Fungu 34 - Wizara ya Mambo ya Nje na
Ushirikiano wa Kimataifa ... .... Sh. 32,079,101,100/=

**MHE. KILONTSI M. M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipochangia asubuhi nilizungumzia habari za watu ambao wameuwawa na Majeshi ya Burundi nikaomba maelezo ya Serikali ambayo ni tofauti kidogo na yale ambayo tumekuwa tunaambiwa Burundi hakuna Serikali, Burundi kuna Serikali ya Mpito kwa ajili ya kutaka kuelewa hivi tunachokisema kwa wananchi ni kitu gani? Tunawaeleza hivyo wanatuambia hakuna Serikali au kuna Serikali ya Mpito haiwezi kudaiwa nakadhalika? Au tunakwenda kwenye Jumuiya ya Kimataifa kudai fidia hiyo? Au Serikali inatusaidiaje ili kulinda usalama wa raia wake? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NCHI ZA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti napenda kutoa maelezo ya Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi. Ni kweli kulikuwa kumetokea matukio fulani wakati mmoja ambapo baadhi ya raia wetu waliokwenda kufanya biashara ndani Burundi, ambalo ni jambo la kawaida linatokea kila siku raia wa Burundi wanakuja kwetu katika masoko ya mpakani na watu wa kwetu wanakwenda kwao. Walipokwenda watu wetu kule watu watatu walikamatwa na wakatekwa nyara. Mkuu wa Mkoa wa eneo lile kwa upande wa Burundi alipotakiwa kujibu kwa nini watu wetu wamekamatwa waachiliwe, akajibu hoja akasema hatutawaachilia mpaka ng'ombe walioibiwa Tanzania waachiliwe. Likazusha kidogo mtafaruko na ulikuwa ni uamuzi wake mwenyewe, halikuwa agizo kutoka Serikali ya Burundi na sisi tukachukua hatua tukazungumza na Serikali ya Burundi na watu wetu wakaachiliwa wakarudishwa nyumbani. Lakini hawakukamatwa ndani ya Tanzania walikamatwa ndani ya Burundi. Vile vile ni kweli kwamba katika matukio ya mpakani zipo kesi mbili/tatu kama alivyozungumzia Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, asubuhi kwamba hatimaye baadhi ya raia wetu waliuwawa. Anauliza je, tunafanya nini ili kufuatilia haki zao na hasa haki za familia zao? Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, pamoja na Kamati yako tukufu, kwamba hatupuuzi wala hatudharau na tunaendelea kutetea haki za Watanzania. *(Makofi)*

**MHE. KILONTSI M. M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake. Naomba niweke rekodi sahihi. Katika wale watu watatu ni mmoja tu aliyekamatwa Burundi, wawili walikamatwa nyumbani kwao ndani ya Tanzania na Majeshi ya Burundi, wakapelekwa kupita bondeni kwenye mito wakavushwa mpaka Burundi wakapelekwa makambini. Ndicho nilichokuwa nasema. Mimi nilipenda nipate kauli ya Serikali katika hili kwamba tunawaeleza nini wananchi kule?*(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NCHI ZA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawaeleza nini Watanzania wale? Tatizo limetokea na Naibu Waziri amelisimamia yeye mwenyewe. Tulimwita Balozi wa Burundi tukamweleza tatizo hilo na taratibu za kidiplomasia. Baada ya jitihada hizo raia wetu wale wakaachiliwa. Mauaji kila yanapotokea tunapopata Serikali tunawapelekea wenzetu *notes* za masikitiko, malalamiko na yote hayo tumeyafanya. Hatuna maelezo zaidi ya hayo juu ya hatua tulizozichukua, vingine tunaweza tukasema basi kama nao wameua wawili na sisi tuue watatu, hatuwezi kufanya hivyo na hatukusudii kufanya hivyo. Kwanza tunaomba Mheshimiwa Mbunge atuamini kwamba tunafanya jitihada kubwa na jitihada tulizozifanya ndiyo maana wale watu wakaachiliwa. Wale wameshakufa, ndiyo wamekufa hatuna namna ya kurudisha maisha yao. Kwa hiyo, tuseme tu kwamba ni hayo na kama ya kusema basi aende akawaambie tu kwamba Serikali

inajitahidi na tunakwenda kuhakikisha usalama wao unakuwepo, jeshi letu lipo pale, kama kuna lazima hatutafikia kwenye hatua hiyo, lakini yapo yanayotokea mimi nadhani yatatokea hakuna namna ya kutokea lakini kila linapotokea Serikali imekuwa inachukua hatua kama tulivyojieleza. Kwa hiyo, tutaendelea kuchukua hatua na tutaendelea kuchukua hatua na tutaendelea kufanya jitihada kuhakikisha usalama wa wananchi wa mpakani. *(Makofi)*

**MHE. JACKSON MAKWETTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kweli nasimama hapa kuomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu wanielewe nia yangu nzuri kwamba Tanzania mwaka 1964 iliomba na *OAU I-set land* kwa ajili ya ukombozi na kwamba makambi niliyoyataja kwa Historia ya Afrika ya Tanzania inaweza ikafutika kabisa. Nimependekeza kwamba Wizara ichukue jukumu hili kwamba kwa kuwa *OAU* ndiyo iliyoomba hivi na sasa ni *AU* ipeleke agenda ili tujenge *monument* ya kumbukumbu ya *liberation* ya Afrika katika Tanzania. Najua muda haukuruhusu lakini nadhani wazo linaeleweka, naomba kauli kutoka Wizarani.

**WAZIRI WA MAMBO YA NCHI ZA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa sababu ya muda mdogo hatukuweza kumjibu kila mmoja. Lakini wazo ambalo ni zuri tumelipokea. Hata hivi sasa katika matayarisho yetu ya *SADC* moja ya mambo ambayo tumekuwa tunajaribu kuyafikiria hatujafikia mwisho ni kwamba ikiwezekana tuitumie nafasi hii ya Mkutano wa *SADC* ambapo watakuja viongozi wengi wa nchi ambazo zimeanzia hapa kwamba pengine tungeweza kuwa mnara maalum Kongwa na tukaitumia nafasi hiyo ku- *inaugurate.* Tatizo lake kubwa ni namna ya kuiwinisha ratiba hiyo na umbali uliopo Kongwa na Dar es Salaam, ambako mkutano unafanyika. Lakini nasema hata kama tutashindwa kwa kipindi hiki lakini tunayo dhamira hiyo. Tumeshakuwa na mazungumzo na nchi zetu za *SADC* na hasa zile nchi ambazo viongozi wake wameanzia hapa, juu ya namna ya kuhifadhi kumbukumbu zetu. *(Makofi)*

Kwanza kuandika historia yenyewe kwa sababu wale waliohusika sasa wameanza kufa wengi, Mwalimu hayupo, Samora hayupo, Chris Han amekufa, Josiah Tongo Gara amekufa, Mzee Sisuru alitumia muda mwingi sana *Roben Island,* lakini wale ambao walikuwa hasa kwenye harakati yenyewe wengi wale wenye hizo kumbukumbu wameanza kufa. Juzi amekufa Yomo Disse. Kwa hiyo, wanaanza kufa wengi. Katika mazungumzo yetu tumezungumza kwamba tutapata nafasi ili tuzungumze tunafanyeje kuihifadhi kumbukumbu hii. Nachingwea tangu KJ 17 pale, sasa kambi ile zamani Jeshi letu lilikuwa liko pale. Lakini sasa hivi jeshi limeondoka kwa hiyo yale majengo ambayo walikuwa wanakaa wenyewe hawapo sasa yanaanza ku-*disintegrate.* Tulipokuwa Maputo nilizungumza na Waziri wa Ulinzi wa Mozambique ambaye amesema atakuja huku na moja ya mambo ambayo tumeyazungumza ni kwamba ni namna tutaihifadhi historia hii. Kwa hiyo, ni jambo ambalo tumeliafiki na pengine tukipeleka njia ya *African Union* ni njia ndefu sana bado tunaweza kutumia njia ya *SADC* ambako wenyewe hasa wahusika wapo na itakuwa ni rahisi zaidi. *(Makofi)*

*(Fungu lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MAMBO YA NCHI ZA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imeyapitia Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ya mwaka 2003/2004 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila ya mabadiliko. Hivyo naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako tukufu liyakubali makisio hayo. Naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*Makadirio ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa Kwa mwaka 2003/2004 Yalipitishwa na Bunge.*

*(Saa 01.15 Usiku Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Jumatano Tarehe 30 Julai, 2003 Saa Tatu Asubuhi)*